# F3 TOPICAL REVISION
# KISWAHILI

***A SERIES OF TOPICAL QUESTIONS IN FORM THREE KISWAHILI***

***FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657***


**MR ISABOKE 0705525657**

# INSHA

## 1.INSHA ZA KIUAMILIFU

1. Suala la ufisadi limekuwa tatizo sugu katika jamii ya Kenya. Andika mahojiano kati ya mwenyekiti pamoja na Afisa wa Sheria katika Tume ya Kupambana na Ufisadi nchini na mwandishi wa habari juu ya mbinu za kupambana na ufisadi.

2. Mkuu wa mkoa wa Tuinuane ameongoza mkutano wa viongozi mkoani uliojadili kuhusu amani na maridhiano baada ya vita vya kikabila mkoani humo. Andika kumbukumbu za

   mkutano huo

3. Matokeo ya mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne yametangazwa. Imesadifu kwamba wewe ndiye mwanafunzi bora katika Mkoa wa Magharibi. Mwanahabari wa Gazeti la Tujivune amekutembelea nyumbani kwenu. Andika mahojiano yenu.

4. Wewe ni Katibu wa kamati ya chama cha wazazi na walimu shuleni mwenu. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanyika hivi karibuni.

## 2.INSHA ZA KAWAIDA

1. Wewe kama Mwalimu ambaye amehitimu katika chuo kikuu cha Kenyatta, kuna nafasi ya kufundisha katika shule ya upili ya Angeko. Andika wasifu-kazi utakaoandamana na barua yako.
2. Mgema akisifiwa tembo hulitia maji.
3. Vizingiti \Vikwazo vya kuundwa na kupatikana kwa katiba mpya nchini Kenya sio wanasiasa pekee.Fafanua.

4. Andika insha itakayomalizikia kwa: **. . .** Na katika uchaguzi wa marudio uliofanywa baada ya kisa hicho, Hidaya akapata ushindi mkubwa na kuwa mbunge wa eneo bunge la Kubali.
5. Mchama ago hanyeli, huenda akauya papo
6. Uavyaji wa mimba ni suala sugu hapa nchini Kenya. Jadili
7. Ilikuwa mara ya kwanza kufikishwa mahakamani…………….. endeleza
8. Kisa cha mwanafunzi kilingane na chanzo hiki na aonyeshe ubunifu na matumizi mazuri ya lugha
9. Eleza jinsi haki za watoto zinavyokiukwa katika jamii huku ukipendekeza suluhu.
10. Cha Mchama huchama, cha Mgura hugura.
11. Rais Julius Kabarage Nyerere ni mtu anayejulikana katika taifa la Afrika kusini na Mataifa mengine. Alipozaliwa.............................................................................
12. Shughuli ya kuavya mimba iharamishwe. Jadili
13. Ganga ganga ya mganga humlaza mgonjwa na matumaini.

# UFAHAMU

**1.** ***<u>Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:-</u>***

Kitabu kinaeleza Mungu kamuumba mwanamke kutokana na ubavu tu wa mwanamume. Na hapa bila shaka ndipo linapojisalimishia shina lisilokuwa na mzizi thabiti la ubinafsi wa kiume – mwanamume akijijadilia kimoyomoyo. Ikiwa huyu mwanamke alitokana na ubavu wangu, yeye awe nani kwangu? Hakuna shaka ni wangu, mali yangu. Kwa sababu hii, miaka nenda miaka rudi mwanamke amekuwa akiugua na kuguna chini ya uonevu wa mwanamume.

Swala la kitabu kumleta duniani mwanamke kupitia ubavu wa mwanamume laweza kueleweka katika muktadha wa kile ambacho kimekuja kujulikana kama taasubi ya kiume. Na ili tuelewane barabara kuhusu maoni haya, tujisitishe kidogo katika kunusa tumbako huku tukijiuliza: ni nani au ni kina nani walihusika katika kubuni au kuandika hadithi ya asili ya mwanamke kitabuni? Ni kawaida ya binadamu kutazama na kueleza jambo kibinafsi. Asili ya mwanamke ilivyoelezwa kitabuni katika mkururo wa fikra hii yaweza kutambulikana kama uzushi tu.

Kiutamaduni, hasa wa Kiafrika, huku akiwa yuakua, mtoto wa kike husombezewa kasumba ya mawazo akilini, na kwa bahati mbaya sana, aghalabu na mamake au nyanyake, kuhusu namna anavyotarajiwa kutabasamu, kujinyenyekeza, na jumla kujidunisha mbele ya mvulana. Ni mwiko kwake kudhihirisha tabia za kimabavu, sitaji kujitetea, ili asije **<u>akatiwa mdomoni</u>** mitaani! Msichana atacharazwa na wazazi wake kwa ujasiri licha ya kuthubutu kupigana na mvulana. Na hapo ndipo ilipojificha siri ya kuwa anapoolewa na akosane na mumewe, daima yeye hutolewa makosa na kupatikana na hatia mbele ya wazee.

Wavulana kwa upande wao ni wanaume na lazima afanye mambo kiume. Si ajabu kuwa kinyume cha yale yanayowafika wasichana, wavulana wengi **<u>huonyeshwa mbovu</u>** na baba zao kwa sababu wamepigwa na wenzao. Ni vibaya baba kusikia mtoto (mvulana) wake amepigwa.

Nyumbani msichana hutarajiwa kujilindia heshima kimwili hasa kwa kuhifadhi ubikira mpaka aolewe. Anapotembea na wanaume huitwa Malaya. Ni ajabu kuwa hakuna bikira wala Malaya mwanaume. Mvulana ambaye hajajuana kimwili na mwanamke kabla ya ndoa huchukuliwa kuwa zuzu; ilhali anayetembea ovyo na wanawake ndiye dume.

Fauka ya hayo, inasikitisha kabisa kuwa mwanamke hana mahali pa kutua kikamilifu duniani. Kabla hajaolewa nyumbani, huchukuliwa kuwa mpita njia tu. Na anapoolewa ni poa kaolewa. Isitoshe mwanamke huolewa, haoi wala yeye na mume hawaoani. Mwanamke mahali pake ni jikoni pia anaonekana tu; ni hatia kwake kujaribu kusikika.

Mkutano kuhusu mwongo wa wanawake uliofanyika miaka miwili iliyopita jijini Nairobi ilinuiwa kupalilia vizuri mwamko juu ya ukweli kuwa binadamu ni binadamu na hakuna haja ya wao kubaguana. Tofauti za kimaumbile haziwezi kuwa hoja. Tusiupigie makelele ubaguzi wa rangi huko Afrika kusini ilhali kwetu tuna ubaguzi wa kimaumbile. Tusipozingatia ushauri huu daima tutakuwa kwenye kile kinaya cha kuchekwa katika muktadha wa methali kuwa **<u>nyani haoni ngokoye</u>**.

Ni kweli kosa lilifanyika tangu awali ambapo kufumba na kufumbua, mwanamke akapigwa jeki na kuachwa akilewalewa katika hali ambayo hangeweza kujitetea hivyo basi

akachukuliwa kuwa kiumbe duni. Lakini haidhuru, **yaliyopita si ndwele**, tugange yajayo. Kinachohitajika ni wanawake kuwa na nia na msimamo imara. Ni lazima wajifunge kibwebwe na kujitoa mhanga na kupambana dhidi ya taasubi ya kiume.

**Maswali**

(a) Andika kichwa kinachofaa kutokana na taarifa uliyoisoma
(b) Taasubi ya kiume ilianzaje?
(c) Katika utamaduni wa mwafrika ni kasumba gani anayosombezewa mtoto wa kike anapokua?
(d) "**Wavulana walidekezwa na utamaduni".** Eleza
(e) Taja kwa ufupi mambo muhimu yaliyoshughulikiwa katika mkutano wa mwongo wa wanawake mjini Nairobi
(f) ***Eleza maana ya semi zifuatazo kama zilivyotumiwa katika taarifa uliyosoma:-***
(i) Nyani haoni ngokoye .
(ii) Akatiwa midomoni
(iii) Huonyeshwa mbovu
(iv) Wajifunge kibwebwe
(v) Yaliyopita si ndwele ganga yajayo

**2.** ***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali***

Asifuye mvua imemnyea. Huu ni msemo wenye hakika isiopingika, na kutilia shaka ni sawa na kudai jua linaweza kubadilika na kuchomozea upande wa magharibi badala ya mashariki. Huu ndio ukweli uliodhihirika juzi katika vyombo vyetu vya magazeti.

Lisemwalo lipo, na kama halipo li njiani. Waama, pafukapo moshi pana moto. Mwanafunzi mmoja wa kike kwa jina P.N. katika chuo kikuu kimojawapo nchini alishangaza umma wa Kenya na ulimwengu kwa jumla alipodai kuwaambukiza wanafunzi wenzake wa kiume mia moja na ishirini na wanne virusi vya Ukimwi.

Kisa na maana? Aliambukizwa Ukimwi na mwanafunzi mwenzake aliyekuwa akifanya majaribio ya ualimu katika shule yao ya upili. Baada ya kushawishika sana alijuana naye kimwili, na matokeo yakawa kifo ambacho sasa alikuwa anawagawia wenzake.

Kisa kama hiki kinachangia kueleza kina **kirefu cha kutamauka** na upweke ambao maisha ya waja wengi yameingia kiasi cha kuwaacha wanyama ijapo wanaenda kwa miguu miwili bado. Katika mojawapo ya mafunzo ya kidini ambayo Padre alinifunza mimi na wanafunzi wenzangu, tuliambiwa kisasi ni chake Mola, sisi waja wetu ni kushukuru tu. Mbona basi mwanafunzi kama huyu kutaka kulipiza?

**Ima fa ima**, na waswahili husema, "mlaumu nunda na kuku pia". Huyu mwanafunzi hawezi kuachiwa atende alivyotenda. Aliyekula naye raha alikuwa mtu aliyefahamika vizuri sana kwake. Isitoshe, huenda wakati huo alikosana na mama na baba kulala nje. Huenda alikosana na ndugu zake kwa kuepa nyumbani usiku wa manane kwenda kumwona huyu kalameni. Huenda alikosana na mwalimu wake kwa sababu kiburi kilianza kuingia. Kwa vyovyote vile, alikula raha na hastahili kuwaadhibu watu wasio na hatia **kufidia makosa yake**. Je, kama yeye na huyo jamaa wasingekuwa na Ukimwi, raha kiasi gani wangezila hadi leo?

Jamii na watu wote kwa jumla hawana budi basi kulaani vitendo vya P.N. vya kuambukiza wanafunzi wenzake virusi huku akijua. Hili ni kosa ambalo linastahili adhabu ya kifo. Dawa ya moto ni moto ni adhabu inastahili kuchukuliwa haraka ili P.N. ambaye tayari amekiri hatia, atiwe nguvuni na adhabu itolewe.

Barua ya P.N. inafafanua jambo jingine sugu. Kwamba kiwango cha maadili katika vyuo vyetu kimezorota kiasi cha kufanyiana unyama usiosemeka. Vijana wengi siku hizi wanashiriki tendo la ndoa bila haya. Huu upotofu wa maadili katika jamii wapaswa kushutumiwa na wote. P.N. hana sababu yoyote ya kibinadamu, kidini au kitu chochote kile kudai haki kwa uovu huo wake.

**Maswali**

1.Taja kichwa kwa makala haya

2. Katika aya mbili za kwanza, mwandishi anamlaumu mwanafunzi kwa kosa gani?

Eleza chanzo cha tabia za P.N

4. Mwandishi wa taarifa hii anataka P.N achukuliwe hatua gani? Kwa nini?

5. Barua ya P.N. bila shaka imeonyesha uvumbuzi mpya. Utaje

6. Eleza maana ya vifungu hivi kama vilivyotumiwa katika taarifa:

(a) Kina kirefu cha kutamauka

(b) Ima fa ima

(c) Kufidia makosa yake

3. ***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali***

**CHIMBUKO LA USHAIRI**

Ushairi ni fani kongwe kama mwanadamu mwenyewe alivyo mkongwe duniani. Na mashairi yamekuwepo kitambo sana hata kabla ya lugha ya Kiswahili bado haijanawiri na kushamiri kama ilivyo hivi leo. Ndipo tunasikia kuna mashiri ya kipemba, mashairi ya kimvita, mashairi ya kivumba, mashairi ya kipate, mashairi ya kiyunani, ya kirumi na kadhalika,. Almradi kila jamii na kila kabila lilikuwa na mashairi yake.

Katika utafiti na kongomano zao, wataalam wa arudhi za Kiswahili asili wamechambua na kufafanua kwamba mashairi ya Kiswahili asili yake ni nyimbo za jadi zilizokuwa zikiimbwa na manju, wangoi au waimbaji stadi wa tangu na tangu walipojumuika katika matukio na hafla mbalimbali kama za jando, arusi, matanga, ngoma na shangwe zao za maishani.

Nyimbo hizi zilitumiwa na watangulizi wetu, kidhamira hazikuhitalafiana hata kidogo na mashairi ya Kiswahili tunayohimiza wakati huu. Farka iko katika lugha na umbo kwani kila jamii ilitumia lugha yake na lahaja ya mazingira yake. Na kwa upande wa umbo, tungo hizo za awali kabisa hazikuwa na sanaa kwa maana ya ushauri tunauona leo. Bali tungo hizo zilijengeka katika nguzo mbili kuu. Kwanza ni uzito wa mawazo maadilifu ambayo yalitaamaniwa sana. Na pili ni mizani ya sauti ya manju kulingana na lahani, pumzi zake pamoja na madoido katika uimbaji ambao ulikuwa burudani naathari katika noyo za wasikilizaji wake.

Kwa kifupi ni kwamba, nyimbo hizo ziliuhifaid umma kwa njia mbili, mawaidha kwa mapana na taathira au jadhba kutokana na sauti tamu ya manju.

Kama utakubalika, basi huo ndio ushairi wa awali kabisa ullioambatana na nyimbo zetu za kienyeji. Kila kabila katika nchi zetu lilikuwa na ushauri wake au nyimbo zake zenye undani uliolenga sababu maalum na tukio maalum katika jamii.

Nyimbo kama hizo kwa jina la sasa tunaweza kuita mashairi ndizo zile zilizoitwa 'mwali' na wakamba; gichandi kwa 'wakikuyu'; 'gigia gi sigele' kwa waluo na 'wagashe' kwa wasukuma zilikuwa na undani wa kipekee tena uliodidimia ambao si bure kutolewa hadharani.

Aina za mashairi ya watu wa mwambao ni kama lelemama, misemele, gungu, nyiso, kongozi n.k.

***(Walla Bin Walla – Malenga wa Ziwa Kuu , E.A.E.P)***

1. Ni nini haswa chimbuko la ushairi?

2. Kulingana na kifungu hiki, ni nini umuhimu wa ushairi ?

3. Ni maswala gani yaliyowapendeza wasikilizaji wa tungo hizo za zama ?

4. Tofauti kati ya nyimbo za zama na ushairi wa leo upo kwenye vipengele gani viwili ?

5. Kifungu : '**haijanawiri na kushamiri'** ina maana gani katika lugha nyepesi ?

6. **Eleza maana ya :**
   (a) Kongamano …
   (b) Jadhiba
   (c) Farka
   (d) Awali..

4. ***<u>Soma taarifa hii kisha ujibu maswali</u>***

Chamkosi alipiga goti huku machozi yakimdondoka njia nne nne. Mbele yake, palikuwa na makaburi mawili. Waliokuwa wamelala mle hawakuwa na habari juu ya kihoro na simanzi ya aliyepiga magoti pale. La kwanza, lilikuwa kongwe kiasi na lilikuwa limemea vichaka na magugu. La pili lilionyesha upya kwani shada za maua zilizowekwa na waombolezaji zilikuwa bado kukauka. La kwanza, ndimo babake mzazi alipolala. Nalo la pili, ndimo mamake alimolazwa kiasi cha siku mbili zilizopita.

Kwa Chamkosi, maisha hayakuwa na maana tena. Alikuwa mwanafunzi wa miaka kumi na miwili. Hakuwa amehitimu kujitegemea na kukimu mahitaji yake. Aliokuwa akiwategemea sasa wamemwacha akiwa yatima. Hakuna yeyote ambaye angejaza pengo la wazazi wake wawili kwa kipindi cha mwaka mmoja. Haya yalikuwa kama donda sugu lisilopona.

Kwa sasa, Chamkosi anayakumbuka mengi. Anakumbuka maisha ya babake. Alikuwa jibaba nene, zito lenye sura jamala na sifa nzuri. Baba mtu alikuwa na chake na alijiweza kiuchumi. Wengi pale mjini walimheshimu na kumstahi kutokana na uwezo wake wa kiuchumi. alitunza familia yake vizuri. Chamkosi hakumbuki siku moja aliyokosa chochote alichohitaji kutoka kwa babake. Alikuwa na bidii kazini mwake pia.

Walakini, kama mja asiyekamilika, baba mtu alikuwa na dosari moja. Aliyapenda maisha ya anasa na kufukuzia wasichana wadogo pale mtaani. Mamake Chamkosi aliyajua haya. Alijaribu kuzozana na mumewe ili aachane na tiabia hizi lakini kila akitaka ushauri,

mama mtu alikemewa na kufokewa kuwa aache upuzi wa wanawake. Akafikia kufyata ulimi na kumwachia Mungu aongoze maisha ya bwanake.

Hata hivyo hakuna marefu yasiyo na kikomo. Baada ya kuponda raha na vimada si haba, baba mtu alianza kuugua. Maradhi yake yakawa ni msururu. Mara, alipata mafua yasiyopona, mara kuendesha, mara maradhi ya ngozi. Haya yalimtia wasiwasi. Baada ya kukaguliwa na daktari, alipatikana kuwa *ameumwa na mbuzi*. Hakuamini haya. Baba aliyekuwa bashasha na mcheshi aliingiwa na upweke na kutotaka kutangamana na yeyote hata jamaa zake.

Waliosema kuwa hakuna msiba usiokuwa na mwenzake, hawakukosea. Maradhi ya baba mtu yaliifilisi jamaa huku waking'ang'ania kumtafutia tiba. Wakaenda kwa waganga si haba. Waganga nao wakafaidi tamu.

Muda si mrefu, mama mtu naye akaanza kuugua. Baada ya uchunguzi, alipatikana kuwa na maradhi yayo hayo ya bwanake. Ikawa ni kama mji umelogwa. Baada ya muda mfupi baba mtu aliaga dunia, mama naye hakukawia. Naye akasalimu amri na kumfuata bwanake kaburini. Familia ikawa kama inaangamia. Chamkosi kijana mdogo akaachwa pweke.

Kama kawaida, mja hakosi neno. Wengi walisikika wakisema hili na lile kuhusu vifo hivi. Wengi walieneza uvumi. Lakini, Chamkosi alijua ukweli wa vifo vya wazazi wake.

Sasa hapa alipo aliyatambulia macho makaburi ya wazazi wake, anasononeka. Anaomboleza zaidi kifo cha mamake ambaye alimwona hana hatia na hakupaswa kufa kwa maradhi yale. Anaukumbuka vizuri wema wa mamake usio na kifani. anakumbuka alivyojitunza kama mke na mzazi.

Anakumbuka jinsi mamake alivyomshughulikia babake katika siku zake za mwisho licha ya baba mtu kuungama maisha yake maovu. Chamkosi alishindwa kujua kwa nini mamake akawa msamehevu kiasi hicho. Hakukosa kukumbuka wasia wa mama yake. Haya yalimfariji. Faraja hizi zilimpa nguvu mpya za kuyakabili maisha.

Chamkosi aliwaza juu ya maisha yake. Akaona kuwa, kama yatima atawategemea wafadhili miongoni mwa jamaa na marafiki wenye huruma iwapo wapo. Aliwaza jinsi anasa za babake zilivyowaathiri watu wengi.Alitambua kuwa Ukimwi haumwathiri aliyeupata tu, bali na wengine wengi. Kweli, mtego wa Panya huingia waliokuwemo na wasiokuwemo. Lakini akiwatazama watu, hakuelewa kwa nini walidhamiria kuishi ujingani. Aliwaona baadhi ya vimada wa babake wakishikana viuno na vijana wadogo. Akawasikitikia. Akabaki na swali kwa nini watu wengine wanafikiria kuwa virusi hivi haviwezi kuwapata. Kwani wanafikiria kuwa vinabagua na kuwa wao hawahatarishi maisha yao? Alishindwa kufahamu watu watabadili vipi mienendo yao miovu na waweze kukabili janga hili lini?

Kwa wakati huu, Chamkosi alikata shauri kusomea Taaluma ya Uelekezi na Ushauri kutokana na vifo vya wazazi wake. Alitaka kupata ujuzi utakaomwezesha kuwashauri na kuwaelekeza vijana wenzake ambao wanahatarisha maisha yao. Kama mshauri, alinuia kuhamasisha na kuzindua jamii juu ya hatari za Ukimwi.

Alitaka kuhakikisha kuwa hatua zimechukuliwa na kila mtu katika jamii kukabili janga hili n kuliangamiza

Chamkosi aliomba dua fupi. Akainuka na kuondoka huku akiwa na faraja na matumaini moyoni kutokana na azimio lake lile.

(a) Toa kichwa mwafaka kwa makala haya

(b) Eleza madhara mawili ya ugonjwa sugu uliotajwa katika makala haya

(c) Taja mifano ya tabia zinazoweza kumfanya mtu aathiriwe na ugonjwa wa Ukimwi

(d) Tofautisha tabia za baba na mama wa Chamkosi

(e) Chamkosi baada ya kufikwa na madhila hayo yote aliamua kufanya nini? Toa maoni

(f) ***Eleza maana ya:***

(i) Tumbulia macho
..........................................................................................................

(ii) Ameumwa na mbuzi..........................................................................................................

**5. UFAHAMU**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***.

Watoto wamekuwa wakiteswa na kusumbuliwa sana kwa miaka mingi. Wengi wao wamekuwa wakinyimwa chakula, kukosa elimu, kuishi katika maisha ya dhiki na kufanyizwa kazi ngumu.

Lakini hapana msiba wa milele. Hali hii imeanza kubadilika baada ya ulimwengu mzima kutambua umuhimu wa haki za watoto.

Takriban mataifa yote ya ulimwengu ambayo ni wanachama wa umoja wa mataifa isipokuwa Somalia (ambayo haina serikali kuu) na Marekani yametiana saini makubaliano kuhusu haki za watoto. Makubaliano hayo yalifikiwa katika mkutano mkuu wa Umoja wa mataifa uliofanyika mwaka wa 1989. Hata hivyo, utekelezaji wenyewe wa makubaliano hayo ulianza mwezi wa Septemba mwaka wa 1990. Je, haki hizo za watoto ni zipi lakini? Haki za watoto zinaweza kupangwa katika makundi manne makuu ambayo ni: haki za kukua, haki za kuishi, haki za kulindwa na haki za kushiriki.

Haki ya kimsingi kabisa ni ile ya kuishi. Mtoto yeyote hawezi kufurahia haki zozote zile asipokuwepo, lazima awe hai. Maisha ya mtoto hayapaswi kukatizwa na chochote kile. Lazima ziwepo juhudi za kupinga vitendo vyovyote vinavyotishia maisha ya mtoto. Aidha, lazima mtoto atunzwe ipasavyo kimatibabu.

Haki nyingine ya watoto ni ile ya kulindwa. Aghalabu ulinzi wa mtoto hufanyika katika familia. Lakini sio watoto wote ambao wana bahati ya kuwa na familia inayoweza kuwapa ulinzi ufaao. Hawa wanapaswa kulindwa na kutunzwa na familia nyingine au na taasisi ambazo zinahusika na watoto. Ulinzi huo lazima ufungamane na sheria na utamaduni wa mtoto anayehusika. Mtoto pia ana haki ya kulindwa dhidi ya ajira ya watoto ambayo inawahusu watoto wanaofanya kazi wakiwa na umri wa chini ya miaka kumi na sita. Kazi huathiri ukuaji wa akili, kimwili, kijamii na hata kimaadili kwa mtoto anayehusika. Isitoshe, lazima mtoto alindwe dhidi ya mateso, dhuluma, adhabu na kunyimwa haki na uhuru wa aina yoyote ile. Kwa mfano, haifai mtoto kuadhibiwa kwa hukumu ya maisha au kif'ungo cha maisha gerezani. Mtoto anapaswa kulindwa pia dhidi ya kubaguliwa kwa misingi yoyote ile, majanga, kulazimishwa kushiriki vitani na kuteswa kwa sababu ya maumbile yake. Pia tunapaswa kuhakikisha kuwa mtoto hateswi wala kudhulumiwa kwa sababu ya utamaduni fulani. Kwa mfano, zipo tamaduni zinazowalazimisha watoto wa kike kuolewa mapema au hata kupashwa tohara.

Haki nyingine kwa mtoto ni haki za maendeleo. Msingi mkubwa wa maendeleo ni elimu. Mtoto aliyepata elimu bora anaweza kuzielewa na kuzifurahia haki nyinginezo kwa njia nzuri na akawa anaishi maisha mazuri. Suala hili la maendeleo lazima lihusiane pia na uhuru wa kuweza kutambuliwa na kupewa utambulisho bila kubaguliwa.

Mwisho kabisa kuna haki ya kuishi. Haitoshi tu kuweza kuishi bali pia lazima mambo mengine muhimu yazingatiwe. Kwa mfano mtoto ana haki ya kupata habari kuhusu mambo mbalimbali yanayomhusu na kuhusu jamii yake. Habari ni msingi mkubwa wa kuwa na uwezo wa kujielewa. Mtoto anaweza kupata habari hizi kwa njia mbalimbali kama kupitia vyombo vya habari, kwa kupitia kompyuta n.k. Hata hivyo lazima mtoto huyo alindwe na picha au habari zinazoweza kumpotosha. Mtoto pia anao uhuru wa kushiriki na kujumuika na wenzake na hata kujiunga na vikundi vingine anavyopendelea. Haki hii ya kuishi haikamiliki bila ya kuwapo kwa haki ya kufikiri na kutoa maoni na hata kafanya maamuzi.

Jamii yetu inapaswa kushirikiana bega kwa bega kuhakikisha kuwa watoto hawatendewi dhuluma ya aina yoyote. Asilimia kubwa ya jamii zetu ni vijana ambao ndio tegemeo la jamii ya

kesho. Ikiwa tunataka kuujenga msingi imara na mzuri wa jamii hiyo ya kesho, pana umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kuwa tumewatunza watoto vizuri.

***Maswali:***

1. i). Toa anwani itakayofaa sana kwa taarifa hii.. (Alama 2)

ii). Kifungu. "hapana msiba wa milele" ina maana gani kulingana na taarifa hii?(Alama 2)

iii). Je, ajira ya watoto ni nini? (Alama 2)

iv). Ajira ya watoto huwaathiri vipi? (Alama 2)

v). Maendeleo ya mtoto hayawezi kunawiri bila uhuru. Thibitisha (Alama 2)

vi). Mtoto atasaidiwa na nini ili aweze kupanua akili yake vizuri? (Alama 2).

vii) Msingi mkubwa wa maendeleo katika taarifa hii ni nini ? (Alama 1)

viii) Eleza maana za

2. -Takribani (Alama 1)

3. - Tia Saini (Alama 1)

**6. Soma tarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Jamii yoyote ile ulimwenguni haiwezi kukua, kuimarika na kuendelea bighairi ya kuwatunza na kuwaenzi watoto wake. Watoto ni mbegu ya jamii ya kesho na kama mbegu hiyo haikutunzwa ipaasavyo jamii ya kesho haitakua na endapo itakua itadumaa na kushindwa kuendelea. Ili kuhakikisha kuwa watoto wametunzwa ipasavyo, inaijuzu jamii nzima kufanya kulihali kuhakikisha kuwa watoto wake wamepata elimu ifaayo, afya inayowastahiki, ulinzi murua na usalama unaostahili. Jamii hiyo lazima ithamini haki za kibinadamu alizo nazo mtoto.

Serikali zote uilmwenguni zinapaswa kuthamini na kuenzi Muafaka kuhusu Haki za Mtoto. Nchi nyingi ulimwenguni zimekwisha kuafiki Muafaka kuhusu haki za mtoto. Muafaka huo unahakikisha kuwa zinaridhia kuhakikisha kuwa haki za mtoto hazitakiukwa na endapo zitakiukwa ziko tayari kukubali ukiukwaji huo mbele ya jumuiya ya ulimwengu mzima. Muafaka huo unashadidia haki za kimsingi za mtoto popote pale na bila ya ubaguzi. Haki hizi ni haki ya

kuishi, haki ya kujiendeleza ipasavyo; haki ya kulindwa dhidi ya taathira mbaya, kudhalilishwa au unyanyasaji wa jinsi yoyote ile; kushiriki kikamilifu katika maisha ya kijamii, kiuchumi na hata kisiasa pamoja na dhidi ya kongwa la ajira.

Katika mataifa mengi, watoto wamesakamwa na wingi wa matatizo. Mathalan, kusokomezwa kwenye vita vya kikabila, ajira ya watoto, unyanyasaji wa kijinsia na maovu mengine ya ukiukwaji wa haki za kibinadamu. Zipo nchi ambapo watoto wanaoishi katika maeneo ya mashambani wana fursa chache za kupata elimu ifaayo na afya ya kimsingi wakilinganishwa na wenzao wanaosakini katika maeneo ya mijini. Muafaka huu unasisitiza kuwa kuwepo kwa tofauti za jinsi hii katika jamii ni ukiukaji wa haki za kibinadamu. Inahalisi serikali za nchi hizo kuhakikisha kuwa hali hizi zimefilia majinani.

**: UFAHAMU ALAMA 15**

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuatia**

(a) Kwa nini jamii ya kesho inategemea hali nzuri ya watoto?
(alama1)

(b) Ni hatua gani kuu ambazo zafaa kuchukuliwa kuhakikisha kuwa watoto wanatunzwa ipasavyo?
(alama4)

(c) Eleza haki zozote mbili za kimsingi walizo nazo watoto. (alama4)

(d) Taja dhiki wanazokumbana nazo watoto.
(alama3)

(e) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika kifungu: (alama 3)

(i) bighairi ya

(ii) Kufanya kulihali

(iii) Kongwa la ajira

**7. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia: (JUMLA ALAMA 15)**

Nchi yetu imeraukia <u>mawio</u> ya machafuzi ya kisiasa baada ya shughuli za uchaguzi zilizogonga mwamba mkuu. Hili lilijiri baada ya Tume ya Uchaguzi kukosa kuendeleza uchaguzi kwa njia iliyostahiki. Jambo hili lilizaa msukosuko wa kisiasa usiomithilishwa katika historia ya taifa letu.

Hivi sasa Wakenya wanaishi kwenye kambi za watu wasio na makazi. Hiki ni kinaya kikuu kwani matukio haya yamezuka baada ya zaidi ya miongo minne ya uhuru. Vilio vya Wakenya vimeshamiri na kupaaza sauti vikilalamikia kukosa makazi, lishe na hata ndoa kusambaratika. Ndoa zimevunjika baada ya 'wenyeji' kuwatimua 'wageni' na damu kumwagika.

Misukosuko ya kisiasa kama hii imekumba mataifa mengi ya Afrika miaka nenda rudi na kuchangia bara kudumaa na <u>kuvia</u> kiuchumi.

Kenya imekuwa miongoni mwa mataifa yanayowapa faraja wakimbizi kutoka nchi jirani zinazokumbwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe, zikiwemo Somalia na Sudan. Kinaya ni kwamba Wakenya wamekuwa wakimbizi katika nchi yao wenyewe. Vita katika Somalia vimesababishwa na koo mbali mbali zinazopigania uongozi hali ambayo imekwamisha shughuli zote za kiuchumi.

Hali ya sasa ya Kenya imechochewa na msururu wa sababu.

Ukabila na tamaa ya uongozi zilionekana wazi katika miundo ya vyama vikuu vya kisiasa na katika kampeni zao. Wakenya walipiga kura kwa misingi ya kikabila kila upande ukitazamia mtu wao kushinda uchaguzi huo.

Kwa upande mwingine, viongozi hao kutokana na tamaa ya uongozi walikuwa wameamua kushinda uchaguzi huo kwa vyovyote vile. Leo tunavuna matunda ya siasa za ukabila na tamaa ya mamlaka.

Maelfu ya Wakenya ni wakimbizi nchini na katika nchi jirani ya Uganda. Wakenya hao wanahitaji msaada wa chakula na mahitaji mengine ya kimsingi. Serikali na Shirika la Msalaba Mwekundu zimefanya juhudi kuwasaidia wahasiriwa Lakini, kuna tetesi kwamba ubaguzi umejipenyeza katika ugawaji wa msaada huo.

Waliopewa jukumu la kugawa msaada huo ni sharti waelewe kuwa waathiriwa ni Wakenya wenzao na hawafai kubaguliwa kwa misingi ya makabila yao.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Matukio kama haya hayastahili kutukia asilani katika taifa hili.

Twahitaji zao aali la viongozi wasiojitwika ubabe bali wawe watumishi wa wananchi. Wanastahili kutupilia mbali tamaa za kujilimbikizia mali na kung'ang'ania uongozi. Pia katiba inafaa irekebishwe. Wakenya wanastahili kuelimishwa kuhusu udugu na utaifa. Fauka ya haya, masuala yanayohusiana na umiliki wa ardhi yanafaa kutadarukiwa kwa dhati.

**Maswali ya Ufahamu**

a. Toa anwani mwafaka kwa makala haya. (alama 1)

b) Taja madhara manne ya ukabila. (alama 2)

c) Shughuli za ugawaji wa misaada zimekumbwa na changamoto gani? (alama 1)

d) Eleza tofauti ya chanzo cha vita nchini Somalia na Kenya. (alama 2)

e) Mwandishi anatoa mapendekezo yepi kwa kutatua tatizo hili la ukabila. (alama 4)

f) Eleza kinaya cha maisha ya wanakenya kwa sasa. (alama 1)

g) Eleza maana ya maneno haya yalivyotumika katika kifungu cha ufahamu.

a) Mawio

b) Kuvia

c) Aali

d) Tadarukiwa.

(Alama 4)

## 8.UFAHAMU

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Siku moja , mtu ambaye alijulikana kwa jina la Moto , alikuwa Ameketi chini ya kivuli cha mbuyu. Alikuwa akifanya hivyo kwa kungojea kulungu kunaswa na mtego wake. Hapo mbuyuni, ndipo palikuwa na njia ya kulungu ya kwenda mtoni kunywa maji. Kupitia mbuyuni, iliwabidi kwanza wapitie pale mtegoni. Lakini kwa kuwa kwa siku hii ya leo wakati wao wa kunywa maji ulikuwa bado kuwadia, naye Moto, badala ya kurudi ili aje baadaye, akaonelea heri angojee hapo.

Haikuwa mara yake ya kwanza kutega kulungu. Alikuwa amewanasa wengi na kwa muda mrefu sana. Na ingawaje alifurahia nyama yao laini, ni kuwachuna ndiko alikokuzira. Hii ilikuwa ni kwa sababu ya vifaa butu vya mawe ya kuchonga alivyokuwa akitumia. Kwa sababu hii basi, haikuwa rahisi kuwachuna. Pia, alikuwa akiwala wabichi. Ili kujipa kazi akisubiri, akaonelea amtengenezee utunda mpenzi mkewe. Hakuwa na shida kuamua utunda huo

ungekuwa wa namna gani. Nyakati hizo, shanga zilikuwa bado hazijavumbuliwa. Ni jiwe na mti tu ndivyo vilivyokuwapo, navyo ndivyo vilivyokuwa mali ghafi.

Kwa ala yake, jiwe la kuchonga, Moto akakata vijiti viwili. Kikubwa akakiita 'mama' na kidogo, 'baba'. Dhamira yake ilikuwa kumtengenezea mkewe ushanga na tembe zikiwa za mti. Akiweka kijiti mama chini, alitumia kijiti baba kupekejea tundu. Alifanya hivi kwa nguvu zake zote, Haja ilikuwa ni atoboe matundu mengi, halafu ayakate na kuyaviringisha na baadaye ayaunge na uzi wa muaa ili apate huo ushanga. Akizidi kupekecha, na jasho kumtoka, na huku mawazo yake yote yakiwa juu ya uso wa mkewe, hakuwa ameona cheche zikianguka juu ya majani makavu yaliyokuwa katikati ya mapaja yake. Alichokisikia kwa ghafla, kilikuwa ni kuchomeka na kuona moshi ukifusika. Alishtuka na akaruka kwa woga. Hakuwa ameshawahi kuona kioja kama hiki maishani!

Huku akitetemeka kwa hofu, cheche hiyo ikaanza kusambaa. Ilijieneza kwa haraka na kuwasha majani, nyasi na miti. Sasa ikawa imepata nguvu na kuwa tsanzala ambayo ilienea kwa upesi na kumeza vichaka na misitu iliyokuwa mbele yake. Kuangalia hivi, akajiona amesimama peupe! Kutoka kwa upande wa mtegoni, kukaja harufu nzuri ya kunukia. Alifuata na alipofika, akaona kulungu ambaye alikuwa ameshikwa na mtego, ameokwa vizuri sana na nguvu hizo ngeni. Hakujua zinaitwaje wala hakujua aziiteje. Kwa hivyo, hakuwa ameshawahi kuona ama kuonja kitu cha kuchoma sembuse cha kupikwa!

Ni harufu ya kuiva ya kulungu na kudondoka kwa mafuta ya kunona ndivyo vilimtia ujasiri. Naye kwa hatua za woga, akanyatanyata akanyakua kinofu na kukionja. Si utamu huo aliousikia! Sasa akanyafua jinofu. Halafu akaingilia maini, moyo na mafigo. Kulungu akamshinda ingawaje alimla maradufu ya kawaida yake. Aliyebaki, akamfunga ndani ya majani ya mgomba na kuwapelekea watu wake. Pamoja na kulungu, akawa amechukua pia kinga kilichokuwa kikiwaka na vile vijiti viwili ambavyo baadaye kijiti mama alikuja kukiita "wimbombo" na kijiti baba, " ulindi"...

Ilikuwa alfajiri asubuhi watu waliposhitukia "tatata" za kualika kwa kuni na kulipuka kwa moshi kutoka nyumbani kwa Moto. Nyumba yenyewe ilionekana ikiwa na nuru nyekundu ya ajabu na ya kutisha. Walinyatanyata kuelekea kwenye kioja hicho. Kiliwavutia zaidi kwani walivyozidi kulisongelea, ndivyo ile baridi ya asubuhi ilivyozidi kuwatoka. Mvuto huo ukawapumbaza. Lakini walipumbazika zaidi walipoona - nyuma ya kioja hicho na kupita pazia la moshi, Moto ameketi.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Macho yake yalionekana mekundu mno. Hii ilikuwa sababu ya moshi; lakini hawakuwa wakijua hivyo. Kiwiliwili chake kilionekana kikiyumbayumba nyuma ya miale. Haya yote yakamfanya kutisha. Wenzake wasijue la kufanya kwa sababu ya bambuazi, wakawa wamesimama tuli wameduwaa. Hapo ndipo waliposikia sauti ikinena: "Mimi ndimo Moootoo...; naivisha na kuunguza, natokeza na naoteka. Anitakaye nitakuja kwake nimpe huu uwezo wangu..."

Ili kuwaogofya zaidi, akaupulizia nao ukaalika kwa moshi na cheche nyingi zilizowafanya wenzake kurudi nyuma kwa hofu. Kuona hivi, akaendelea kuwatia woga kwa kusema, "Hizi ndizo nguvu za Moootoo... mimi ndimi Moootoo...nijieni niwageuzie maisha yenu..."

Akiwa bado ana sehemu ya nyama ya kulungu, akawagawia na kuwaambia wale. Kila mmoja wao akakubali kuwa ilikuwa tamu sana. Naye ndipo aliwaambia siri ya kioja. Hakuwaambia ule ukweli wa mambo, badala yake, aliwaambia ati ni malaika ndiye aliyemtunukia uwezo huo! Aliwalambisha kwa kuwapa kaa kuchukua makwao. Nao, kwa kukosa jina la kufaa, wakaliita "Moto".

Punde si punde, watu wakawa wamezoea moto na wengi wakawa wanakuja kwake tu. Hakutaka uenee vivi hivi tu. Kwa hivyo, akaweka masharti: moto ulipatikana kwake tu kila jioni, na uzimwe mara moja baada ya matumizi. Ni hapo kwake tu ambapo "moto mpya" ungeweza kupatikana. Moto hauibiki wala haufichiki, akawakanya. Na ambaye angefanya ujasiri wa kuuiba ama kuuficha, basi asije kulia kwake baadaye, akawaeleza.

Masharti haya yalifuatwa, naye akawa mgawaji wa moto wa pekee. Uwezo huu ulimtia hisia za ukubwa - na punde si punde, za utukufu pia! Sasa watu wakawa, bila moto, hakukuliwa kitu na basi kumtegemea yeye kukazidi. Hapa ndipo aliwageukia na kuwaambia:

“Ili kuulinda huu Moto Mtakatifu usife, imenibidi kuacha kazi zangu. Lakini siko radhi kuendelea kufa njaa na familia yangu."

" Tutakugawia chakula chetu ili uzidi kuuchunga huo Moto Mtakatifu ili usife," wakamkatiza.

Basi, kwa kila mtu kumpatia theluthi ya chakula chake, Moto akapata uwezo wa kurundika ziada. Siku si nyingi, mkewe na watoto wake wakawa hawana haja ya kufanya kazi. Hali watu hawakukoma kumpatia "kodi ya moto", ndivyo yeye na kizazi chake walivyozidi

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

kujiepusha na kufanya kazi, huku wakizidi kuzua masharti magumu ya kuficha "Utukufu wa Moto".

**Maswali**

a) Ipe makala uliyoisoma anwani mwafaka
(alama 1)

b) Moto alikuwa ameketi chini ya kivuli cha mbuyu kwa sababu gani?
(alama 2)

c) Ala za pekee za wakati huo zilikuwa zipi**?**
(alama 2)

d) Uvumbuzi wa Moto ulikuwa na athari zipi katika maisha ya jamii?
(alama 2)

e) Kwa kutotaka Moto uenee hivi hivi tu, Bwana Moto aliuwekea masharti. Taja mawili

(alama 2)

f) Moto na Aila yake walifaidikaje baada ya ufumbuzi huu?
(alama 2)

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa.
(alama 4)

(i) Kioja
(ii) Alikokuzira
(iii) meza kichaka
(iv) Wimbombo

## 9.UFAHAMU

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Watu husema mengi kuhusu maisha, Wengine husema mtu anapozaliwa hatima yake huwa imeshaamuliwa na Mwenyezi na hata afanye nini hakuna wa kubadilisha, yaani kama *majaaliwa* yake ni awe mwizi stadi katika *siku zake za halafu*, basi atakuwa mwizi stadi bila shaka; kama majaaliwa yake ni awe daktari maarufu, basi atakuwa daktari mashuhuri, na kadhalika, Watu

kama hawa wana msimamo sawa na ule wa raia wa Uyunani (Ugiriki) wanaoamini kuwa maisha ya kila binadamu yana sehemu mbili kuu: sehemu mbaya na sehemu nzuri. Wayunani hawa w'anashikilia kuwa kila mtu lazima azionje sehemu zote mbili katika aushi yake na kwamba haiwezekani kuliepuka jambo hili. Watu hawa pia wanaamini kuwa miungu wao ndio wanaoamua maisha yao yatafuata mkondo gani. Yaani, wana imani kamili kwenye jaala eti kwa vile *wino wa Mungu haufutiki*.

Kwa bahati mbaya, humu nchini mwetu wapo watu ambao wanashiriki imani hiyo ya majaaliwa. Wao wanaamini kuwa wanapozaliwa, kazi yao kuu ni kuponda raha kwani hatima yao Mungu anaijua na hata wafanye nini hawawezi kuibadilisha. Kwa hivyo kazi yao hapa ni kukaa *sambejambe* na kuingojea hatima hiyo. Ukipiga alinacha utagundua kuwa asilimia kubwa ya watu wanaishi katika ufukara mkubwa lakini si kwa sababu hayo ndiyo majaaliwa yao kama wanavyodai, lakini ni kutokana na tabia ya kufanya *msirimbo miradi* yote iliyo mbele yao.

Maisha si majaaliwa. Hutegemea mipango na juhudi. Mtu asipojibidiisha na kupanga maisha yake vilivyo, basi bila shaka mambo *yatamwendea mvange* na ataishia kuishi maisha ya ufukara wa sina sinani. Ukitazama binadamu wengi katika nyanja mbalimbali, utaona kuwa hawana utaratibu imara wa kuendesha maisha yao. Chukua mfano wa vijana.Wao ndio waliokabiliwa vikali na tatizo hili. Wawapo shuleni, wengi wao hawana haja na elimu. Wanaamini kuwa shuleni ni pahali pa kuonjea utamu wa maisha huku wakingoja kubaleghe na kuoa au kuolewa. Wengi hujihusisha na vitendo vya ajabu kama kushiriki katika migomo. Sigara haziwatoki midomoni. Majira ya jioni hawapatikani tena shuleni kwani huwa wametorokea mijini na vitongojini kuponda raha. Dawa za kulevya nazo ndizo hizo. Wengine wanazielewa zote kwa majina hata wameshawahi kuonja kila sampuli ya dawa zenyewe. Si ajabu kuwa tayari baadhi yao ni wagonjwa wa ukosefu wa kinga mwilini. Wapo wale *mahiri* wa kufanya biashara yenyewe ya kusambaza dawa hizo za kulevya; walanguzi waliokubuhu hasa. Kuwepo kwao-shuleni hakuhusiani kwa vyovyote na elimu. La hasha. Ni mahali tu kwa kusukumia miradi yao hiyo. Wengine ni majambazi. Wao hushirikiana na wavunja sheria wengine kupora mali ya wenyewe bila ya mtu yeyote kuwashuku. Haya yote huweza kuonekana kama *yamepigwa chuku*. Lakini ukikumbuka hivi majuzi kifurushi kilichojaa bunduki kilipatikana chumbani mwa mwanafunzi mmoja chuoni, basi utaanza kuyaamini haya yote.

Wanafunzi wengine huifanya kazi yao kuu kuwa ile ya kuwahangaisha wenzao. Katika baadhi ya shule, wanafunzi hasa wa kidato cha pili hujihusisha na vitendo vya kuwadhulumu wenzao wa kidato cha kwanza. Wengine wamefika kiwango cha kuwatisha na hata kuwapiga walimu wao. Wawapo huko nyumbani huwa ni balaa tupu, Baadhi yao huvaa mavazi ya ajabu. Kina dada huvaa nguo fupi kiasi kwamba utadhani wako uchi. Ukiwauliza kisa na maana wanakujibu kuwa eti ndio.mtindo. Wengine huweka herini chungu nzima masikioni mwao na kujipaka rangi za kutisha midomoni. Wengine bila kusita hushirikiana kimwili na wavulana na hata wazee ambao huwafurahisha daima kwa *darahima* na zawadi kochokocho. Ugonjwa wa 'Ukimwi' si mgeni kwao. Sababu kuu ni kuwa wengine, hasa waliokulia mijini, wana mazoea ya kutembelea vilabu na kushiriki ulevi pamoja na ngono. Si ajabu kwamba baadhi yao *wameenda jongomeo* na wengine wako safarini kuelekea kuko huko. Wakikutana na kina dada watalii kutoka ng'ambo wanazuzuliwa na hizo ngozi zao nyeupe pepepe na kuapa kuwa nao pia ni lazima watakuwa kama wao. Wanafanya juu chini kutafuta ngwenje ili kujinunulia vipodozi aina aina vya kupaushia ngozi zao. Wasichana wengine hawasomi tena. Wametulia tuli kama maji mitungini humo majumbani wakiwanyonyesha wana wao waliopata kupitia harakati zao hizo.

Wavulana nao hawaachwi nyuma. Neno ‘nidhamu’ ni istilahi mpya kwao. Wao wanaishi leo, kesho itajililia. Wengine nywele wameziacha kuwa *matimtimu* utadhani ni wajukuu wa majemedari wa vita vya Mau Mau. Wamejitoboa mashimo chungu nzima masikioni ili wavae herini mbilimbili au tatutatu kulingana na mtindo uliopo. Wengine hata nywele wameonelea bora kuzisuka ili wafanane sawa bin sawa na akina dada. Na ili wasiachwe nyuma sana na kina dada hao, hawasahau kuvaa mikufu inayong'ara kuliko hiyo ya akina dada. Nayo mitindo ya nguo huzihangaisha akili zao saa ishirini na nne za kutwa. Macho na masikio yao hukaa chonjo kila dakika ili wafahamu ni mitindo gani mipya iliyoingia hasa kutoka ng'ambo kunakoishi wazungu wenyewe. Wengine nywele wameziweka 'kalikiti'. Suruali wanavaa zilizoganda mwilini utadhani zimewekwa gundi. Nao wengine wana mikururo ya marafiki wasichana. Ukiwauliza kisa na maana ya kutongoja hadi wakati ufike wanasema ndio mtindo. Ukiwauliza na 'Ukimwi je? *Wanakuchezesha kayamba* huku wakilumba kuwa Ukimwi ni porojo tupu; eti wamefanya vituko vyao miaka yote hiyo; inakuwaje *hawajaenda na ulele ngoma?*

Hata hivyo, kwa vile *unga wa manga si dawaya chongo,* baada ya pata shika zote hizo,

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

kilichokuwa na mwanzo kinaanza kufikia hatima yake. Ukweli unaanza kuchukua mahali pake. Muda ambao wangetumia kujizatiti kwa minajili ya siku za baadaye wanashtukia ghafla kuwa tayari umeshawapa kisogo. Majuto na mikasa inawafuata unyo unyo.

Ni muhimu sana vijana kufungua macho yao ili kuona mwanga.Wanafaa kuelewa fika kuwa ujana ni moshi tu. Dakika hii upo, dakika nyingine ushatoweka. Mungu alipoamua kuwa kila binadamu ni lazima apitie ujanani alikuwa na sababu maalumu. Ujana ni kipindi cha maisha cha kujifunga masombo kwa majukumu ya baadaye. Ni kipindi cha kujitafutia maarifa tunu. Iwapo hali ni kinyume, basi mambo hayana budi kwenda mrama

**Maswali**

1. Ipe taarifa hii kichwa mwafaka. (alama 1)
2. **Eleza** msimamo wa watu wengi imani kwenye jaala. (alama 2)
3. **Taja** vitendo vyovyote vinne vinavyoonyesha upotovu miongoni mwa vijana. (alama 4)
4. Kutokana na taarifa; **eleza** jinsi vijana wanavyo ambukizwa ugonjwa wa ukimwi (alama 3)
5. Unadhani ni mambo yapi mengine yanachangia tabia potovu kati ya vijana? (alama 2)
6. **Toa** maana ya: (alama 3)
   (a) Kufanya msirimbo
   (b) Unga wa manga si dawa ya chongo
   (c) Kwenda mrama

## 10.UFAHAMU

***Soma makala yafuatayo kisiha ujibu maswali***

Utandaridhi (au globalization kwa lugha ya kiingereza) ni jinsi maisha inavyoendelea kuutawala ulimwengu wote katika karne ya 21. Neno utandaridhi ni neno mseto ambalo maana yake ni utamaduni uliotanda au kuenea ardhi nzima. Mtu mtandaridhi hivyo basi ni mtu aliyebobea kikamilifu katika

utamaduni huu mpya kwa jinsi moja au nyingine. Mtandaridhi hujihusisha sana katika kutandaridhirisha na moja au nyingine ya *amor a* muhimu za kutandaradhi. Hizo ni kama vile biashara za kimataifa aina za mavazi zilizotokea kupendwa ulimwenguni kote, muziki wa kisiku hizi has vile pop, regge, raga, rap ambao asili yake yahivi majuzi ni Marekani. Muziki huo wambaji wake hutumia, sana sana lugha ya kiingereza hususan kile cha Marekani na kadahlika. Watandarishi wana nyenzo zingine kadha wa kadha za kuendeshea maisha yao au kujitambulisha. Wao huwasiliana kutoka pembe moja ya dunia had nyingine wakitumia vitumeme yaani vyombo vitumiavyo umeme kufanya kazi vya hali ya juu kama vile tarakilishi na simu hata za mkono. Watu huwa hawakosi runinga sebuleni mwao usiseme redio. Hawa husikiliza na kutazama habari za kimataifa kupitia mashirika matandaridhi ya habari kama vile BBC la uingereza na CNN la marekani. Aidha wtu hawa husafiri mara kwa mara kwa ndege na vyombo vingine vy kasi. *Hawa hawana mipaka.* Wale wanaohusudu utandaridhi wanaamini kindakindakika kwamba utamaduni huu wa kilimwengu umeleta *mlahaka* mwema baina ya watu binafsi, makampuni makubwa makubwa ya kimataifa na uwiano bora baina ya mataifa. Watu hawa husikia wakidai ya kuwa aina hii ya utamaduni irneupigisha mbele ustaarabu wa wanadamu ulimenguni kote. Kwa upande mwingine, *wakereketwa* wa tamaduni za kimsingi za makabila mbalimbali ulimwenguni wanadai ya kwamba utandaridhi umeleta maangamizi makubwaya tamaduni hizo. Kwa ajili hiyo basi, utandaridhi umesemekana kwamba unasababisha kutovuka kwa utu miongoni ma wanadamu wote, ambao wamo mbioni kusaka pesa na kunemesha ubinafsi. Inadaiwa pia kwamba utandaridhi umesababisha kutovuka kwa adabu kwa vijana wengi ulimwenguni kote ghaya ya utovu. Huku kutovuka kwa adabu kwa vijana, hasa wale wa mataifa yanayojaribu kuendelea, kumeleta zahama *chungu mbovu*, ikiwa ni pamoj a na kuenea kwa UKIMWI kwa kasi ya kutisha

## Maswali

(a) (i) Bainisha kwa kutoa maelezo kamili kwamba *utandaridhi* ni neno mseto (alama 3)

(ii) Toa maneno mawili kutokana na neno *kutandaridhisha* kisha ueleze maana za maneno hayo (alama 2)

(b) (i) Nini maana ya hawana mipaka? (alama 3)

(ii) Kwa nini watandaridhi wanapenda kusikiliza na kutazama habari kupitia BBC na CNN (alama 2)

(c) (i) ElezaldkamilifomaoniyawataM (alama 3)

(ii) Je, utandaridhi unalaumika kwa nnini katika kifungu hiki? (alama3)

(d) Msemo: "chungu mbovu" ni msemo wa kimtaani tu. Msemo sawa ni upi?

(alama 1)

(e) Elezamanayamanenoyafuatayo

(i) amara "

(ii) mlahaka

(iii) wakereketwa

(alama3)

## 11.UFAHAMU

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Wahenga walisema "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo." Hii ina maana ya kuwa ukiogopa kutumia ufito kumchapa mtoto wako, ukamdekeza, atadeka na hatimaye ataharibika. Methali hii ina pacha yake ambayo ni, "Ukicha mwana kulia,utalia wewe".

Hizi ni methali zilizojaa busara kubwa. Mathalani, wewe ni mzazi au mtu mzima aliyetunukiwa madaraka juu ya watoto, lakini kila wanapokiuka uadilifu au mmoja wao anapokosea wewe unambembeleza tu, basi huwa unaizorotesha tabia yake. Mwisho, mtoto huyo anaweza kuishia kuwa mtundu.

Hata hivyo, ni sharti tujue ya kwamba tuko katika njia panda hapa. Kwa upande mmoja, zamani ilichukuliwa kwamba watoto na hata wanawake watu wazima hawana akili. Kwa ajili hiyo, iwapo mwanamume mtu mzima ana jambo la kuwaeleza, njia pekee ya kuliingiza katika "akili" yao “hafifu" ni kuwatwanga ili <u>kulikongomeza jambo hili</u>.

Ukweli ni kwamba akili ya mtoto si hafifu hata. Unaweza kusema ni kama mmea, ambao "usiporutubishwa kimakusudi, ukapaliliwavyemanakustawishwastahiki yake, basi hudhoofii"namwishowekufifia.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Kwa upande mwingine, mtazamo wa kisasa ni tofauti kabisa. Irnethibitishwa ya kwamba wanawake ni sawa kabisa katika maumbile yao wakilinganishwa na wanaume. Kwa jinsi hiyo, kweli wapo wanawake ambao hawana mwelekeo timamu kuhusu maisha, lakini ni kweli pia kuwa wapo wanaume watu wazima mamilioni ambao hawana akili. Kadhalika, si kweli kuwa watoto wote, kwa sababu ya umri wao tu, basi hawana akili,

Ama kwa kusema kweli binadamu yeyote huzaliwa na akili zake timamu, isipokuwa wale ambao kwa bahati mbaya maumbile yamewapa akili pungufu. Hili litokeapo, basi tunalikubali tu, Hatuwezi kumlaumu mtu kama huyo aumuumba wake. Kwa» hakika him ndio msingi wa methali, "Akili ni nywele, kila mtu ana zake." Vinginevyo, mtazamo wa kizamani ni taasubi kongwe tu za kiume zilizopitwa na wakati.

Aidha kwa sababu watu wote huzaliwa na akili timamu, tena hawawi watu wazima kabla ya kuwa watoto kwanza, mtu mzima yeyote ana hali gani ya kuwadhulumu watoto na kujipambaniza na lawama za uongo dhidi ya vijana hao kwa madai kuwa hawana akili? Na je, ikiwa hawana akili, basi ndipo waonewe? Wanyanyaswe? Hili si jambo la busara. Kurudi mtoto kwa visa vya maonevu ni kumrudisha nyuma kiumbe huyo. Kurudi kufaako ni kwa kupeleka mbele, sio kwa kurudisha nyuma. Kurudi kuelekezako mbele ni kwa uongozi mwafaka, uongozi ambao lengo lake ni kummulikia mtoto kurunzi ilimradi kumwangazia tariki njema.

Mtoto asinyimwe vya tunu vyovyote ambavyo ni stahiki yake, kwa kisingizio kuwa vimetengewa mtu mzima, ndugu mkubwa, mwalimu, au mtu awaye yeyote yule aliyekabidhiwa jukumu la kumlea au kumwongoza mtoto.

Mtoto ana haki ya kuhudumiwa kwa nj ia yoyote ifaayo ili akue na akili yake ikomae kikamilifii. Inafaa asomeshwe, apewe malezi bora ili naye aje alee wengine kistahiki.

**Maswali**

(a) "Mapenzi yasiyo kipimo yanaweza kuwa hatari kwa mtoto." Eleza kikamilifii huku ukirejelea habari uliyosoma (alama 3)

(b) Fafanua njiapanda inayorejelewa na mtunzi (alama 3)

(c) Mtoto analinganishwa na mmea katika taarifa hii, kwamba "usiporutubishwa kimakusudi, ukapaliliwa vyema na kustawishwa stahiki yake basi hudhoofika".

Tathmini kulinganishwa huku, huku ukirejelea taarifa (alama 4)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(d) "Akili ni nywele, kila mtu ana zake". Eleza maana ya ndani ya methali kulingana

na taarifa (alama 4)

(e) Onyesha kwamba unaelewa mana ya:

"Kurudi mtoto kwa visa vya maonevu ni kumrudisha nyuma kiumbe huyo" (alama 4)

(f) Eleza maana ya:

(i) Kulikongomeza

(ii) Kujipambaniza (alama2)

## 12.UFAHAMU

***Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali***

Nairobi, mji mkuu wa Kenya, ni jiji la maajabu na mastaajabu chungu nzima. Nadhari ya mtu anaye wahi kuingia jiji hili kwa mara ya kwanza huvutiwa na huo msheheneko wa majumba ya fahari, marefu ajabu, kiasi cha minazi mitano sita, iliyoiunganishwa kuelekea juu mbinguni.

Jumba linalowavutia watu wengi ni lile la makongamano ya kimataifa liitwalo kwa kiingereza Kenyatta International Conference centre. Jumba hili, hadi miaka michache iliyopita, ndilo lilikuwa refu zaidi mjini. Jumba lenyewe lina ghorofa ishirini na tisa hivi,usipohesabu hilo pambo kama kofia kileleni mwake, linalojulikana kama mwavuli. Hata hivyo, miaka michache iliyopita jengo hili lilipitwa kwa urefu na Mnara wa Nyakati (Times Tower). Mnara huo hasa ni jumba linaloafiki lakabu yake ya kikwaruza mawingu. Jumba hili lina ghorofa zisizopungua thelathini na mbili.

Mbali na mjumba haya mawili mengine zaidi ya ishirini katikati yajiji ambayo, japo mengine ni mafupi kiasi, yana maumbo ya kustaajabisha kweli kweli. Hebu zingatia mwenyewe jumba liitwalo "mdomo wa kengele" au "bell-bottom" ambalo ni vioo vitupu, toka chini hadi juu. Fauka ya hayo, umbo lake ni la kipekee iilimwenguni kote. Jumba hili lina kama miguu, kisha kiuno mithili ya kinu hivi japo si mviringo. Linapaajuu mbali sana, likichukua umbo pana kuliko lilivyo chini: umbo la fua pana kama kengele.

Halafu rudia barabara. Hizi hazina hesabu katikati ya jiji na ni pana, tena safi sana.

Magari yanayotumia barabara hizi ni kochokocho, ya kila aina na yanashindania nafasi.

Ajabu kubwa ya Nairobi hata hivyo ni idadi ya watu. Hakuna hasa anayejua idadi kamili ya watu wa Nairobi, lakini sio kupiga chuku ninaposema kwamba, hasa nyakati za kuelekea kazini asubuhi, kwenda kula chakula cha mchana, kuelekea nyumbani baada ya kazi na kuvuka barabara wakati wa msongamano, watu hukanyagana. Mtu anayesema kwamba watu wa Nairobi, ni wengi kama chungu, au kama mchanga wa ufuo wa bahari hatii chumvi.

Watu wa Nairobi, kwa tabia ha mavazi, si kama watu wa kwingineko nchini Kenya. Watu hawa huvalia nadhifu sana. Wanawake rii warembo ajabu na hutengeneza nywele zao mithili ya hurulaini peponi. Wengi huvaa suruali ndefu! Kucha zao na midomo yao hupaka rangi maridadi sana. Huzungumza Kiswahili na kiingereza takriban wakati wote. Wanawake wengi ajabu huendesha magari yao wenyewe, jambo ambalo litakushangaza mara tu uingiapo jijini, hasa kama ulilelewa ukidhkni maskani mwafaka ya wanawʳake ni jikoni peke yake, yaani kuzingatia ile falsafa kuwa "kuoa ni kupatajiko".

Wanaume nao huvaa suti safi, maridadi na shingoni wamefunga tai stahiki yao. Wanaume hao huendesha magari na kuyaegesha karibu na afis zao. Huingia afisini mwao kwa m aringo na madaha, huku funguo za magari yao zikining' inia vidoleni.

Hawa nao husema Kiswahili na Kiingereza kupiiia puani, utadhani ni waingereza hasa.

Kwa upande mwingine, watoto ni nadhifti kweli kweli hasa watoto wa shule. Hawa huvalia sare zilizofuliwa na kunyoshwa vizuri kwa pasi. Wake kwa waume, shingoni huvalia tai. Watoto wa shule Nairobi huongea Kiswahili, Kiingereza na Sheng, ambayo ni "lahja" yao waliyoibuni. "Lahja" hii ni mchanganyiko wa Kiswahili, kiingereza na msamiati mchache wa lugha nyingine za wakenya zisemwazo jijini Nairobi na vitongoji vyake.

Kwa jumla, watu wote wa Nairobi hutembea kasi sana. Hawana wakati wa kutembea pole pole na kuangazaangaza huku na huko. Iwapo weweni mgenijijini, ukizubaa utapigwa kumbo na waendelee na hamsini zao kama vile hapakutokea jambo. Hili linapojiri, usidhani limefanywa rnakusudi. La hasha. Ni vile tu kwamba Wanairobi hawana muda wa kupoteza.

**<u>Maswali</u>**

(a) Kwa nini-majumba ya jiji la Nairobi yana majina au lakabu za kiingereza?

(alama 2)

(b) (i) Baadhi ya maajabu ya Nairobi ni barabara safi, msongamano wa magari na majumba rnarefu. Ongezea maajabu mengine manne. (alama 4)

(ii) Watu wa Nairobi wanajipenda kweli kweli. Fafanua (alama 4)

c) (i) Je, undhani watu wa Nairobi kweli hukanyagana? Eleza ni kwa nini msimulizi ametoa maelezo hayo. (alama 2)

(ii) Unafikiri ni kwa nini hasa wanake wa Nairobi wanaonekana nadhifu? (alama 3)

(d) Kwa nini "lahja" limewekwa alama za mtajo? (alama 1)

(e) Eleza maana ya maneno na tamathali zausemi zifuatazo (alama 4)

(i) Nadhari

(ii) linaloafiki (iii) kikwaruzamawingu.

(iv) waendeleenahamsinizao.

**13.** ***Soma makala yafuatayo kisa ujibu masawali:***

Ulimwengu unapaswa kuzuka na mbinu za kulitadarukia tatizo la umaskini ambao unakwamiza juhudi za maendeleo. Umaskini unaoyakabili mataifa yanayoendelea unayatosa kwenye dhiki kubwa huku mataifa ya kimagharibi ya kipiga hatua kubwa kimaendeleo. Ufa uliopo baina ya mataifa yanayoendelea na yale yaliyoendelea kama vile Marekani, nchi za Ulaya na Ujapani unapanuka kila uchao.

Vyanzo vya umaskini huu ni anuwai mathalan, ufisadi, uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyitabirika, idadi ya watu inayoipuka uwezo wa uchumi wa taifa linalohusika na ukosefu wa nyenzo na amali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini. Ukosefu wa elimu na nafasi adimu za ajirahuchangiapia katika tatizo hili.

Jamii ya ulimwengu inapaswa kuelewa kuwa umaskini unaoathiri nchi Fulani una athari pana sana. Uvunjifu unaotokana na umaskini unaweza kuwa mboji ambako matendo mabaya huchipuka. Raia maskini huweza kushawishiwa haraka kujitosa kwenye matendo ya kihalifu ili kujinasua kutoka dhiki ile. Hii inaweza kuwa mbegu ya kuatika maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.

Mataifa ya magharibi yanapaswa kuyaburai madeni mataifa yanayoendelea kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipia madeni hayo. Katika hali hii inakuwa muhali kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na pingu za umaskini. Njia nyingine ni kustahabu kutoa ruzuku za kimaendeleo badalayamikopo kwa nchi zinazoendelea.

Kwa upande wake, mataifa yanayoendelea yanapaswa kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini. Ni muhimu pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini. Pana dharura ya kuzalisha nafasi za ajira, kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tegemeo kuu la mataifa mengi, kuendeleza elimu na kuimarisha miundo msingi. Ipo haja pia ya mataifa haya kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru unaoutawala ulimwengu sasa hauishii kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umaskini zaidi. Kwa ufupi, maamuzi yote ya sera za kiuchumi lazima yauzingatie uhalisi wa maisha ya raia wa mataifa hayo.

**<u>Maswali</u>**

a) Kwa nini umaskini umetamlaki katika mataifa yanayoendelea? ( alama 4)

b) Madeni yana athari gani kwa mataifa yanayoendelea? (alama 2)

c) Ni mapendekeo yapi ambayo mwandishi anatoa kwa mataifa machanga kuhusu

utatuzi wa tatizo la umaskini (alama 4)

d) Mfumo wa soko huru una mathara gani kwa mataifa machanga? (alama 2 )

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

e) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya: (alama 3)

i) Kulitadarukia ii) Kuatika iii) Kuyaburai madeni

# UFUPISHO

1. ***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali***

Umaskini ni tatizo sugu katika jamii. Binadamu wengi hujikuta katika hali hii kwa sababu hawakubahatika kusoma. Baadhi yao huenda walijaribu kusoma wakashindwa mapema kujipandisha kielimu. Ukosaji wa elimu huchangia sana katika kukuza ukata. Elimu huweza mtu kupata tonge kwa kujipatia kazi za kumwezesha kuyakidhi mahitaji ya maisha. Hali kadhalika, elimu humsaidia binadamu kupata maarifa mengi ya kutendea shughuli zake za kimaendeleo. Kwa mfano, kama ni wakulima wanaweza kutumia **pembejeo** zifaazo ili kuboresha uzalishaji wa mazao. Wakulima wenye elimu hawatapendelea njia duni za kuendeleza kilimo kama vile kutumia visagilima na mbinu nyingine za kijadi. Badala yake watatumia njia za kisasa za kuvunia mazao yao.

Umaskini mwingine huwa mwiba wa kujichoma. Baadhi ya watu ni mikunguni. Kulaza damu kwao kunawafanya kuwa wategemezi katika familia na jamii kwa jumla. Kwa vile hawajazoea kuinamia cha mvunguni, hata wakifunzwa kuchakura hawawezi. Ili kujaribu kuutibu uwele wao na ufukara baadhi yao hutafuta njia za mkato kama vile upwekuzi wa vitu vya wale waliojitahidi. Wakifanikiwa huweza **kufurisha vibindo vyao.** Hata hivyo mkono mrefu wa walinda usalama ukiwakumbatia wao hubakia kusagika kwa dhiki isiyomithilika ndani ya magereza.

Majanga ya kimaumbile kama vile mitetemeko ya ardhi, mikurupuko ya maradhi hatari, moto, ukame na mafuriko huchangia na kuzidisha umaskini. Matukio hayo yakiandama kidindia watu wengi huhasirika. Licha ya mali nyingi kupotea, manusura huachwa wakiwa maskini hohehahe. Matumizi yao hupotea kwani wengi huhitajika kuanza maisha upya.

Vijana ni nguzo muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote ile. Endapo watajiingiza katika uraibu wa dawa za kulevya, wataathirika wao wenyewe na jamii kwa jumla. Pamoja na kuwa vijana hawa hufuja pesa nyingi katika ununuzi wa dawa hizi, dawa zenyewe huwadhoofisha na kuwapoka nguvu za kushiriki katika uzalishaji mali. Kutokana na hali hii,umaskini hupaliliwa na kushamiri zaidi.

Umaskini huzua matatizo mbalimbali katika jamii. Ufukara huchachawiza juhudi za serikali za kuwapa raia wake mahitaji ya kimsingi kama vile huduma za afya. Pia umaskini husababisha maovu mbalimbali ya kijamii kama vile mauaji na ukahaba.

FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

Baadhi ya wanajamii huona kwamba njia ya kipekee ya kukabiliana na changamoto zinazosababishwa na hali ya ulitima ni kupitia kwa biashara haramu. Hali hii huchochea zaidi kudorora kwa maadili ya kijamii.

Mataifa mbalimbali ulimwenguni yamezua mikakati mahsusi ya kukabiliana na umaskini. Baadhi ya mataifa yamebuni utaratibu maalum wa kupunguza mwanya mkubwa uliopo kati ya matajiri na maskini. Mojawapo ya mipango hiyo ni kupandisha viwango vya kodi inayotozwa wenye mishahara minono na wafanyibiashara wenye pato kubwa. Aidha huduma za burudani hutozwa kodi ya kiwango cha juu. Kupitia kwa kodi hizo, na njia nyinginezo, serikali za nchi hizo hupata pesa za kuwahudumia maskini.

Mataifa yanayoendelea yanaweza kuwakwamua wananchi kiuchumi kwa kuwapa wahitaji mitaji ya kuanzisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo. Mifano ya miradi hiyo ni viwanda vya 'Jua kali', ususi wa vikapu na uchongaji wa vinyago. Hali kadhalika, serikali inaweza kuwatafutia masoko ya nje wafanyi biashara wadogo wadogo. Aidha, serikali inaweza kupunguza ushuru kwa bidhaa zinazoagizwa na masoko ya nje wafanyibiashara wa aina hiyo. Mathalan, ushuru unaotozwa nguo kuukuu zinazoingizwa nchini ukipunguzwa, wauzaji wa nguo hizi watafaidika zaidi na hali ya umaskini itaendelea kupungua.

Sehemu za mashambani ni mhimili mkubwa wa uchumi. Ingawa kumekuwa na juhudi za kuzistawisha sehemu hizi kwa kusambaza huduma za umeme na maji kwa gharama nafuu, bado hali haijawa ya kuridhirisha. Ili kuimarisha sehemu hizi na kukabiliana vilivyo na tatizo la umaskini, hatuna budi kusambaza huduma hizi hasa katika sehemu kame. Sehemu hizi zikipata maji, kilimo chenye natija kitaendelezwa na umaskini utakuwa karibu kuzikwa katika kaburi la sahau. Ikiwa tutazitekeleza sehemu hizi, vijana wanaoweza kusistawisha watahamia mjini kutafuta maisha 'bora'. Hali hii itazidisha msongomano wa watu mjini.

Umaskini ni nduli ambaye lazima aangamizwe ima fa ima. Vijana hawana budi kubadili mtazamo wao hasa kuhusu kazi za mashambani na kujitahidi kuimarisha kilimo. Fauka ya hayo, mifumo mwafaka ya elimu ibuniwe ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi ya taifa. Badala ya kuhimiza elimu ya kinadharia, elimu tekelezi isisitizwe zaidi ili wale wanaokosa kazi za kiafisi waweze kujiajiri katika kazi za kiufundi. Ukusanyaji wa ushuru uimarishwe zaidi. Hali ya usalama iendelee kustawishwa ili kuzidi kuwavutia wawekezaji, na hivyo kubuni nafasi zaidi za kazi.

**Maswali**

(a)Kulingana na kifungu '**umasikini ni hali inayoletwa na udhaifu wa mtu binafsi**'. Jadili

(maneno 30-40)

(b)Jamii ina uwezo wa kukabiliana na hali ya umaskini inayowakumba raia wake. Thibitisha kwa mujibu wa kifungu (maneno 40-50)

2. **MENO YA BINADAMU**

Kila mara tunapokula, meno yetu huuma, kutafuna na kusaga chakula tunachokula. Meno yanatuwezesha kukivunja chakula ili kuwezesha mwili wetu kukitumia. Ili mwili uweze kukitumia chakula hicho, pana vitu fulani vinavyokifanyia chakula hicho kazi mpaka kikaweza kuingia kwenye mwili wenyewe. Hivi hujulikana kama vimeng'enya.

Binadamu ana meno ya aina nne kuu. Kwanza, kuna meno ya mbele au makato ambayo kazi yake ni kuuma au kukata chakula. Haya yanasaidiana na mengine yanayojulikana kama michonge; yanakata pia lakini yako sehemu ya nyuma. Michonge hufuatwa na meno mengine yanayosaga chakula na ambayo hujulikana kama masagego. Masagego hufanya kazi na meno mengine yajulikanayo kama magego. Kazi ya aina hizi mbili za meno ni kutafuna na kusaga chakula kabisa kabla ya kukimeza. Idadi ya meno ya mtu mzima ni thelathini na mbili. Bila ya kuwa na meno mazuri, binadamu hukabiliwa na matatizo makubwa wakati wa kula. Meno huweza kuharibika kwa sababu ya kutopigwa mswaki vizuri mara kwa mara. Ili kuhakikisha kuwa meno yetu ni mazuri, pana umuhimu wa kudumisha afya nzuri ya meno. Kila baada ya kulala, lazima tuhakikishe tumeyapiga mswaki vizuri bila ya papara ili kuondoa mabaki ya chakula yanayoweza kuwa chanzo cha viini vinavyoharibu meno. Pili, lazima tuhakikishe kuwa hatuharibu ufizi wa meno, yaani ile nyama inayoshikilia meno hasa kwa vijiti katikati ya meno baada ya kula. Afya ya meno ni muhimu ili kuhakikisha kuwa meno yetu yanadumu na kuendelea kutufaidi katika uhai wetu.

. (a) Kwa nini ni muhimu kudumisha usafi wa meno?
(Tumia maneno yasiyozidi 25)
(b) Fupisha taarifa uliyosoma. (Tumia maneno yasiyozidi 80).

3. ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Nchi nyingi za ulimwengu wa tatu huathirika na biashara ya kimataifa.Biashara hiyo inaweza kuwa inafanya kwa uagizaji ama uuzaji wa bidhaa za nchi nyingine.

Biashara ya kimataifa ina umuhimu mkubwa. Kwanza, inawezesha nchi kupata bidhaa ambazo haitengenezi mbali na kusaidia kuwepo na uhusiano kati ya nchi mbalimbali. Uhusiano huu huiwezesha nchi kupata bidhaa kwa bei rahisi kuliko ambavyo ingekuwa kama zingetengenezwa kwao, hasa ikiwa nchi inayohusika haina malighafi yanayohusika katika utengenezaji wa bidhaa hizo. Pia husaidia wakati nchi imekumbwa na dharura au majanga kwani itaauniwa na nchi nyingine ingawa hali kama hii haihakikishwi, ushirikiano huu vile vile huchochea upatikanaji wa nafasi za kazi kwa wengi.

Kwa sababu za kushughulikia utengenezaji wa bidhaa na utoaji huduma nyingine kutokana na uzoefu wa muda na kuwepo raslimali, nchi huwa na uzoefu fulani. Ni kwa sababu hii nchi inawezeshwa kupata pesa za kigeni na kuuza bidhaa za ziada.

Hata hivyo kuna matatizo yanayozikumba nchi za kiafrika katika biashara hii. Kwanza, biashara ya aina hii hutatiza viwanda vichanga katika nchi zinazoendelea kwa ushindani usio sawa. Ajabu ni kwamba nchi zilizoendelea zimetumia bishara hii 'kutupa' bidhaa za hali ya chini ama zenye athari kwa hali za kijamii.Urafiki haukosi. Ikiwa nchi inategemea uagizaji wa bidhaa, haitaweza kuikosea ama kuhitilifiana na nchi ambayo inategemea, hivyo kuathiri uhuru wa nchi kama hiyo.

Hata hivyo, nchi mbalimbali zimeweka mikakati ya kulinda viwanda kutokana na athari ya biashara kama hii. Baadhi zimeweka ushuru wa juu kwa bidhaa zinazoagizwa utoka nje kwa wasio washirika wa kibiashara. Licha ya hayo, baadhi ya bidhaa zinazonuiwa kwa nje kwa matumizi ya kielimu, utafiti wa kisayansi nabidhaa za maonyesho huagizwa bila ushuru huo. Wakati mwingine ni benki kuu ndiyo hutoa leseni kwa niaba ya serikali kama njia ya kudhibiti bidhaa kutoka nje. Njia nyingine ya kuvisaidia

viwanda nchini ni kuuza bidhaa kwa njia ya kuvipunguzia ushuru, usafirishaji nafuu na kuvipa ushuru.

Serikali nyingine huhakikisha kuwa ni bidhaa kiasi fulani tu ambazo zinaweza kuagizwa kwa kipindi fulani. Kwa mfano, kuna idadi fulani ya magari kutoka nje yanayoweza kuagizwa kuja Kenya kwa mwaka mmoja. Hata hivyo, wakati mwingine, serikali husitisha uagizaji wa bidhaa kama vile dawa, sinema, maandishi ya kisiasa na vitabu kutoka nje; bidhaa ambazo zinachukuliwa kuwa hatari kwa nchi. Licha ya matatizo haya, biashara imekuwepo na inaendelea kujiimarisha.

**Maswali**

(a) Kwa mujibu wa mwandihsi wa makal haya, bishara ya kimataifa itaendelea kujiimarisha.
Eleza (al. 6) (maneno 40-50)

(b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika aya mbili za mwisho. (maneno 40-50)

**4.** ***Soma taarifa inayofuata kisha ujibu maswali yaliyoulizwa***

Usafiri ni upelekezi wa watu na bidhaa au mizigo kutoka mahali pamoja hadi mahali pengine. Tuseme kutoka kituo A na kuenda kituo B.

Katika ulimwengu wa leo, watu na bidhaa husafirishwa barabarani kwa mabasi au motokaa za kila aina au kwa kutumia magari moshi yanayopita juu ya reli, au meli zinazopita majini, kadhalika, usafiri unaweza kufanyiwa hewani.

Hivyo, hali haikuwa hivyo zamani. Usafiri uliojulikana sana kale ni usafiri kwa miguu. Watu waliposafiri kutoka eneo moja hadi jingine walilazimika kufanya hivyo kwa miguu. Kadhalika, watu waliposafirisha mizigo mizito kutoka eneo moja hadi nyingine, iliwabidi kuibeba mizigo hiyo wao wenyewe. Mpaka leo usafiri huu upo.

Wanyama vilevile walitumiwa kama njia moja ya usafirishaji. Huku Afrika ya mashariki kulitumika wanyama wengine kama vile punda. Punda ni mnyama anayependwa sana kwa sababu anaweza kuenda mwendo mrefu pasipo na kunywa maji. Mpaka leo, mnyama huyo hutumika sana na wamaasai, wagala, warendile na wengine.

Mnyama mwingine aliyetumika sana, na mpaka leo anaendelea kutumika ni ngamia. Ngamia anafaa sana katika usafiri wa jangwani. Kwato za ngamia huweza kusafiri kwa urahisi jangwani ama popote penye mchanga mwingi kwa sababu kwato zake hazizami kwenye mchanga. Isitoshe ngamia wanaweza kwenda mwendo mrefu bila maji au chakula huku wakitegemea mafuta yaliyohifadhiwa kwenye nundu zao.

Katika ulimwengu wa kisasa, binadamu amepiga hatua kubwa sana katika masuala ya usafiri. Baadhi ya maendeleo hayo ni ya kustaajabisha. Kwa mfano, binandamu anaweza kuruka kwa kutumia vyombo vya angani kwenda kwenye anga za mbali. Katika karne iliyopita binadamu anaweza kuruka kwa kutumia vyombo vya angani kwenda kwenye anga za mbali. Katika karne iliyopita binadamu amefika mwezini kwa kutumia vyombo hivyo. Kuna tetesi kwamba sasa anajaribu kuzizuru sayari zilizoko mbali na ardhi.

Ama kwa hakika, usafiri bora in kipimo kimojawapo cha maendeleo ya nchi yoyote katika ulimwengu wa sasa. Bila njia ya kisasa za usafiri, baadhi ya mambo yanayofanyika katika nchi zetu hayangefanyika.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(a) Katika habari hii, punda na ngamia wana sifa gani muhimu zinazowawezesha kutumiwa

kwa usafirishaji? (maneno 30-40) (ala. 6, 1 mtiririko))

(b) Kwa mujibu wa taarifa, usafiri wa zamani unatofautiana vipi na ule wa siku hizi? (maneno 40-50) (al. 7, 1 mtiririko)

5. ***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali***

Sisi vijana wa Kenya inatupasa tuwajibike kufanya kazi kwa bidii na kwa dhati ya mioyo yetu uweze kupata ufanisi na uwezekano wa kuinua nchi yetu changa katika kiwango cha juu. Tukumbuke, "Ajizi ni nyumba ya njaa". Kwa hivyo basi haifai kulaza damu ikiwa matatizo chini mwetu yametuzonga. Lazima tufanye kazi kwa busara, adabu njema na jitihada kwa moyo mmoja. Sharti tutilie maanani zaidi elimu ya vijana na watu wazima, kilimo, uchumi na amani katika nchi yetu.Tunahitaji taifa la watu walioelimika, kwani bila elimu itakuwa vigumu sana kuweza kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo. Tupende tusipende lazima tuzidishe mazao mashambani, kwani kila kukicha idadi ya watu inaongezeka. Ni sharti tuweze kujitosheleza katika vyakula. Zaidi ya hayo lazima tujishughulishe na biashara ambapo kwa sasa ni Wakenya wachache sana ambao wanatambua umuhimu wake. Wengi ni wale wenye mawazo kwamba lazima kila mmoja aajiriwe maishani. Yatupasa tujitahidi kuleta uchumi katika mikono ya wananchi wa Kenya badala ya kuwaachia wageni .

Mafunzo tunayopata nyumbani, shuleni na hata katika jamii, lazima yatuwezeshe kutambua mbinu za kupitia. Tunahitaji elimu tambuzi ambayo itamfanya mwana Kenya kujua wajibu wake katika jamii. Tumesinywa na elimu pumbao; inayotupumbaza na kutufanya tusione mbele. Sisi vijana tukiwa viongozi wa siku zijazo tuwe kielelezo chema kwa wengine. Watu wazima washirikiane na kufikiria kwamba wao ni wamoja, "Utengano ni uvundo". Lugha ya taifa ndicho chombo cha pekee ambacho kinatuunganisha na kuweza kutuwasilishia mapendekezo, mawaidha na hisia zetu. Kukosa ndiko kibinadamu ,wakati tunapokosea na kufanya masahihisho mara moja kwani, :Usipoziba ufa, utajenga ukuta. "Tusikasirike kwa sababu tumesahihishwa makosa yetu na wenzetu. Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi yetu tukiwa wazalendo halisi.

Sisi tukiwa vijana sharti tujishughulishe na kuyaangalia matatizo ya nchi, pia kutafuta njia za kutatua matatizo hayo. Siku zote tutekeleze nidhamu. Ni jambo la kusikitisha kwamba sisi vijana twashtumiwa mara kwa mara kwa kutokuwa na nidhamu shuleni na majumbani mwetu. Utamaduni wa asili unakariri sana kuwa tuwe na nidhamu shuleni na nyumbani mwetu. Ili watu waweze kuishi maisha bora na kuwa na maendeleo, amani na upendo; lazima tuwe na bidii, ushirikiano mwema na kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo. Tukiwa viongozi ambao hawajishughulishi na maendeleo, basi tutabaki nyuma kama mkia siku zote. Bahati mbaya ni kwamba wananchi wengi siku hizi huchagua viongozi wao kwa kufuata ukoo ama kwa utajiri wake. Kwa hivyo basi, tuchagueni viongozi ambao watatuletea ufanisi badala ya viongozi wanaotokana na nasaba au ya utajiri.

a) Dokeza mambo muhimu yaliyomo katika aya ya kwanza. (Maneno 65 – 70)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

b) Fupisha aya ya mwisho kwa kuzingatia mambo muhimu yanayowapasa vijana kufanya (Maneno (maneno 35 – 45)

**6.** ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:***

Usawa wa wanadamu upo kimaumbile – maumbile ya mtu kamwe hayatakosewa na yale ya mnyama wa mwituni. Lakini fikira, tabia, kimo, uwezo na mahitaji huwa tofauti kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Kwa mintarafu hii yapasa wakufunzi na wazazi kuwapa watoto wao widhaa mapema ili wachague kwa wakati unaofaa kazi watakayoifanya maishani.

Watoto wanapopelekwa chuoni, wazazi wao huukilia kuwasomesha hadi kiwango fulani cha masomo kisha wajitafutie kazi ambayo itawapa masurufu na pesa za shughuli zingine maishani.

Katika nchi yetu tangu tupate uhuru mtindo wa kutoa kazi umekuwa ni ule wa kuchukua watu waliofaulu mitihani ya viwango fulani na kuwapa kazi moja kwa moja. Mwenendo huu wa kuajiri watu kazi umeendelea muda mrefu lakini sasa yamkinika utasitishwa na njia mpya kufuatwa. Sababu ya kufanya hivyo ni kuwa nafasi za kazi zimekuwa finyu sana. Kabla na punde baada ya uhuru nafasi hizo zilipatikana kila mahali. Nyingi ya hizo ziliachwa wazi na wageni walioihama nchi hii tulipojitawala. Siku hizi wanafunzi wanaokomea darasa la saba, kidato cha pili na hata cha nne huwa hawazioni ahadi za kupata kazi za madaraka fauka ya kazi yoyote. Wanaoiona tabasamu ya kazi mbele yao ni wale wanaotasawari masomoni wakifuata taaluma fulani.

Tatizo la kazi laeleweka vema kwa serikali na ni kwa ajili hii serikali imemtasulia kila mwananchi kuwa wakati wa kuania kazi za utanashati umetimiuka. Wakati uliopo ni wakati wa kujifunga vibwebwe kisaki na kuchapa kazi zile ambazo hadi sasa zafikiriwa kazi chafu na zisizofaa wasomi. Dhana kama hiyo ni ya kibwanyenye, na ubwanyenye hauji ila kwa sulubu. Usemapo kuna kazi nzuri na mbaya huwa unazusha maswali mengi. Utatakiwa ueleze kinaganaga kazi nzuri au mbaya kwa nini? Kazi huwa nzuri kwa upande wa tija au kwa upande wa wepesi wake? Kujibu maswali ya namna hii kutahitaji wekevu mwingi, waima mtesi ataonekana dufu.

Zipo kazi aina mbili. Ipo kazi ya kuajiriwa na ya kujiajiri. Kazi ya kujiajiri kwa kulinganishwa huonekana ngumu na yenye matatizo mengi mwanzoni. Lakini itakubalika pato lake ni kubwa zaidi ikishapata msingi imara. Msingi imara huwekwa kwa juhudi za mwanzoni zikiambatana na ujasiri. Mtu asiyejasiri kutenda tendo lolote maishani ni sawa na yule asiyejua atokako na kule aendako; yuaishi kungozwa. Ardhi ni thawabu, tena thawabu tunu. Ukiwa na kipande cha ardhi ifaayo kwa kilimo ufakiri ukikutawala ni wewe mwenyewe kupenda: la sivyo ufa umo ubongoni unaohitaji bwana mganga

(a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa taarifa, fupisha aya ya kwanza na ya pili. maneno 60-70)

(b) Kwa kuzingatia aya mbili za mwisho. Eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi. (maneno (50-60)

7. ***Soma taarifa ifuatayo kisha ufupishe taarifa hii kulingana na maswali yanayofuata:-***

Katika kipindi cha mwongo mmoja uliopita, tumeshuhudia mabadiliko na maendeleo makubwa kuhusu vyombo vya habari nchini Kenya. Hapo awali, redio ndicho chombo cha habari cha kipekee kilichotamalaki kote nchini. Familia nyingi ziliweza kumiliki chombo hiki. Runinga ilikuwa miliki ya wachache, hasa mabwenyenye. Sasa hivi, hata akina yahe nchini na mashambani wanamiliki chombo hiki.

Runinga kama kifaa kingine chochote cha mawasilianao kina manufaa yake. Kwanza kabisa, ni nyenzo mwafaka ya kufundisha. Vipindi vinavyopeperushwa katika runinga huwa na mafunzo kemkem kwa mtu wa kila rika. Hali kadhalika, runinga huweza kuleta vipindi ambavyo huwafahamisha watu mambo yanayoendelea katika mazingira yao na duniani. Aidha, runinga ikitumika pamoja na michezo ya video huauni katika ukuzaji na ustawishaji ya kufundisha au kujielimisha. Michezo ya video, hasa ya kielimu huwafanya watu kujenga umakini pamoja na kuchua misuli ya ubongo na kuwafanya watu kuwa macho wanapofanya kazi.

Fauka ya hayo, televisheni ni chemichemi bora ya kutumbuiza na kuchangamsha. Hakuna mtu asiyependa kuchangamshwa. Televisheni ni mojawapo wa vyombo mwafaka vya kutekeleza hayo kutokana na vipindi vyake. Uburudishaji huu hupatikana kwa urahisi majumbani mwetu.

Vivyo hivyo, runinga hutumika kama nyenzo ya kuendeleza utamaduni, kaida na amali za jamii. Vingi vya vipindi vya runinga ni kioo ambacho huakisi mikakati na amali za jamii.

Kwa upande mwingine, hakuna kizuri kisichokuwa na dosari. Licha ya manufaa yake, televisheni imedhihirika kuwa na udhaifu wake. Kwanza, baadhi ya vipindi vya runinga na video hujumuisha ujumbe usio na maadili, kama vile matumizi ya nguvu za mabavu, ngono za kiholela, lugha isiyo ya adabu, ubaya kimavazi na maonevu ya rangi, dini, jinsia , kabila na utamaduni. Si ajabu kuwa baadhi ya vijana wetu wanaiga baadhi ya mambo haya. Vijana wetu siku hizi wameingilia ulevi wa pombe na afyuni, ngono za mapema kabla ya ndoa na mavazi yanayowaacha takribani uchi wa mnyama. Wengi wamekopa na kuyaiga haya kutoka katika runinga. Ukiwauliza wafanyacho, watakujibu kuwa ni ustaarabu kwani wameupata katika runinga.

Matumizi ya runinga na michezo ya video yasiyodhibitiwa huweza kuwa kikwazo cha mawasiliano bora miongoni mwa wanafamilia. Matumizi kama haya huwapa wanafamilia fursa ya kujitenga. Imedhihirika kuwa runinga haichangii kujenga uhusiano bora wa kijamii ukilinganisha na vyombo vingine vya burudani ambavyo hutoa nafasi ya watu kutangamana na kujenga uhusiano bora, televisheni haichangii haya. Badala yake, tajriba ya televisheni huwa na kibinafsi. Hali hii inapotokea katika kiwango cha familia, televisheni inaweza kutenganisha wazazi na watoto wao.

Halikadhalika, runinga na video aghalabu hueneza maadili yasiyofaa. Mathalan, baadhi ya vipindi vya televisheni huendeleza hulka ya kuhadaa, ngono za kiholela, kuvunjika kwa ndoa, n.k. Hulka hizi zisizoendeleza maadili ya kijamii huchukuliwa kama zinazofaa na zinazofuatwa na waliostaarabika. Huu ni upotovu.

Isitoshe, baadhi ya matangazo huhimiza matumizi ya madawa ya kulevya kama tembo na sigara. Vitu hivi vinapotangazwa, hupambwa kwa hila na udanganyifu mwingi ambao huwavutia vijana na watoto wengi. Si ajabu mtu anapouliza wanaoutumia vileo hivi walivyoanza, watajibu kutokana na athari za matangazo katika runinga na vyombo vingine.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Utafiti umeonyesha kuwa vipindi vya runinga na video ni chanzo cha matumizi ya nguvu za mabavu miongoni mwa wanafunzi. Wazazi wengi huchukulia vibonzo katika televisheni kuwa vinalenga kuburudisha tu na havina ubaya wowote. Lakini ukweli ni kuwa vipindi vingi vya vibonzo hushirikisha matumizi ya hila na nguvu za mabavu. Haya huibusha hamu ya vijana na watoto huyaiga.

Kwa hivyo, ni muhimu wazazi na jamii kutambua madhara ya televisheni. Utambuzi huu utawafanya waelekeze vijana na watoto jinsi ya kutumia televisheni na video ili kuepukana na madhara yake.

**Maswali**

(a) Ukitumia maneno 50-60, fupisha manufaa ya runinga

(b) Fupisha hasara za runinga ukitumia maneno 70-80

8**: Ufupisho**

***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yafuatayo.***

Uhalifu ni tendo lolote linalokwenda kinyume na matarajio ya watu, jamii, au taifa na linaloweza kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria zilizopo ambao unakwenda kinyume na sheria za kidini au kanuni za kimaadili. Kwa mfano, mwananchi anayemwona mwenzake akiibiwa mkoba wake na kusimama bila kufanya lolote, amefanya kosa la kimaadili. Lakini tuangalie ni matendo yapi ambayo yanachukiliwa kama yanayokwenda kinyume na sheria za nchi, yaani matendo ya kihalifu?

Kuna matendo ya kihalifu yanayotendwa dhidi ya usalama wa umma au maadili ya jamii. Uhalifu dhidi ya mtu mwingine unahusu kitendo kinachomwathiri mtu mwingine kama mauaji, ubakaji na unajisi, wizi na ushambulizi. Uhalifu dhidi ya mali ambapo hapana uhusiano kati ya mtu mmoja na mwingine, huhusisha wizi wa kuvunja nyumba, uchomaji magari, uchomaji moto mali, wizi, na uharibifu wa mali. Uhalifu unaohusisha usalama wa umma na maadili unahusisha matendo kama uchezaji kamari, ukahaba, uvunjaji wa sheria zinazohusiana na matumizi ya dawa, udanganyifu unaohusisha amana au mali ya umma na ulevi.

Uhalifu pia huweza kuainishwa kwa kutegemea adhabu anayopewa mhalifu anayehusika. Kuna makosa makubwa au makosa ya jinai na makosa madogo kisheria. Makosa ya jinai ni yale ambayo yanahusisha kifungo gerezani aghalabu cha zaidi ya mwaka mmoja. Kwa mfano, wizi wa kutumia nguvu, uporaji wa magari, mauaji na ubakaji ni makosa ya jinai.

***Swali:***

**Kwa maneno yasiyozidi themanini, fupisha hoja kuu katika aya mbili za mwisho.**

**9. Soma taarifa hii kisha ujibu maswali:**

Ukeketaji ni mfumo wa upasuaji unaofanyiwa wanawake na wasichana sehemu nyingi duniani. Istilahi hii ya ukeketaji ina maana pana kwani inaweza kutumiwa kuelezea upashaji tohara kwa wasichana na ukataji wa sehemu za siri kwa wanawake.

Ukeketaji haupatikani tu katika bara la Afrika bali katika sehemu nyingi ulimwenguni. Umri ambapo ukeketaji hufanyika hutegemea jamii inayohusika. Mwanamke anaweza kufanyiwa ukeketaji siku chache baada ya kuzaliwa au baada ya kujifungua mtoto wake wa kwanza. Miongoni mwa jamii ambazo hupasha tohara wanawake, huthamini sana amali hii kwani kwao ni hatua muhimu ya mpito wa maisha katika jamii za jadi mwanamke hupitishwa kutoka rika moja hadi lingine, yaani kutoka utotoni na kuingia kwenye utu uzima. Ukeketaji unafungamana na sherehe ya kuwapa wasichana mafunzo kuhusu kanuni za uzazi, malezi na ndoa. Dhima kuu ya sherehe hiyo ya kuwapasha wasichana tohara inadaiwa ya kwamba ni kuwapunguzia wanawake uchu na kuhifadhi ubikira. Jamii nyingine hutekeleza tohara kwa sababu za kidini zinazoshikilia kuwa mwanamke aliyetahiriwa huwa nadhifu. Wengine wanaamini kuwa tohara huwafanya watoto wanapozaliwa kuwa na nafasi nzuri ya kuishi, ilhali wengine hupashwa tohara ili wapate waume wa kuwaoa. Kwenye jamii ambazo wanaume wanasisitiza tohara kama kigezo cha mwanamke kuolewa ukeketaji umeshamiri. Katika jamii kama hizi wanaume huwa hawataki kuoa wanawake ambao hawajatahiriwa.

Wanawake wenyewe huhakikisha ya kwamba watoto au wajukuu wao wanapelekwa kupashwa tohara. Wakati mwingine mipango ya siri hupangwa na kina mama hao pamoja na mangariba, kuhakikisha kuwa jambo hili linatekelezwa. Kwa hivyo jambo hili la ukeketaji lina utata miongoni mwa jamii nyingi ulimwenguni.

Hata hivyo ukweli ni kwamba swala zima hili la ukeketaji lina madhara makubwa na linamdhalilisha mwanamke. Katika hali ya upashaji tohara wanawake huvuja damu nyingi na aghalabu huaga dunia. Wale wanaopona huwa kwenye hatari ya kuambukizwa maradhi ya zinaa ambayo huharibu sehemu za uzazi. Kwani madaktari wanadai uchungu wa uzazi huwa mwingi na hudumu muda mrefu.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Kwa sababu tohara hufanywa mara moja kwa mwaka, wasichana wote wa rika moja hukusanyika mahali maalum ili kufanyiwa tohara. Kifaa ambacho hutumiwa sana ni wembe. Wembe huo hutumiwa kuwakatia wasichana wote ambao wanapashwa tohara katika kipindi hicho. Wembe huo hauchemshwi anagalau kuua viini vinavyosababisha na kueneza magonjwa mbalimbali. Hali hii huwaweka wasichana hao kwenye hatari ya kuambukizwa ugonjwa hatari wa ukimwi. Licha ya hivyo wasichana waliotahiriwa nguvu za kinga dhidi ya magonjwa hupungua. Kwa hivyo wanaweza kupata magonjwa mengine ya kuambukiza kwa urahisi. Kwa hivyo ukeketaji ni tendo la hatari na la kumdhalilisha mwanadamu ambalo linastahili kulaaniwa.

(a) Ukizingatia mambo muhimu anayoeleza mwandishi, fupisha aya tatu za kwanza. Maneno (60-70) (alama 9)

**Nakala chafu.**

**Nakala safi.**

(b) Eleza mambo anayoeleza mwandishi katika aya mbili za mwisho. Maneno 40-50 (alama 6)

**Nakala chafu.**

**Nakala safi.**

## 10. UFUPISHO

**Soma makala haya kisha ujibu maswali yafuatayo.**

**HAKI ZA BINADAMU**

Binadamu wana mazoea ya kufikiria kuwa jinsi wafanyavyo, waongeavyo na wafikiriavyo kuhusu vitu ndivyo inavyopasa kuwa. Kama binadamu tunaamini njia yetu ndiyo sahihi, yenye mantiki na inayopasa kufuatwa na kila mtu. Msingi huu huu unakwenda kinyume na kutambua kila binadamu ana haki ya kufikiri, kusema au kuongea na kutenda mradi asikiuke haki ya mwenzake iliyo sawa na yake. Nguzo mojawapo *inayogongomelea hoja* hii ni Haki za Binadamu.

Azimio la kutangaza Haki Bia za Binadamu liliafikiwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 10 Desemba, 1948. Baraza kuu hilo liliyasisitizia mataifa wanachama umuhimu wa kuyasambaza, kuenezea, na kusisitiza kusambazwa kwa azimio hilo katika shule na taasisi za kielimu. Msingi wa uhuru, haki na amani ulimwenguni ni kutambua binadamu wote wana haki sawa. Ingawa kimsingi jamii na mataifa yote ya ulimwengu yanapaswa kuthamini, kusambaza na kuhimiza umuhimu wa Haki za Binadamu zipo jamii ambazo hukiuka haki hizo. Matokeo ya ukiukaji huu yana athari hasi sana kama ilivyotokea nchini Rwanda na Bosnia. Herzegovina kulikotokea mauaji ya halaiki.

Azimio la Haki za Binadamu linajumuisha vipengele kadha ambavyo ni mihimili mikuu ya Azimio lenyewe. Kipengele msingi kabisa kinasisitiza kuwa kila kiumbe anazaliwa huru na ana haki na hadhi sawa na kiumbe mwingine. Ukweli wa kauli hii ulikokotezwa na kauli ya mwanafalsafa maarufu Jean Jacques Rosseau aliyesema kuwa kila kiumbe huzaliwa huru lakini huwa katika pingu ulimwengu mzima. Kauli hii ilitambua ukiukaji huu wa kipengele hiki. Kipengele cha pili kinasisitiza kuwa binadamu wote wana haki za kufurahia uhuru wao pasi na kutengwa au kubeuzwa kwa misingi yoyote ile si rangi, kabila, jinsia, lugha, dini, asilia, utajiri au chochote kile.

Vipengele vingine vinatukumbusha kuwa kila mtu ana haki ya kuishi na kupata ulinzi. Hamna mtu anayepaswa kuishi maisha ya utumwa au unyonge wa kutumikishwa kwa namna yoyote ile. Suala hili linasisitizwa na kipengele cha sita kinachokataza kudhalilishwa kwa watu au kutunzwa kwa namna yoyote ambayo inamfedhehesha kama kiumbe. Azimio la Haki za Binadamu linasisitiza kuwa binadamu yoyote yule ana haki ya kupata ulinzi wa kisheria. Binadamu huyo hapasi kubaguliwa na ana haki ya kupata fidia ya kisheria taraa haki zake za kimsingi zikikiukwa.

Hata hivyo sio watu wote ulimwenguni ambao wanazifurahia haki hizi za kimsingi. Zipo *lukuki za jamii* ulimwenguni ambako haki za kimsingi zinakiukwa. Katika nchi ambazo zinaongozwa na watawala wa kiimla, si ajabu kuona haki za binadamu zikikiukwa. Viongozi wa aina hiyo huwa wamegeuzwa ng'ombe wa shemere na tamaa, ubinafsi na ukatili usiojua thamani ya utu. Viongozi wa aina hii wanasahau kuwa kila binadamu ana haki ya kuishi maisha huru, asipotumikishwa wala kulanguliwa kama bidhaa.

Nchi za kiimla aghalabu huongozwa na itikadi kuwa kiongozi ndiye pekee ambaye ana uwezo wa kufikiri, kuamua na kutenda. Watu wengine wanapaswa kumfuata kisilka kama yule mbwa wa Pavlov ambaye alitokwa na mate kila kengele ilipopigwa. Viongozi wa aina hii hawachelei *kuwatenza nguvu* raia zao; kuwadhalilisha kwa namna nyingi. Viongozi wa aina hiyo huiona sheria ya nchi kama iliyowekwa kwa watu wengine bali sio wao.Msimamo huu unakwenda kinyume na kipengele cha saba cha Haki Bia za Binadamu kisemacho kuwa watu wote ni sawa mbele ya sheria.

Baadhi ya haki zinazokiukwa katika jamii za kimabavu ni haki ya watu kuungana, kuwaza, kushiriki katika maamuzi ya serikali, kuwa mwanachama wa jumuia waitakayo, kumiliki mali, kutembea, kuishi anakotaka, kutohukumiwa bila ya kuwako na utaratibu wa kisheria. Ni muhimu hata hivyo kujua ni muhimu kwa raia wenyewe kujielimisha na kuzijua haki zao. Serikali inapaswa kuwa mlinzi wa sheria zenyewe. Lakini muhimu kujua pia kuwa mlinzi naye hulindwa pia.

a) Kwa maneno kati ya 90 – 100 fafanua Haki Bia za Binadamu zilizoafikiwa na Baraza kuu la umoja wa Mataifa. (Alama 10)

**Nakala Chafu**

**Nakala Safi**

b) Kwa nini viongozi wa kiimla hukiuka haki za binadmu. (Maneno 50 -60).

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

**Nakala Chafu** **(Alama 5)**

**Nakala Safi**

## 11.<u>UFUPISHO</u>

**<u>Soma makala yafuatayo kisha uiibu maswali yanavofuata.</u>**

UGONJWA wa utando wa ubongo ambao kwa kiingereza unafahamika kama *meningitis* huzua hofu miongoni mwa watu wengi. Ugonjwa huo pia hujulikana kama homa ya uti wa mgongo.

Hofu kama hizo zinaeleweka kwa sababu utando wa ubongo ni ugonjwa unaoathiri ngozi inayofunika ubongo na uti wa mgongo na kwa hivyo ni rahisi mno kusababisha kifo ikiwa mgonjwa hatahudumiwa haraka iwezekanavyo.

Utando wa ubongo ni ugonjwa unaosababishwa na virusi na bakteria, Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, utando wa ubongo unaosababishwa na virusi sio hatari sana kwa uhai wa mtu ikilinganishwa na bakteria. Japo watu wengi wanaougua utando wa ubongo hutibiwa na kupona, baadhi yao huachwa wakiwa bubu au vipofu na wengine kufariki.

Shida kubwa ya ugonjwa huu ni kwamba unatokea bila kutarajiwa. Kwa mfano mtoto au mtu wa umri mkubwa anaweza kuwa mzima kwa muda wa dakika kadha ila baadaye kuwa mgonjwa mahututi baada ya kukumbwa na ugonjwa huo. Shida nyingine ya ugonjwa huu ni kwamba huwa vigumu kutenganisha dalili za ugonjwa huu na dalili za magonjwa mengine ya kawaida kama vile maumivu ya kichwa. Kwa hivyo kuna baadhi ya watu wanaomeza dawa za kupunguza maumivu ya kichwa bila kujua wanaugua utando wa ubongo.

Dalili za watoto wanaougua utando wa ubongo ni homa, kutapika, mtoto kukataa kula na kulia kwa uchungu. Mtoto anayeugua ugonjwa huu kadhalika huwa anaonyesha dalili za kufura kichwa, kupumua kwa haraka na kutupatupa miguu huku mwili wake ukiwa umejikunyata. Watu walio na umri mkubwa nao huonyesha dalili za maumivu makali ya kichwa, kuwa na shingo nzito (stiff neck) na mgonjwa kuepukana na mwangaza. Kadhalika mgonjwa hushikwa na homa na pia kutapika kando na kukosa ufahamu.

Utafiti umeonyesha kwamba watu walio na umri mkubwa kadhalika huonyesha dalili za kuwa na mikono au miguu baridi, maumivu ya misuli na tumbo hasa kutokana na damu kuwa na sumu. Ni muhimu kufahamu kwamba sio kila mtu anahisi dalili hizi, ikiwa yeyote atashuhudia

baadhi ya dalili hizi itakuwa bora kufika hospitalini haraka kupata usaidizi wa daktari kabla ya ugonjwa huo kuzidi sana.

Yeyote anayeshuku kwamba anaugua utando wa ubongo anapaswa kupelekwa hospitalini mara moja. Hii ni kwa sababu ni rahisi mno kwa madaktari kutibu mgonjwa anayepelekwa hospitalini punde tu anapoonyesha dalili ikilinganishwa na yule anayepelekwa huko kama amechelewa.

## Maswali

a) Bila kubadilisha maana fupisha aya nne za mwanzo (Maneno 70-80)

( alama 7, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

b) Ukizingatia aya tatu za mwisho, eleza dalili za ugonjwa wa utando wa ubongo na huduma kwa mhasiriwa (Maneno 55-65) (alama 6, 1 ya utiririko)

**Matayarisho**

**Nakala safi**

## 12.UFUPISHO

***Soma habari ifuatayo kasha ujibu maswali***

Miaka mingi ya kutawaliwa na wakoloni iliwafanya wananchi wengi kupuuza umaarufu na uadilifu wa lugha ya kiswahili kama lugha ya taifa kwa manufaa ya kuarifiana habari mbalimbali kwa ufasaha na kuelewana vema.

Wakoloni pia waliwashawishi wananchi waone kwamba lugha ya Kiswahili ni kwa ajili ya watu wale wasiokuwa na elimu na kwa wale ambao hawajastaarabika. Kwa wale 'wenye' elimu na

wastaarabu', wakoloni waliwashawishi kuamini kwamba lugha ya kigeni, yaani kiingereza, ndivyo hasa lugha inayofaa kwa kujieleza na kufahamisana habari.

Kutokana na vikwazo hivi si ajabu kuona hadi hivi sasa, mwananchi halisi akijitwaza kwamba hawezi kujieleza kwa ufasaha au kumpasha mwenzie habari kwa ukamilifu mpaka atumie lugha ya kingereza. Hata katika maofisi mengine ya serikali, hadi hii leo, japo imesha kupitishwa kisheria kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya taifa, bado utawaona wanaona wananchi wengine wanapendelea kuzungumza kiingereza wao kwa wao, ili wajulikane kwamba wana kisomo na wamestaarabika.

Vikwazo vya namna hii vimewalemea wananchi vile vile kwa upande wa magazeti. Utaona mwanainchi ambaye anafahamu kiingereza kidogo sana, akijinunulia gazeti kubwa la kingereza na kuanza kuzurura nalo kutwa nzima bila kuambulia mengi ndani yake. Pia utawasikia wananchi wengi wakijidai kwamba hawataki kusoma magazeti ya Kiswahili kwa sababu inakuwa vigumu kwao kuelewa mambo yaliyomo kama vile ambavyo wangelielewa katika gazeti la kiingereza.

Mabeberu wamesha tugundua kwamba tunao upotofu wa aina hiyo, ndipo utaona mara nyingi wanawaletea wananchi magezeti mengi ya kiingereza, mengine yakiwa na nia ya kuwapotosha wakijua kwamba watayasoma tu, mradi yameandikwa kwa lugha la kiingereza.

Mara nyingi taifa fulani la kibeberu likitaka tuchukiane na taifa jingine fulani ambalo ni adui yake kisiasa au kiuchumi, taifa hilo la kibeberu linaandika habari za uchochezi kwenye magazeti yao ya lugha ya kiingereza, mambo kuhusu taifa lile adui yake (ambalo si adui yetu). Magazeti hayo huandikwa kwa lugha nadhifu ya Kiingereza na kuletewa wananchi hapa nchini. Maskini wananchi wengine waliotopea kwa kudhani kiingereza ndicho lugha nzuri ya kigazeti, wanayanunua mara moja na kuanza kuyasoma magazeti hayo, na pia kuwapa watoto wao wasome. Matokeo yake ni kwamba, bila kujitambua, wanajikuta wanafanya yale Mabeberu waliyotarajia wayafanye, yaani wanaanza kuchukiana bure na taifa lile ambalo ni adui wa Mabeberu hao, lakini si adui zetu.

Madhumuni ya kuandika habari kwenye magazeti, ni kutaka kuwafahamisha wasomaji mambo yaliyotokea au yatakayo tokea siku hata siku,kwa lugha inayofahamika na kueleweka kwa urahisi bila kumtatiza masomaji ikiwa basi ndiyo madhumuni, kuna haja gani kutumia lugha

ya kigeni ili kuwaelezea wasomaji wako jambo ambalo wangaliweza kueleza kuelezwa kwa lugha yao wenyewe ambayo wanaielewa vyema. Mtu aelezewapo jambo lenyewe kutoka moyoni na akilini kwa njia adili ambayo anaifahamu vyema undani wake, huelezea jambo pia wasomaji wake wataielewa kwa ukamilifu. Kwa ujumla jambo ambalo mwandishi huyo ataliandika kwa lugha ambayo ni ya asili yake na ambayo anaielewa vyema, halitamtatiza msomaji wake ambaye pia anaielewa vyema lugha hiyo.

**Maswali**

(a) Fupisha aya tatu za mwanzo (maneno 30-40) (alama 6)

**Nakala chafu**

**Nakala safi**

. **Taja** mambo muhimu yaliyoshughulikiwa katika aya ya nne hadi ya sita (Maneno 50-60)

(alama 6)

**Nakala chafu**

**Nakala safi**

## 13. MUHTASARI

Hapo kale mfanyi-biashara mmoja alisafiri akenda kufanya biashara katika nchi ya mbali na kwao. Baada ya kuuza bidhaa zake alifunga safari ya kurudi kwao. Alisafiri msitu na nyika hata akafika kwenye jangwa. Ilimbidi alivuke hilo jangwa.

Mfanyi biashara huyo alisafiri siku kadha jangwani. Siku hizo za kale kulikuwa hakuna magari. Mfanyi-biashara alikuwa amepanda farasi. Baada ya siku chache farasi alichoka sana akaanguka na kufa. Mfanyi-biashara sasa ikambidi asafiri kwa miguu.

Hatimaye maji aliyokuwa nayo yalikwisha yote, akawa hana hata tone la maji ya kunywa. Kiu ilimbana lakini maji yalikuwa hayapatikani jangwani kote. Ilimpasa aanze kusafiri usiku usiku, kwa sababu mchana jua lilikuwa kali sana na angalisafiri wakati huo kiu ingalimzidi.

Baada ya kusafiri siku mbili tatu katika hali hii, alijiona hawezi tena kuendelea. Alikuwa yu hoi, alishindwa hata kunyanyua mguu. Kwa bahati siku ile alipita msafiri mwingine amepanda ngamia. Alipomwona mfanyi biashara katika hali ile alisimama na kumwangalia. Mfanyi-biashara alimwomba yule msafiri maji.

Msafiri alimjibu, "Maji niliyonayo ni kiasi ya kunitosha mimi tu, siwezi kukupa."

Mfanyi-biashara alisema, "Mimi ni tajiri sana. Milki yangu haihesabiki. Huko kwetu nina majumba na mashamba mengi. Mimi ni tajiri nikukabidhi mali hiyo yote nawe unipe hicho kiriba chako cha maji."

Msafiri alimjibu, "Mimi sina haja ya mali iliyoko nchini kwenu mali hiyo sitaweza kuitumia nchini kwetu."

Mfanyi-biashara aliwaza kisha akamwambia, "Hivi hapa nina kifuko kimejaa almasi na lulu. Hizi nilizinunua huko nilikotoka. Biashara ilinipatia faida nyingi sana. Je, utachukua almasi na lulu hizo zote, nawe unipe kiriba cha maji?"

Msafiri alikubali. Mfanyi-biashara alipata maji akanywa na kukata kiu yake. Maisha yake yakaokoka na kuepukana.

**<u>Maswali</u>**

(a) Eleza matatizo yaliyomkabili mfanyi-biashara katika safari yake toka mwanzo hadi mwisho wa safari. (Maneno 30 - 40) *(alama 8)*

***Nakala chafu***

***Nakala safi***

(b) Katika kila janga mfanyi-biashara alipita, kulijitokeza suluhu. Eleza jinsi hali hii inavyosawirika.
(Maneno 20 - 30) *(alama 6)*

***Nakala chafu***

***Nakala safi***

(c) Eleza kwa ufupi mambo muhimu yanayojitokeza katika mazungumzo baina ya msafiri na mfanyi-biashara. (Maneno 40) *(alama 6)*

***Nakala chafu***

***Nakala safi***

## <u>14.MUHTASARI.</u>

Katika kila kiwango, wanafunzi huonekana kama wana shida kubwa sana katika kuyachambua mashairi. Hali hii ni matokeo ya mambo mengi. Yaweza kuwa mashairi waliyokutana nayo mara

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

ya kwanza yalikuwa magumu, au yalikuwa yamechanganya kiswahili sanifu na lahaja zingine ambazo wasomi hawangezielewa moja kwa moja.

Jambo hili huwakatisha wanagenzi tamaa hasa wanapokosa kulipata katika kamusi msamiati uliotumika. Wanapotamauku, wao huwa hawataki kujishughulisha na mashairi. Huu ndio mwanzo wa kuanguka kwao katika mitihani kwa vile wengi wao hulazimika kukutana na mashairi kwa mara ya kwanza katika chumba cha mtihani. Hiki ni kinyume cha jinsi mambo yanavyostahili kuwa. Ukweli ni kuwa mashairi yanastahili kuwaburudisha wasomi pindi wakutanapo nayo.

Madai kuwa mashairi ya kiswahili ni magumu kufahamika isipokuwa kwa watu maalum wenye vipawa maalum hayafai. Mwanafunzi ambaye anataka kufanya vizuri katika swali la mashairi ni lazima aanze kuyapenda mapema iwezekanavyo. Ni muhimu aazimie kuyapenda hasa ajuapo kuwa atatahiniwa katika sehemu hii. Kwa vile hana njia ya kuyaepuka, azingatie msemo wa wazungu usemao kuwa kama hupati upendacho, anza kupenda kile ukipatacho. Ili kuchochea upendo ndani yake, asijishughulishe na yale mashairi ambayo anayaona kama ni magumu. Ajaribu kuyaelewa yale ambayo anayaelewa na kuudondoa ule ujumbe ambao yameumbeba na vile vile ajaribu kuufurahia utamu wa maneno yaliyotumika. Atalipata hili kwa kuyasoma kwa sauti. Kila mara, akumbuke kwamba kadili atakavyokutana na mashairi mengi ndivyo atakavyofurahia na kuyaelewa.

Pili, akikutana na shairi, asishtushwe na msamiati au lahaja iliyotumika. Hata kama haelewi msamiati uliotumika, ajaribu kuelewa ujumbe uliomo katika shairi. Hata hivyo, lazima ajihami na msamiati mwingi iwezekanavyo. Isitoshe, ni muhimu katika mazoezi yake kujaribu kuandika mashairi yake mwenyewe ili aelewe ni kwa nini waandishi huyaandika mashairi jinsi wanavyoandika; Atagundua kwa nini waandishi huyarefusha, huyafupisha au huyabadilisha maana ya maneno mbali mbali.

**Maswali.**

a) Ni mambo gani yanayochangia kuanguka kwa mwanafunzi katika swali la ushairi ? ***( alama 7) ( maneno 40)***

**Nakala Chafu.**
**Nakala Safi.**

b) Mwandishi amependekeza hatua gani kuchukuliwa ili mwanafunzi afaulu katika maswali ya mashairi **?** ***( alama 8 ) ( Maneno 50 )***

**Nakala Chafu**
**Nakala Safi**

c) Mwanafunzi ahitajika kufanya nini ili kuyapenda mashairi ***( alama 5) ( maneno 20 )***

**Nakala Chafu**
**Nakala Safi**

**SEHEMU YA TATU**
**USHAIRI.**

## 15.MUHTASARI

Babu na nyaya zetu waliweza kifundisha vijana mambo mengi na watu walikuwa wamenyooka sawasawa. Ilikuwa ni wajibu wa kila mzee kupitisha hekima yake kwa vijana kila mara kwa njia ya methali, vitendawili, shirikina na hadithi zenye mafundisho maalum. Mambo yote haya yaliwafanya vijana kuwaheshimu wakubwa kwa wadogo na watu wa marika yao. Watu walipokutana na wageni waliwaheshimu na waliheshimiwa. Ilieleweka kwamba neno 'heshima' lilikuwa la maana kwa kila binadamu na walijua kuwa heshima hainunuliki. Ilikuwa ni nadra sana kusikia zogo limetokea mahali popote.

Vijana wengi wa siku hizo walikuwa wakisifika kwa bidii, ushirikiano, uaminifu, utu, ukarimu, unyenyekevu, utiifu na upole. Wachache waliokosa sifa nyingi kati ya hizo walikosa wachumba. Hakuna aliyeweza kuficha tabia yake mbaya kwa muda mrefu kwa kuwa kila kijana pamoja na ndugu zake walifanya uchunguzi wa kutosha kabla ya kukubali posa. Upelelezi huu wa tabia ulianza tu mara mtu aliposema kuwa anataka jiko. Watu hawakujali ulemavu wa mtu na aghalabu waliokuwa na kasoro za kimwili waliweza kuoa ama kuolewa baada ya kuonekana kwamba wametimiza sifa nilizozitaja hapo awali.

Vijana walikubali kuelekezwa kutenda mambo mengi sana katika jamii bila ya maswali ama ubishi wowote. Hata walipoona mambo yamewawia magumu waliomba msaada kwa unyenyekevu mkubwa.

Hapo kale hapakuwa na mtindo wa vijana kupiga malapa mitaani. Waovu walikuwa wachache na waliweza kuadhibiwa na yeyote. Hakuna kijana aliyetoka kwao na kulala nje bila idhini ya wazazi wake na kama msichana angeweza kufanya hivyo, wazazi wangeweza kumlazimisha kurudi alipokuwa na arudi na huyo mtu aliyekuwa naye.

### Maswali

(a) Kulingana na taarifa hii, unafikiri ni mambo gani hasa yaliyochangia kuimarika kwa nidhamu kwa upande wa vijana? (Maneno 40) (alama 8)

*Nakala Chafu*

Nakala Safi

(b) Eleza ujumbe unaojitokeza katika aya ya kwanza (maneno 40) (alama 6)

*Nakala Chafu*

Nakala Safi

(c) Fafanua aina za makosa na adhabu zilizotolewa hapo zamani kwa mujibu wa taarifa hii (maneno 30-35) (alama 6)

*Nakala Chafu*

**Nakala Safi**

## 16. MUHTASARI

Wataalamu wengi wamelieleza neno hili fasihi. Kwa hivyo fafanuzi na nadharia juu yake ni nyingi. Lakini hata hivyo, karibu wote wamehusika zaidi ama na fasihi maandishi.

Ukitazama fasihi kwa umbo lake la nje na umbo lake la ndani utaona kuwa ni taaluma inayojengwa na maneno, na maneno yenyewe hutumia fani maalumu za aina mbali mbali kutolea

makusudi au maudhui ambayo humzingatia binadamu maishani… Japokuwa sanaa hii ya fasihi mara nyingine huzungumzia vitu, lakini hilo ni umbo lake la nje tu. Umbo lake la ndani hasa hujishughulisha na binadamu na ndiye kiini cha fasihi; ndiye shabaha yake.

Fasihi simulizi ni masimulizi tunayopokea mdomo kwa mdomo. Si masimulizi yaliyoandikwa tangu awali. Kwa ajili hii basi tutaona kuwa katika fasihi hii mna utumiaji wa ulumbi (ufundi wa kusema). Kwa vile chombo cha kutongolea fasihi simulizi ni mdomo, hapana budi kuwepo na mwenye huo mdomo, yaani msimulizi. Msimulizi huyo, anaposimulia anachosimulia, huwa na nafasi si ya kutumia mdomo wake tu kujieleza, bali hali, uso, mikono na mwili wake mzima. Nafasi hii mwandishi wa fasihi maadishi hanayo kwa sababu yeye, kinyume na msimulizi wa fasihi simulizi, huwa hanao mbele zake watu wa kumsikiliza au kumtazama. Badala yake yeye hupambana na msomaji.

Msimulizi katika fasihi simulizi ana nafasi ya kutazama kama amefaulu au la, yaani wasikilizaji wake wanamsikiliza au hawamsikilizi. Kama hawamsikilizi, basi huwa na nafasi ya kubadilisha mbinu wakati huo huo asimuliapo ili wamsikilize. Na hapo ndipo aonyeshapo ufundi wake katika sanaa ya usimuliaji. Lakini nafasi hiyo mwandishi hanayo anapoandika.

Tena msimulizi ana nafasi ya kuwatumia wasikilizaji wake kama wahusika asimuliapo ayasimuayo. Hii ndiyo sababu msimulizi aweza kumfinya mtu, kuigiza jambo, au kuwafanya watu waimbe, au kufanya matendo mbalimbali mengine. Ufundi na nafasi hiyo ni waandishi wachache wanaoimudu na kuitumia maana huhitaji umahiri wa hali ya juu. Kwa njia hii msimulizi kwa upande mmoja huwa na wahakiki palepale, hali mwandishi ni mpaka andiko lisomwapo ndipo anapoweza kuwapata.

Kwa upande mwingine, fasihi simulizi ina wasikilizaji zaidi kuliko wasomaji; wasikilizaji ambao mara nyingi waweza kuwa wahusika wa jambo linalosimuliwa. Wao wana nafasi ya kuuliza maswali, kuonyesha hisi zao, kuhimiza, kukumbusha, na hata kujibizana na msimulizi. Msomaji hana nafasi ya aina hiyo asomapo andiko.

a) Pendekeza anwani mwafaka wa taarifa hii. (alama 2)

a) Kwa kutumia maneno yasiyopungua kumi(10) wala kuzidi ishirini(20), eleza maana na lengo la fasihi kama ilivyotolewa katika taarifa. (alama 4)
**Nakala chafu**
**Nakala safi**

c)Mpokezaji wa fasihi andishi ana vikwazo gani akilinganishwa na yule wa fasihi simulizi? (maneno 70-80) (alama10)
**Nakala chafu**
**Nakala safi**

d) Wapokeaji wa fasihi simulizi wanawezaje kuathiri uwasilishaji wa fasihi? (maneno 20) (alama 4)
**Nakala chafu**
**Nakala safi**.

# 17.UFUPISHO.

**2. Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Ninashukuru wanafunzi wote wa dasara langu kwa kuhudhuria mkutano huu nilioitisha dakika ya mwisho. Najua walimu washaanza kukata vipindi vyote baada ya kumaliza mambo yaliyohitajika kufunza toka juzi. Na sasa mmepewa nafasi kubwa ya kujitayarisha vizuri zaidi kwa ajili ya mtihani wenu wa mwisho, lakini mimi nimeona kwamba upo muhimu wa kuzungumza na nyinyi katika dakika hii ya mwisho. Madhumuni si kufunza zaidi, maana hakuna tulichosaza kwa mujibu wa muhtasari wa masomo lakini ninataka kuwapeni maoni yangu ya mwisho kabisa . Hasa nitawaeleza yale ya kuzibia nyufa ndogondogo zilizobaki na pia kuwafunulia kunga za maisha ambayo wengine mtalazimika kuyakabili kwani ingawa sote tunawatakia heri mufaulu mtihani na hatuna shaka mtafaulu, yawezekana kwamba mtapata bahati mbaya katika mtihani na mlazimike kujiunga na maisha moja kwa moja.

Kwa kuwa tumefika ukingoni mwa safari yetu tuliyoianza miaka minne iliyopita, ninataka kuwapigia kengele ya mwisho. Hapa ninazo karatasi zenu za majaribio mliyoyafanya juma lililopita. Nina furaha kusema ya kuwa nyote mmejaribu maswali kama ilivyostahili. Hata hivyo msivimbishe vichwa mkaja mkachafua mambo dakika ya mwisho katika mitihani yenu. Wahenga wamesema, mgema akisifiwa tembo hulitia maji. Kumbuka hilo jaribio si mtihani wa mwisho, kazi bado ingalipo na inakukodoleeni macho .Pengine si vizuri kwa wakati huu kusoma sana na kukesha, lakini ni wakati wa kuzipiga brashi na kuzisafisha zile sehemu ambazo kila moja wenu anaziona hajazipitia vizuri , au hazijui vizuri au hajaziwekelea uzito. Zidini kujitayarisha vyema, zaidi na zaidi. Mkifanya hivyo, kila kitu kitakuwa wazi kwenu na mtaiona faida ya kazi na uvumilizi wenu.

Ningependa kusema kwamba sasa ninaosha mikono yangu kabisa sina ambacho ni cha lazima sijawafunza. Baadhi ya mengi mjuayo yatatahiniwa lakini mengine hayatatahiniwa kwani kutunga mtihani si kuandika kitabu , bali ni kutunga maswali ya kupima kama unajua mengi uliyofundishwa . Hata hivyo, kwa kuzijua nyanja zote za kiswahili zilizopendekezwa kwenye muhtasari wa masomo, hakuna kitakacho kushindeni.

Naomba myakumbuke maaso yote niliyowapa na jinsi ya kukabiliana na mitihani na hata ulimwengu wenu . Endeleeni na bidii yenu. Na hili la ulimwengu wenu ndilo la muhimu sana. Maana ya kufanikiwa katika mtihani si kufanikiwa na maisha. Maisha yanataka mbinu zake. Mnakokwenda nje ya kuta za darasa kuna ulimwengu, na wazee wamesema, asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. Ulimwengu msiuingie kwa hamu na pupa na kutaka kuyavamia yale yote ambayo mlikuwa mkiyakosa mlipokuwa shule. Mkitaka kufikisha kisugudi kabla vidole havijafika, mjuwe huenda mkavunja mikono yenu.

Ulimwengu una mengi ya kuvutia, lakini si kila zuri na la kuvutia ni zuri katika hakika yake. Vyengine vinang'ara, lakini si dhahabu. Na isitoshe si kila mtu miongoni mwenu ana uwezo wa kupata kila anachokitaka. Lazima wengine miongoni mwetu tujikune tujipatiapo. Tusiwaige watu ambao tunajua ukunjufu wao wa matumizi ulivyo. Hakika mwiga tembo kumeza boga, huchanika msamba.

Lazima katika dunia ya leo uishi pamoja na watu - yaani usijitenge, bali shirikiana na wenzako kwani ulimwengu wa siku hizi ni ulimwengu wa mtu kumtegemea mwenzake, hata ikawaje. Mheshimu anayekuheshimu, mfundishe heshima asiyekuheshimu . Wapende wazee wako, majirani zako, na zaidi ipe nchi yako nafsi yako.Ukipata kazi ithamini kazi yako, maana siku hizi kazi si kitu cha kuchezea .Kama hukupata kazi ya kuajiriwa,tumia akili ,busara na maarifa yako kujitegemea .Mengi mmefundishwa katika mfumo wa elimu

wa 8 : 4 : 4 ili mjitegemee. Si rahisi tena serikali kumpa kila mtu kazi. Usitahimilivu ni msingi wa maendeleo. Jengo halisimami kwa siku moja, lataka idili ya mchwa.

Hii sasa ndio hatima ya mimi kuwa nanyi kama mwalimu wenu wa kidato hiki na nyinyi ndio mwisho kuwa wanafunzi wangu. Tuna mengi ya kukumbuka. Tusisahau uhusiano wetu. Zaidi na watakia kila la heri katika mitihani yenu na maisha kwa ujumla .

(a) Eleza mambo muhimu katika aya ya pili ( maneno 50- 60 ) *(alama 7)*

(b) Eleza maaso ambayo wanafunzi walipewa katika aya ya nne. ( maneno 65-75) *(alama 9)*

(c) Mwalimu alitoa maaso gani kwa wanafunzi iwapo hawangebahatika kuajiriwa ? ***(maneno 35-40) (alama 4)***

## 18.

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali*

Ili kupiga vita propaganda za wakoloni mamboleo katika vyuo vikuu vyetu, inafaa kutumia Kiswahili kufundisha masomo yote. Jambo hili ni la lazima na linawezakana kabisa, ingawa lina matatizo yake. Jambo linalotakiwa kufanywa ni kuchukua wananchi wenye elimu ya juu wakatafsiri fikra za wazalendo katika Kiswahili. Kwa njia hiyo, lugha ya wanachuo itakua ndiyo lugha ile ile ya umma.

Ni jambo la kuepukwakuwana lugha mbili ambazo zinasaidiakuwatenganaumma. Wasomi wetu watakuwa wamekaribia umma kwa kutumia lugha iliyozoelekea na umma wenyewe. Jambo linalotutinga ni hili: mara nyingi wasomi wengine waliozoea kutakalamu lugha ya kiingereza wanapojaribu kuwaeleza watu wengine jambo la kielimu au kitaaluma, hushindwa kabisa. Wao huchanganya sana maneno ya Kiingereza na

Kiswahili hata kufikia kiasi ambacho mtu wa kawaida haelewi chochote.

Kwa kuwa wakoloni mamboleo wameelewa kwamba lugha ni kioo cha kiichuj ia utamaduni, iniaka ya hivi karibuni wamejifunza kwa dhati kuliko wakati mwingine kupigania ufundishaji wa lugha zao, hususan, kifaransa na Kiingereza. Wakati huo wao wanatoa porojo kuwa lugha ya Kiswahili haifai na kwamba ni lugha ya watumwa. Kwa mfano, utaona katika maandishi mengi kila wanapoorodesha lugha kuu za dunia.

Kiswahili hakionyeshwi katikahizo.

Badala yake wanaki weka kwenye kiwango sawa na kiganda, Kikuyu,

Kinyamwezi na lugha kadha wa kadha za kikabila. Hiyo na harakati kubwa ya kudanganya umma na kukivua Kiswahili hadhi yake ilhali lugha hii inatumiwa na zaidi ya watu milioni mia moja wanaosambaa katika sehemu mbalirnbali za ulimwengu. Kwa kutumia hila hii, wao wanawasadikisha watu wengi watu wengi ili wachukulie Kiswahili kama lugha nyingine ya kikabi la. Ndiposa hawa wakoloni mambo leo wanawashawishi baadhi ya watumiaji wa Kiswahili wastawishe lugha za makabila mbalimbali na kuonyesha kwamba umaarufu wa lugha hizo ni sawa na wa Kiswahili. Hayo bila shaka ni mawazo. Ukweli uliopo ni kwamba mawazo kama haya yaweza kuendeleza ukabila. Hata hi wo sharti tueleweke kwamba kusema hivyo si kudhalilisha umuhimu wa kukuza lugha za kikabila. Tusemacho ni kuwa ukuzaji wa lugha hizo ungekuwa na kusudi moj a kuu ambalo ni kustawisha Kiswahili kufikia ngazi za kimataif a

Swali ambalo ni muhimu kujiuliza ni hili: wakoloni - mamboleo wanatuonaje tunapokazania Kiswahili? Je wanaona ni faida kwao au kwetu? Jambo muhimu zaidi ni kutambua jinsi kiswahii kinavyotuwezesha kuungana na kuwa kitu kimoja. Ni dhairi kwamba wakoloni - mamboleo hawafurahii wanapoona Kiswahili kikituunganisha. Machoni mwao Kiswahili ni ishara mojawapo ya kujikomboa wetu kutokana na minyororo yao. Hivi si kusema kwamba hatupaswi kujifunza Kiingereza, Kifransa au

Kijerumani, la hasha. Tunachosema ni kwamba tutumie

Kiswahili ambacho ni kioo cha utamaduni wetu.

**Maswali:**

(a) Mwandishi amesema nini kuhusu utengano kati ya umma na wasomi?

(maneno 30-40) (alam4)

(b) Eleza pingamizi zilizowekwa na wakoloni -mamboleo ili kudunisha Kiswahili

(alam5)

c) Kulingana na mwandishi ni sababu gani zinazo fanya wakoloni mamboleo kupinga maendeleo ya Kiswahili? (alama 8)

# 19.

**UFUPISHO**

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali ,***

Mababu walituachia msemo maarufu kuwa "kuzaa si kazi. Kazi kubwa ni kulea." Busara iliyomo katika methali hii inatupambazukia peupe pindi tukianza maisha ya vij ana wa siku hizi katika jamii zote hasa zile za Afrika. Kwa upande mmoja, maisha ya vijana hawa yanaonyesha cheche ya matumaini kwa maisha ya siku za usoni kwa sifa zao za mori na kupenda kujaribu na kushika mambo upesi kama sumaku. Lakini kwa upande wa pili, tunashuhudia upotovu wa kimawazo ha hulka ambayo ndiyo kipingamizi cha kuendelea kwao kama raia wa kutegemewa.

Kuwanyeshea vijana'lawama na kashfa za kila aina hakufai wala haufui dafu katika juhudi za kuwaongoza na kuwalea. Kwa hili hatuna budi kusadiki. "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo." Basi hivyo badala ya kuwashambulia vijana hatuna budi kupeleleza na kurekebisha mbinu zote tuzitumiazo za kuwalelea na kuwaelii nisha vijana wenyevve. Tutafanya hivyo kwa imani kuwa "mwiba uchomeako ndiko utokeako." Kiini cha matatizo ya vijana wa leo ni namna ya mwongczo na vielezo wanavyopokea kutoka kwa wazazi, waalimu, vie ngozi wa kijamii wakiwemo pia wale wa madhehebu tofauti na hasa kutokana na vyombo tofauti vy habari, vitabu, majarida, filamu, magazeti na kadhalika.

Jamii ina haki gani kuwashtumu vijana iwapo mzazi, tangu utotoni mwao amewahubiria maji na huku mwenyewe anakunywa mvinyo? Kama fasihi na mandishi mengine wanayobugia vijana yamejazwa amali, picha, j azanda na tas wira zinazo himidi ugeni na kutweza Uafrika, tutashangazwa na nini pale vijana watakapoanza kupania zile amali za ugenini? Iwapo jamii na mazingira wanamokulia vijana yanatukuza kitu kuliko.utu, hatupaswi kupepcsa macho nakukonyeza tunapowaona vijana wakihalifu shfcria zote kwa tamaya kujinufaisha binafsi.

Ni hoja isiyopingika kuwa kulea sio tu kulisha na kuvisha au kumpeleka mtoto shuleni. Sharti itambulikane wazi wazi kuwa sehemu kubwa ya elimu na mwongozo unaoathiri mienendo ya vijana na watoto haitokani na yale waambiwayo bali hasa yote wanayoshuhudi kwa macho na hisia zao.

(a) Katika aya ya kwanza, maisha ya vijana wa kisasa yameelezwaje? (alama 6)

(maneno25-30)

Jibu

(b) Kwa nini vijana hawapaswi kulaumiwa kulingana na mw^andishi? (alama 8)

(Maneno30-35)

Jibu

c) Elezasifazamalezibora (alama6)

(maneno 20-25)

Jibu

# 20.MUHTASARI

***Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali***

Vijana wengi wake kwa waume, walikuwa ndio tu wakamilishe shughuli ya kusajiliwa chuoni. Walikuwa bado nadhari zao zimetekwa na ugeni$_y$ hawajapata starehe akilini mwao wala kujisikia wamekaribia kama kwao nyumbani. Kwa hakika mazingira yale mpya yalikuwa yanawapa kiwewe kidogo au tuseme hata woga kiasi. Kusema kweli, kwa wakati ule walikuwa hawajui ni maisha ya namna gani yanayowasubiri mahali pale. Hawakuweza kukadiria kwa uyakinifu wowote iwapo makaazi yao pale ya rniaka minne mizima kuanzia wakati ule, yangekuwa ya; ufculivu na raha au pengine yangeondokea kuwa ya roho juu juu na matatizo chungu nzima Walisubiri.

Walimsuburi Mkuu wa Chuo aingie wamsikize atakalosema, kisha ndipo waweze kubashiri vyema mkondo wa maisha yao utakavyokuwa. Lakini j insi walivyosubiri mkuu wa chuo aingie ukumb i ni ndi vyo wayo wayo 1 ao lilivyozidi kuwacheza shere, Waliwaza ugeni jamani kweli ni taabu. Mawazo

mengi yaliwapiti bongoni mwao. Wakawa kimya ukumbi mzima, kama kwamba wamekuja mazishini badala ya kuja kusoma. Waliwaza na kuwazua.*I* Waliona au pengine walidhani kuwa kila kitu ni tofauti.

Wanafunzi hawa waliona tofauti nyingi kati ya mambo pale chuoni na yale waliyokuwa wameyazoea. Kwa mfano, Mwalimu mkuu hapa hakuitwa 'headmaster' kama kule katika shule za msingi na vilevile shule za upili, bali aliitwa 'vice-chancellor'. Nyumba zakulala hazikuitwa 'dormitory' au 'mabweni' kama walivyozoea, bali ziliitwa 'halls' kwa sababu sio kumbi za aina yoyote ile bali ni nyumba hasa zenye vyamba vya kulala, kama nyumba nyingine zozote zile. Shule yenyewe haikuitwa shule au skuli, au hata chuo kikuu kama walivyozoea kuiita walipokuwa shule zao za upili huku, bali hapa wenyewe wenyeji waliita kwa majina mengine kabisa!. Mara Uni versity, mara

Zutafindaki, mara Ndaki kwa ufupi, mara Jamahiriya na kadahlika na kadhalika. Waliwaza kweli mahali hapa panaweza kumkanganya mtu! Kwakweli kabisa panaweza kumzubaisha mtu hadi kufikia kiwango chakuonekana kama zuzu! Hata hivyo hawakuvunjika moyo, bali walipiga moyo konde wakanena kimoyomoyo: potelea mbali! Ukiyavulia nguo yaoge! Walikuwa wamo katika hali hii ya kurandaranda katika ulimwengu wa mawazo pale katika ulimwengu mwingine kabisa usiofanana hata chembe na ule waliouzoea, Mkuu wa Chuo alipoingia.

Kuingia Mkuu wa Chuo, wote walisimama kwa pamoja na kwa mjiko, wamekauka kama askari katika gwaride. Kuona hivyo, Mkuu wa Chuo akawaashiria wakae tu, bila kujisumbua. Kicheko kikawatoka bila kukosa adabu na heshima, kisha wakakaa kwa makini. Ndio mwanzo wakajisikia wamepoa.

Kuona kuwa sasa wametulia na wamestarehe, Mkuu wa Chuo akaanza kwa kuwaamkua, kisha akawajulisha kwa wakuu wote wa vitivo mbali mbali na idara mbalimbali waliokuwa wamekaa pale jukwaani alipo yeye upande huu na huu.

Kufika hapo, alaka ikawa imeungwa baina ya wenyeji na wageni wao. Kila mtu akaona mambo yamesibu tena; huo bila shaka ni mwanzo mwema, na kama ilivyosemwa na wenye busara, siku njenia huonekana asubuhi. Hii kwa wote ndiyo asubuhi: na si asubuhi tu, bali ni asubuhi njema si haba. , .......

*(Baadaya kila swali umeachrwa nafasiya kuandaliajibu lako kablaya kuliandiku kikamilifu)*

a) Ukirejelea aya ya kwanza na ya pili, eleza wasiwasi wanafunzi waliokuwa nayo

wakati wakisubiri (maneno 45-55)

(alama7)

Jibu

(b) Ni mambo gani mageni ambayo wanafunzi hawakuyazoeleshwa katika kifungu?

(Maneno25-30) (alama3)

Jibu

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(c) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za mwisho kwa kutumia maneno yako niwenyewe

Tumia maneno 40-45

(alama10)

Jibu

## 21.UFUPISHO

***Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata***

Lugha ya Kiswahili ni lugha iliyoendelea sana. Leo hii lugha hii inasemwa na watu wote nchini Tanzania, Rwanda na Burundi. Inasemwa na watu wote nchini Kenya. Nchini Uganda, Zaire, Malawi, Msumbiji, Zambia, Somalia, Bukini (Madagascar) na Ngazija (Comoro), inasemwa na asilimia kubwa kubwa za wananchi wa huko. Aidha lugha hii ina wasemaj i si haba katika kisiwa cha Soktra na nchini Oman.

Fauka ya maendeleo haya, Kiswahili kinatumika kwa minajili ya matangazo ya habari katika idhaa nyingi za mashirika ya habari ulimwenguni. Nchi zenye idhaa za Kiswahili ni kama vile hizi zetu za Afiika ya Mashariki na ya kati, Afrika ya Kusini,

Nigeria, Ghana, Uingereza (Shirika la B.B.C), Marekani (Shirika la V.O.A), Ujerumani (Shirika la Radio Duetch Welle, Cologne), Urusi (Radio Moscow), China, India na kadhalika.

Maendeleo mengine yanapatikana upande wa elimu, Marekani peke yake, kuna vyuo zaidi ya mia moja vinavyofundisha Kiswahili kama lugha muhimu ya kigeni. Huko Uingereza, vyuo kama London, Cambridge na Oxford vinafundisha lugha hii. Nchi nyingine ambazo zina vyuo vinavyofunza lugha ya Ki swahili ni kama vile Japan Korea, Ghana, Nigeria na kadhalika.

Kweli Kiswahili kimeendelea jamani. Lakini kilianza vipi? Na ilikuwaje kikaweza kupiga hattia hizi zote?

Kiswahii kilianza kuzungumzwa na kabila dogo la watu waliokuwa wakiitwa Wangozi.

Watu hawa walikuwa wakiishi maliali palipoitwa Shungwaya. Shungwaya ni nchi ya zamani iliyokuwa eneo lililoko katika nchi mbili j irani ambazo siku hizi ni Kenya na

Somalia. Kabila hili la Wangozi liliishi jirani na makabila mengine kama vile Wamijikenda, Wapokorno, Wamalakote, (au Waelwʳana) na Wangazija (kabla hawajallamia visiwa vya ngazija). Lugha ya Wangozi siku hizo, ambayo ndiyo mzazi wa Kiswahili cha leo, ilijulikana kwa j ina Kingozi. Kama ilivyosemwa hapo awali, Kingozi kilisemwa na watu wachache sana.

Je, lugha hii ilikuwaje mpaka ikapata mendeleo haya makubwa tunayoshuhudia siku hizi? Ama kwa hakika, Kiswahili ni lugha iliyobahatika tu. Inaweza kusemwa kwamba lugha hii ilipendelewa na mazingira na historic.

Jambo la kwanza wageni waliotoka Mashariki ya kati kufikia hizi janibu zetu za Africa ya Mashriki walikaribishwa vizuri na hawa Wangozi. Wakaingiliana wageni na wenyeji kindakindaki, kjdini, kitwala, kibiashara na kitamaduni kwa jumla. Punde si Punde Wangozi, ambao walijulikana kama Waswahili na wageni hawa, wakaelimika katika dini (ya Kiislamu), biashara na mambo ya utawala aina mpya. Lugha yao nayo ikapanuka pale ilipochukua msamiati wa kigeni hususan wa Kiarabu na Kiajemi na kuufanya uwe wake, ili kueleza kwa rahisi zaidi mambo haya mageni katika taaluma za dini, biashara, siasa na hata sayansi kama vile unajimu. Wakati huo lugha ya Wangozi sasa ikitwa Kiswahili wala si kingozi. Tatizo hapa ni kuwa kwa vile Kiswahili kilichukua msamiati mwingi wa kigeni ili kuelezea taaluma hizi mpya, baadaye kimekuj ashukiwa kwamba ni lugha ya kigeni ilhali ni lugha ya kiaftika asilia, na kitovu chake ni nchi mpya za Kiafrika ziitwazo Kenya na Somalia hii leo.

(a) Thibitisha kuwa Kiswahili kimekuwa lughayakimataifa (maneno 35-40) (alama 6) Jibu

(b) Eleza kwa ufupi asili ya Kiswahili hadi kuja kwa wageni (maneno20-25)

(alama 4) Jibu

(c) Ukitumia maneno yakomwenyewe, elezaujumbe uliomo katika ayayamwisho

(maneno 50-60) (alama 10) Jibu

## 22.UFUPISHO

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Siku hiyo nilipitia mahali hapo kama yalivyokuwa mazoea yangu. Nilimuona yule mtu amelala pale pale, hatingishiki, kama nilivyokuwa nikimuona siku hizi zote, mwaka nenda mwaka rudi. Nilisimama huku nikishangaa kwa mara nyingine tena.

Nilikuwa najitayarisha kujiendea na hamsini zangu mtu huyo alipojipinda kwa mbali sana. Kwa hakika nilidhani macho yangu yananihadaa. Nikayakodoa zaidi ili nione vizuri zaidi ibura iliyonifunikia pale. Kwa muda, hakuna lililotendeka. Nikafikicha macho yangu nikitumia nishati yote iliyomo mwilini mwangu ill niyatoe matongo ambayo nilituhumu kwamba yalitia zingezinge nadhari yangu kiasi cha kunifanya kutoona barabara. Nilipohakikisha ya kwamba ni akili yangu tu iliyokuwa imenihadaa, nikaamua kuendelea na safari yangu kwenda kujitafutia riziki.

Hatua ya kwanza na ya pili, moyo haukunipa. Sauti katika kilindi cha moyo wangu.ikanisihi na kunitafadhalisha nitazame nyuma. Kutupa jicho nyuma, nikamnasa mtu huyo akigeuka! Nikashtuka sana! Jambo la kwanza nilidhani macho yameingiwa na kitu kilichoyafanya kuona mambo yasiyokuwepo. Pili nilidhani iwapo niliyoyaona yana msingo wowote, basi huenda ama nina wazimu, au yule mtu ni mzuka, hasa kwa vile ilionekana ni mimi tu nimuonaye. Nilikuwa nike katika hali ya kufanya uamuzi kuhusu dhana zangu hizi aina aina mtu huyo alipojigeuza, kisha akafunua macho! Moyo ulinienda mbio. Nilitaka kutifua vumbi ili wazimu usinizidie, lakini sikupata nafasi. Mtu yule alijizoazoa na kuketi kitako. Kisha akatokwa na maneno katika lugha iliyofanana sana na Kiswahili. Niliyaelewa aliyokuwa akisema

Ajabu ya maajabu, mtu yuyo alidai ya kwamba tangu alio lala kivulini hapo tangu jana baada ya chakula cha mchana, hakuota ndoto hata moja bali usingizi wake ulikuwa mithili ya gogo! Sasa nilikuwa na hakika kwamba ikiwa mimi sina wazimu basi kiumbe yule aliyevaa ngozi iliyochakaa sana katika rnpito wa miaka hakika ana wazimu. Nilitaka kuhakikisha, hivyo nilimkumbusha kwamba amelala mahali hapo kwa muda wa miaka mingi sana.

Kusikia hayo alianza kunikagua. Akasema nimevaa kizungu. Akanitajia tofauti nyingi baina ya vijana aliowazoea na mimi. Mwisho wa yote akaniuliza kama siku hiyo si tarehe kumi na nane mwezi wa pili mwaka wa 1897. Nikadhani anafanya mzaha kwa hivyo nikacheka. Nilipoona kicheko changu kinamuudhi, nikamwambia siku hiyo ni tarehe kumi na nane mwezi wa pili mwaka wa 1997. Nilipoona ameshangaa kwa dhati, nikagundua ukweli. Alikuwa amelala kwa karnenzima!

Maswali

(Baada ya kila swali umeachiwa nafasi unayoweza kuitumia kuandalia jibu lako kabla ya kuliandika kikamilifo)

(a) Eleza hoja nne muhimuzinazojitokeza katika aya tatu za mwanzo

(Maneno 75-85) (alama 12) NakalachaJEu:

B) Kwa maneno yako mwenyewe, fupisha aya mbili za mwisho bila kubadilisha maana. (Tumia maneno 40-50) (alama 8)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

# 23.UFUPISHO

***Soma makala yufi atayo kisha ujibumaswali***

Raha ni kitu gani? Je ni kitu kizuri au kibaya ? Mbona kila mtu hupigania na kama ionekanavyo, kila aionjaye hatimaye hunrvvunguza? Au pengine wakop wengine wasioungua? Hebu basi tuzingatie wale wasemekanao huitafuta sana raha na penginepo wakafanikiwa kuipata.

Chukua mfano wa msichana na mvulana wapendanao. Hawa wawili wanapopendana, lengo lao huwa ni kuoana na wakishaoana, waishi raha mustarehe milele. Hata hivyo, jambo la kwanza ni kwamba hata kabla hawajaoana, wanadhikika na kudhikishana kwa kutaka sana kuaminiana lakini kwa vile ni binadamu, wanatiliana shaka akila wanapokuwa mbali mbali. Watu hawa hulaumiana lakini kwa vile ni binadamu, wanatiliana shaka kila wanapokuwa mbali mbali. Watu hawa hulaumiana si mara haba wakati wakiwa wapenzi. Mara kadha wa kadha husameheana na kuendelea na mapenzi. Baadaye wakiwa na bahati huoana.

Mara tu wanapooana hugundua kuwa huko kuishi raha mustarehe ilikuwa ni ndoto tu ya ujana iliyotengana kabisa na uhalisia. Uhalisia unapowabainikia huwa ni kuendelea na huko kudhikishana, kutoridhishana, kutiliana shaka, kuombana msamaha na kuendelea tu.

Ama tumwangalie mwanasiasa. Huyu anapigania usiku na mchana ili awe mjumbe. Mwisho anachaguliwa lakini afikapo bunge, anakuta hakuna anayemtambua kama Bwana mkubwa. Inambainikia kwamba ubwana-mkubwa hautegemei kuchaguliwa tu bali unategemea mambo mengine pia, kama vile pesa nyingi magari makubwa makubwa, sauti katika jamii na wadhamini wanaotambulikana. Ralia kwa mwanasiasa huyu inakuwa mithili ya mazigazi tu, "maji" uyaonayo kwa mbali wakati una kiu kali sana, kumbe si maji bali ni mmemetuko wa jua tu.

Mwingine na kupigiwa mfano ni msomi. Huyu huanza bidii yake akiwa mdogo sana. Lengo lake huwa ni atambuliwe kote kwa uhodari wake katika uwanja wa elimu. Basi mtu huyu husoma mpaka akaifikia daraja ya juu kabisa yausomaji. Akapata shahada tatu : yaukapera,ya uzamili na ya uzamilifu. Akajiona yuu peoni mwa ulimwengu.

Akatafuta kazi akapata. Kisha akagundua kwamba watu hawakijali sana kisomo chake. Wakamwona ni kama mwehu tu. Fauka ya hayo wakamlaumu kwa kupoteza muda wake mwingi kupekuapekua vitabu wakamfananisha na mtu mvivu.

Mwisho tuangalie mfano wa mwanamuziki. Huyu analaghaika na wazo la kwamba sauti yake ikiwaongoa watu, atapendwa sana na wengi na kuwazuzua wengi kama mbalarnwezi au kuwaongoza kama nyota. Mtu huyu anapofikia kilele cha malengo yake, hata husahau kama ni binadamu wa kawaida, akawa anai shi katika muktadha wa watu kuzirai kwa sababu ya akili kujawa pomoni na upungaji wake. Watu hutamani hata kumgusa tu. Hata hivyo, mtu huyu huishia kujisikia mkiwa pale wakati unapowadia wa kupumzika. Je, raha yote huwa imekimbilia wapi?

(a) "Mapenzi ni kuvumiliana". Kwa maneno yako mwenyewe, eleza jinsi msemo huu ulivyo muhtasari mwafaka wa aya ya pili na ya tatu ya habari hii

(Maneno 30-35) (abmiaS) Nakalachatu:

Jibu:

(b) Kwa muhtasari, raha ni "asali chungu" Fafanua dai hili huku ukirejele mwanasiasa, msomi na mwanamuziki (Maneno 45-55) (alama 12)

Jibu

# 24.UFUPISHO

Yusuf Bin Hassan, Mflame wa mwisho wa halali wa Mombasa, alijitayarisha kuihama himaya yake. Alikuwa amewashinda Wareno, mahasimu wake, vibaya, lakini alijua watarudi na watamwadhibu vikali. Hivyo basi, badaa ya kusubiri waje wazitie baruti nyumba na kuzilipua, badala ya kungojea waje wawachinje raia wake kama kuku, badala ya kungoja ashuhudie minazi yote kisiwani na miti mingine ya manufaa kukatwakatwa na maktii hao, badala ya kuj itayarisha kichwa chake kukatwa j uu ya gongo, na mwili wake kuchanjwa vipande vipande aliamua auchome yeye mwenyewe mji, fauka ya kuikatakata miti yote ili Wareno wakija wasikute chochote cha kuvutia macho na watokomee kabisa. Alijua asipotekeleza uamuzi huo mkali, basi Wareno watakuja na hasira zote na kuadhibu waliomo na wasiokuwemo, kama walivyofanya

Unyama uliofanyika huko alikuwa ameusikia ukisimuliwa marazisizohesbika. Katika masimulizi hayo, alikua amesikia ya kwamba Falme hiyo ya Faza ilipoasi utawala wa kireno, askari wa Kireno, chini ya uongozi wa Martin Affenso de mello, walifanya unyama hapo mjini Faza ambao ulikuwa haujawahi kutokea, hata katika mawazo. Inavyosemakana ni kwamba Wareno waliamua kuangamiza chochote chenye uhai, hata wanyama na miti na wakautimiza muradi wao. Ajabu ni kwamba hata kasisi aliyeheshimika sana wa Kireno enzi hizo, baba Joan Dos Santos, aliunga mkono tukio hili akisema ya kwamba wafaza walistahili kuadhibiwa. Hakuna mtu hata mmoja upande wa Wareno aliyekilaani kitendo cha kutisha.

Hii ndiyo sababu Mfalme Yusuf na raia wake walipowazima wareno hapo Mombasa, aliwaamuru watu wake wahame, na yeye mwenyewe auangamize mji na chochote kilichomo, ili Wareno watakapokuja kulipiza kisasi wasikute chochote cha kuvutia.

Uamuzi mwingine aliofanya ni wa kivita. Aliamua ya kwamba Wareno hawawezi kushindika mahali pamoja pamoja kama vile Mombasa. Ilibainika kwamba ili kuwakomesha kabisa ilibidi watu wajitolee kuwashambulia kwenye vituo vyao vyote katika mwambao mzima wa mashariki ya Afrika. Baada ya kuamua hivyo aliendaUarabun kutafuta silaha ili atekeleze azimio lake.

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Alipopata zana za kutosha, ikiwa ni pamoja na silaha na meli, alianza kupambana na Wareno huko Uarabuni, mahali paitwapo Shihr. Halafu alielekea mwambao wa pwani ya Africa Mashariki ambako aliungwa mkono kila mji alioenda. Alifika hata Msumbiji ambako aliwasumbua sana maadui zake. Mwisho alikita makao yake Bukini ambako aliendelea kuwashambulia Wareno kokote walikokuwa.

(a) Eleza sababu zilizomfanya Mfalme Hassan kuuangamiza mji wake, na halafu kuuhama (maneno 30-40) (alama5)

(b) Ukitumia maneno yako mwenyewe na bila kupoteza maana, fupisha kuanzia aya ya pili hadi mwishc wakifungu. (Maneno 75-80) (alanial2)

Nakalachafu

Jibu

---

# MATUMIZI YA LUGHA

1. (a) ***Andika sentensi ifuatayo bila kutumia*** “**amba**”:-

(i) Jitu ambalo linatusumbua sharti liadhibiwe vikali

(ii) ***Weka sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea***:-

Mmea ambao unapandwa katika msimu wa masika unamea

(b) ***Badilisha sentensi hizi hadi usemi wa taarifa:-***

(i) “Nitarudi tu ikiwa mtakubali kuomba msamaha”. Juma alisema

(ii) “Elezeni vile mlivyokuja hapa na namna mtakavyokwenda.” Mwalimu mkuu alisema

***(c) Fuata maagizo uliyopewa baada ya kila sentensi ili kujibu maswali haya :***

(i) Aliogopa kumwangalia simba aliyekula mzoga. (Tumia neno ‘Ogofya’ bila ya kubadililsha ya sentensi:-)

(ii) Mti wa zambarau ni rahisi kukatwa ukiwa unatumia msumeno. (***Anza*** **Ni rahisi...**)

(d) **Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii** :-

Alimlilia mwanawe

(e) (i) **Kanusha sentensi hii:-**

Tungewalaki kama tungejua watakuja

(ii) **Sahihisha sentensi ifuatayo na uiweke katika wingi**:-

Ningalifanya kazi ningekuwa tajiri

(f) Tunga sentensi **nne** kuonyesha matumizi na maana nne za kijineno '**ki**'

(g) **Tumia kivumishi kilichoko kwenye mabano kukamilisha sentensi:-**

(i) Bibi yule alinunua gari ________________________(-pya)
(ii) Mti (-ingine) ________________________uliangushwa badala ya ule wa kwanza.

(h) **Unda majina mawili mawili kutoka vitenzi hivi na utumie katika sentensi ili kubainisha maana**

(i) Safiri
(ii) Zaa

(i) **Akifisha kifungu hiki**:-

Yohana na Emanueli walifunga safari wakielekea mashariki kusini na hatimaye magharibi walifikia huko novemba mwaka jana walipokuwa wakirudi walimkuta mwalimu mkuu njiani ambaye alishtuka kuwaona pale

(j) ***Geuza sentensi hii hadi udogo***:-
Nyoka yule mrefu alifukuzwa na watu wengi

(k) ***Andika upya sentensi hii kwa kuandika kinyume cha kila neno lilipigwa mstari***:-
Wifi **alipovaa** nguo na kusimama ajuza yule **alikaa**

(l) Sauti hizi ni za aina gani na hutamkwa wapi?
(i) **gh**
(ii) **j**

(m) Mahabusu walifyeka uwanja vizuri
**Andika sentensi hiyo upya ukimaliza kwa neno mahabusu**

**2.** (a) **Onyesha maneno yaliyokopwa toka lugha za kigeni na kuswahilishwa kwa kuyaongezea irabu** ***k.m. Bint (Kiarabu) – Binti***
Toa mifano minne

(b) *Andika sentensi ifuatayo kwa usemi halisi:*
Mwalimu alipoingia darasani aliuliza kitabu chake kilipokuwa.

(c) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi nafsi huru umoja

(d) **Kanusha sentensi hizi kwa wingi**:-
(i) Mtoto huenda shuleni kila siku
(ii) Mwalimu amemfunza mwanafunzi vizuri

(e) **Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo**
Wanafunzi waliandikiana barua

(f) **Ziandike sentensi hizi bila maneno yaliyopigiwa mstari:-**
(i) Mwanafunzi **ambaye** alituzwa ni wa shule yetu
(ii) Sikuziona nyuzi **ambazo** huzitengeneza ngoma **ambayo** huiona pale

(g) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vielelezo vya vishale:**
Kiarie ni mwanafunzi mtiifu

(h) **Bainisha ngeli za nomino hizi :-**
(i) Kisu

(ii) Nyavu
(iii) Chai

(i) **Ainisha viambishi katika neno lifuatalo** :-
Kilichokikata

(j) **Nyambua kitenzi 'oa' katika hali tatu zifuatazo: tendewa, tendwa, tendea**

(k) **Eleza matumizi manne ya nukta**

(l) **Onyesha shamirisho kipozi, kitondo na ala katika sentensi ifuatayo**:
Kamau alimlimia mamake shamba kwa trekta

(m) **Unda nomino kutokana na vitenzi hivi**:-
(i) Chapa (ii) Goma

(n) **Tambua kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii :-**
Chakula ambacho ni muhimu, huweza kujenga au kobomoa mwili wako.

(o) **Sahihisha sentensi ifuatayo:**
Ukienda mle pao atakuweko

(p) **Andika sentensi ifuatayo katika udogo:**
Mbwa mdogo amekanyagwa na gari.

3. (a) **Andika katika usemi halisi**
Mama aliwahimiza warudi siku hiyo la sivyo wangekosa tuzo

(b) **Andika kwa umoja**

Uovu waliotuonyesha hautasahaulika

(c) Tunga sentensi moja moja kuonyesha tofauti kati ya vitate vifuatavyo:

(i) Pamba
(ii) Bamba

(d) Sauti zifuatazo hutamkiwa wapi?

(i) /f/
(ii) /v/

(e) Onyesha matumizi **manne** ya kistari kifupi

(f) **Tunga sentensi ya neno moja yenye mofimu zifuatazo**

(i) Nafsi ya tatu umoja
(ii) Wakati uliopita
(iii) 'O' rejeshi
(iv) kitendwa
(v) mzizi
(vi) kiishio

(g) **Tambulisha aina za vitenzi vilivyotumika katika asentensi hizi**

(i) Kazi hii **ni** nzuri.
(ii) Mazingira **yamekuwa yakihifadhiwa.**

(h) Pigia mistari chini ya viwakilishi katika sentensi zifuatazo

(i) Ambaye ni mjinga hatafaa kwa shughuli hizi
(ii) Nani anaye huzunisha?

(i) Ngeli ya LI-YA hujumulisha nomino za vitu vya aina mbalimbali. Toa mifano **minne** ambayo ni tofauti na uelezee

(j) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo na ueleze ni shamirisho ya aina gani?

Wazazi wanalipia watoto karo kwa hundi;

(k) Neno **'tikiti'** hupatikana katika **ngeli mbili** tofauti. Taja ngeli hizo na utunge sentensi

(l) **Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale.**
Hakimu alimwadhibu kinyama.

(m) Nyambua vitenzi hivi kulingna na kauli ya kutendua na kutenda

| **Kutenda** | **Kutendua** | **Kutendama** |
|---|---|---|
| Ficha | | |
| Tanda | | |

(n) Ni nini maana ya neno kirai ?

**4.** (a) Kati ya nomino za Kiswahili taja **ngeli mbili** ambazo nomino zake hazibadiliki katika umoja
na katika wingi. Kisha utoe mfano mmoja kwa kila ngeli

(b) **Yakinisha:** Waumini wale hawaimbi wala hawaombi

c) **Andika kwa umoja**
Nguo zile uzionazo zilinunuliwa Ulaya

(d) Taja na kutolea mifano aina nne za silabi za Kiswahili

(e) **Unda nomino moja kutokana na nomino hizi**
(i) Mtu. (ii) Mhasibu..

(f**) Andika kwa ukubwa**
Kipaka hiki hakitosheki kwa maziwa haya kimezoea kipanya

(g) Onyesha shamirisho kipozi na shamirisho kidondo katika sentensi hii:-
Mama amempikia moto chakula kizuri

(h) **Tunga sentensi ya neno moja inayoonyesha sehemu zifuatazo**:-

(i) Kiambishi kikanushi nafsi
(ii) Kiambishi kiwakilishi cha hali timilifu
(iii) Kiambishi kiwakilishi cha kitendwa (nafsi)
(iv) Kauli
(v) Kiishio

(i) **Sahihisha sentensi hii kwa njia tatu tofauti**
Mtoto mwenye alicheza ameteguka

(j) **Andika visawe vya maneno haya**

(i) Rabsha..... (ii) Damu..

(k) Jaza mchoro ufuatao kwa irabu inayofaa

(i) (ii)

(v)

(iii)

(iv
)

(l) Tunga sentensi ukitumia **'ni'** kama

(i) kitenzi (ii) kielezi

(m) Andika katika msemo halisi

Johana alisema kuwa angepata alama zote katika majaribu ya wiki iliyotangulia

(n) Tumia '**O'** Rejeshi ya mazoea katika sentensi ifuatayo;

Jembe ambalo lilinunuliwa limepotea

(o) Changanua ukitumia mtindo wa mishale

Mtoto anayelia sana ameadhibiwa leo asubuhi

(p) Onyesha matumizi mawili katika sentensi ya alama (**'**)

(q) Wafuatao wana ulemavu upi?

(i) Toinyo . (ii) Huntha

**5. MATUMIZI YA LUGHA**

a) **Kanusha sentensi zifuatazo;** (alama 2)

(i) Uliugua malaria

(ii) Nimejenga kasri

b) **Andika nomino mbili katika ngeli ya U – YA.** (alama 2)

c) **Andika nomino zinazoweza kuundwa kutokana na vitenzi vifuatavyo.**(alama 2)

(i) Safiri

ii) Penda.

d) **Andika kwa umoja** (alama 2)

i) Machaka ya waridi hayazai maua meusi

ii) Walituandikia nyaraka ndefu.

e) **Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya kila kivumishi cha pekee ulichopewa.**

(alama 2)

i) -Ote

ii) –o-ote

f) **Onyesha vihisishi katika sentensi zifuatazo.** (alama 2)

i) Sawa sawa tutakutana kesho.

ii) Nabii Musa! Eti kifaru hula nyama

g) **Geuza sentensi zifuatazo katika <u>usemi wa taarifa</u>** (alama 4)

i) "Mabasi hayapiti hapa siku hizi, kuna nini" Mazrui aliuliza

ii) Karen: Tafadhali usiukanyage mguu wangu

Kadzo: Ah! Mbona niukanyage?

[h] **Ukitumia mifano mwafaka, tunga sentensi kudhihirisha matumizi mbalimbali ya;**

(alama 2)

i) Jinsi

ii) Ikiwa

i) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maelezo. (alama 2)

i) Mchwa wamezila mbao zetu zote. (Anza na mbao)

ii) Sijali hata kama hunipendi. (Andika kinyume)

j) **Kamilisha jedwali hili** (alama 4)

| Kitenzi | Kutenda | Kutendana |
|---|---|---|
| Fa | ………………………………. | ……………………………… |
| Cha | ……………………………….. | ……………………………... |

[k] **Ukitumia <u>mchoro wa matawi</u>, onyesha <u>muundo wa sentensi</u> ifuatayo.**(alama 4)

Mtoto huyu alikunywa maziwa mengi

[l] **Tofautisha maana za sentensi hizi.** (alama 2)

i) Ningalipandishwa madaraka, ningalinunua gari

ii) Ningepandishwa madaraka ningenunua gari

[m] **Eleza matumizi ya <u>ni</u> katika sentensi hizi.** (alama 2)

i) Njoo<u>ni</u> kwangu nyinyi nyote

ii) Dunia<u>ni</u> waja wote ni sawa

[n] **Taja aina ya vitenzi vilivyopigiwa mstari chini katika sentensi zifuatazo.**

(alama 2)

i) Huyu <u>ndiye</u> aliyetukomboa.

ii) Baba <u>amekuwa</u> mgonjwa

[o] a) **Eleza maana ya semi zifuatazo** (alama 2)

i) Kata bei

ii) Tia ngoa

p) **Kamilisha majina haya ya makundi.** (alama 2)

i) Mkungu wa ……………………………………………………………………..

ii) Thurea ya ………………………………………………………………………

c) **Andika visawe vya;** (Alama 2)

[q]i) Sarafu ………………………………………………………………………..

ii) Daktari ……………………………………………………………………….

6. a) Unda nomino kutokana na vitenzi hivi**.** (alama 2

(i) Sujudu

(ii) Haribu

(iii) Hiliki

(iv) Abiri

b) Onyesha silabi inayowekewa shadda kwenye maneno haya. (alama 4)

(i) Karatasi

ii)Samahani

c) **Akifisha kifungu kifuatacho** (alama 3)

Karibu mgeni akaitikia mwenyeji mbona huingii na mlango u wazi naam stareheni kwenye kiti ahsante wakajibu.

d) **Andika sentensi hizi kwa udogo.** (alama 2)

(i) Mlete huyo mwizi afunguliwe mashtaka.

(ii) Sijui kwa nini hindi lake ni bichi

(e ) **Andika sentensi hii kulingana na maagizo.** (alama 2)

Chombo kilichozama kiliandikishwa uingereza.

(Maliza kwa kiliandikishwa)

(f ) **Onyesha kinyume cha vitenzi vifuatavyo.** (alama 2)

(i) Epua

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(ii) Tapanya

(iii) Nena

(iv) Unga

(g) **Kanusha** ( alama 3)

(i) Chovi angekuwa na bidii angependwa na wengi.

(ii) Kilima kwake kulisifiwa sana.

(iii) Ukicheza na moto utachomeka.

h) **Geuza kwa wingi.** (alama 2)

(i) Njia hii huenda Kisumu

(ii) Wembe huu utafaa.

**i) Tumia kauli ya kutendesha katika sentensi zifuatazo:**. (alama 2)

(i) Mukhwana alikunywa pombe mpaka akalewa sana

(ii) Tafadhali hakikisha Omari ameelimika vizuri

j) **Changanua sentensi hii.** (alama 4)

Watoto wanafanya kazi zao lakini wazazi wanazungumza sana.

k) **Geuza katika msemo wa taarifa.** (alama2)

"Lo! Siamini kuwa yule mtoto aliyetaabika vile ameishia kupata udhamini" Alisema Mariamu

**l) Sahihisha sentensi zifuatazo.** (alama2)

i)Hao mandugu wamekosana juu ya pesa.

ii) Mtu mwenye anakula mkate ametumana aletewe chai.

m) **Eleza matumizi ya KWA katika sentensi zifuatayo:** (alama 2)

(i) Wanawake kwa wanaume walifika mkutanoni.

(ii) Yule mtaalam alielezea maana ya utandawazi kwa ufasaha.

n) **Fafanua maana mbili zinazojitokeza katika sentnsi hii.**(alama2]

Jambazi lilimwibia Okoth gari jipya.

o) **Tunga sentensi kubainisha maana tofauti ya maneno haya;** (alama 2)

i) Dalili

ii) Dhalili

p) **Toa neno jingine lenye maana sawa na;** (alama3)

i) Karadha

ii) Mtaji

iii) Mshitiri

q) **Eleza maana ya misemo hii.** (alama2)

i) Umbo la mkonge

ii) Kupata hiji wa hoja

r) **Eleza maana ya methali ifuatayo:** (alama2)

Akikalia kigoda mtii.

# 7. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

1. **Andika methali inayoafikiana na maelezo haya**

   Kwa kawaida, mtu hupendelea nafsi yake (alama 2)

2. **Andika katika udogo**

   Mwanamke alimuua mbuzi kwa shoka. (alama 2)

3. **Weka shadda katika neno 'barabara' ili kuibua maana tofauti ya neno hilo**

   i) Barabara (maana)

   ii) Barabara (maana)

4. **Tunga nomino mbili kutokana na vitenzi hivi. Hakikisha viko katika umoja. (Alama 2)**

| **Kitenzi** | **Nomino** | **Nomino** |
|---|---|---|
| Elewa | | |
| Suka | | |

5. **Onyesha mofimu katika neno lifwatalo na utaje ni za aina gani**

   Kilichowaumiza. (alama 3 ½ )

6. Tunga sentensi yenye mpangilio huu wa kisarufi. (alama 2 ½ )

   I + W + T + N + V.

7. **Tunga sentensi kudhihirisha maana tofauti kati ya**

   (a) Jozi

   (b) Njozi (alama 2)

8. **Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa.**

   "Ninataka kumwona askari aliyemletea mfungwa tupa sasa hivi," alisema Batu. (alama 2)

9. **Eleza na uonyeshe matumizi manne tofauti ya kiambishi 'ku'** (alama 4)

   (i) …………………………………………………………………………………………………

   (ii) ……………………………………………………………………………………………..

   (iii) …………………………………………………………………………………………….

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(iv) ……………………………………………………………………………………………….

10. **Kanusha sentensi hii katika wingi**

Mgonjwa mwenye kichomi aliyelazwa hospitalini ameaga dunia. (alama 2)

11. Changanua sentensi hii kwa kutumia matawi na useme ni sentensi ya aina gani

Wale wanafunzi stadi walioibuka na alama bora zaidi, wameajiriwa kazi.

a) Aina ………………………………………………………………….. ( alama ½ )

b) Mchoro (alama 7 ½ )

12. Onyesha virai vitatu katika sentensi hii na utaje ni vya aina gani.

Mtoto yule mdogo amekunywa maziwa kwa kikombe. (alama 3)

(i)………………………………………………………………………………………………

(ii)……………………………………………………………………………………………

(iii)……………………………………………………………………………………………

13. Tunga sentensi tatu ukitumia neno papara liwe na sifa hizi. (alama 3)

a) Kielezi

b) Nomino

c) kivumishi

14. Sauti hii hutamkiwa wapi na huitwaje?

|Ch| (alama 1)

## 8..MATUMIZI YA LUGHA

(a) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli zipi**?**

i) neno …………………………………

ii) mate ………………………………….

(alama 2)

(b) Eleza matumizi mbalimbali ya 'ni' katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Nendeni mkamwite Kanini ambaye ni mwanafunzi wangu niliyemwacha maktabani

(c) Taja ala zinazotumika katika kutamka sauti zifuatazo

i)/dh/ ………………………………………

ii)/gh/ ………………………………………..

(alama 2)

(d) Ainisha matumizi ya –ema katika sentensi ifuatayo (alama 3)

Mwanafunzi mwema ametunzwa vyema kwa wema wake

(e)Andika katika usemi wa taarifa (alama 2)

“Atamkuta papa hapa akija kesho”.Alisema.

(f) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia ‘o’ rejeshi na kiambishi ngeli

(alama 2)

Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.

(g) Andika sentensi zifuatazo kulingana na maagizo uliyopewa.

i) Tano ondoa tatu matokeo ni mbili (anza: Mbili…………)

(alama 1)

ii) Mwalimu huyu anafunza Kiswahili

(Maliza kwa kiashiria kisisitizi) (alama 1)

iii)Ng’ombe aliyekuwa nyuma ya ua alichechemea kwa vile aliumia ukwato wake.(andika kwa wingi)

(alama 2)

(h) Tunga sentensi ukitumia kisawe cha neno lifuatalo

(alama 2)

Ndwele

(i) Ainisha sentensi hii (alama 3)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Aliyenichokoza

(j) Geuza sentensi hizi ziwe katika kauli ya kutendewa (alama 4)

i) Muktubi amempa mwanafunzi jarida.

ii) Bate alivua samaki wengi.

(k) Tunga sentensi zinazoonyesha matumizi ya vihusishi katika hali zifuatazo (alama 4)

i) Uhusiano wa zaidi ya hayo

ii) Kuonyesha chanzo

(l) Changanua sentensi ifuatayo kwa vistari/vishale (alama 4)

Kandanda ni mchezo maarufu duniani

(m)Sahihisha sentensi ifuatayo (alama 2)

Wanafunzi ambao waliokuwa wakarimu walimpenda Bi Keti

(n) Yakinisha sentensi hizi (alama 2)

i) Asingeenda safari asingepata ajali

ii)Usije

o) Andika kwa wastani (alama 2)

Magoma hayo yatachezewa mawanjani

## 9.MATUMIZI YA LUGHA

(a) Weka nomino hizi katika ngeli lake. (alama 2)

  (i) Mvule

  Kipofu

(b) **Tunga** sentensi kuonyesha matumizi ya parandesi (alama 2)

(c) **Andika** sauti mbili zinazotamkiwa menoni (alama 2)

(d) **Changanua** sentensi ifuatayo kwa kutummia jedwali.

Mwanafunzi huyu mwerevu atapita mtihani vyema. (alama 4)

(e) **Andika** katika kauli ya kutendesheka. (alama 2)

  (a) Iga

  (b) Vaa

(f) **Onyesha** aina ya vitenzi katika sentensi.

Wewe umewahi kufika shule ukiwa umechelewa? (alama 2)

(g) **Andika** kulingana na maagizo yaliyotolewa. (alama 2)

Jina langu ni maliki lakini huitwa mali kwa kifupi. (Anza kwa: Watu -----------)

(alama 2)

(h) Kwa kutunga sentensi **eleza** tofauti kati ya:

Sentensi ambatano na sentensi changamano

(i) **Onyesha** aina za virai katika sentensi (alama 2)

Gari lao lilianguka kando ya jengo.

(j) **Unda** vivumishi kutokana na vitenzi : (alama 2)

  (i) Samehe

  (ii) Kakamaa

(k) **Eleza** matumizi ya viambishi vilivyopigiwa kistari. (alama 3)

  (i) Kaandika barua

  (ii) Nikisoma kwa bidii nitapita mtihani

  (iii) Oliech acheza mpira vizuri

(l) **Kanusha**.

  (i) Wakimenyanamenyana (alama 1)

  Ningefika mapema ningewahi basi hilo (alama 1)

(m) **Onyesha** aina za mofimu zilizopigiwa kistari. (alama 2)

Alisita alipofika chumba cha sita

(n) **Tunga** sentensi kubainisha: (alama 2)

(i) Inchi

(ii) Nchi

(o) **Sahihisha** sentensi ifuatayo.

Mkutano uliyohairishwa juma lililopita utafanywa leo (alama 2)

(p) **Andika** katika usemi wa taarifa:

"Nikifaulu nitamshukuru sana Mungu pamoja na wazazi wangu." Mungai alisema.(alama 3)

(q) **Andika** katika wingi:

Kuku wa jirani kijijini mwetu aliangua kifaranga aliyelemaa. (alama 2)

**10.**

A. (a) Eleza tofauti iliyopo katika jozi hii ya sentensi

Alimpatia soda na chupa

Alimpatia soda kwa chupa (alama2)

(b) *Kamiliska jedwali ukifuatia mfano uliopewa*

| | | |
|---|---|---|
| Wimbo | Mwimbaji | Uimbaji |
| Jengo | ........................ | ............. |
| Pendo | ........................ | ............ |

(c) *Taja vielezi vinavyopatikana katika sentensi hizi; kiska eleza nl vielei4 vya aika gain* (alama4)

(i) Aliamka alfajiri

(ii) Mtu huyu ni hodari sana

(d) *Andika kwa usemi kalisi*

Yohana alisema kwamba nj iani kulikuwa kumenyesha sana ndio sababu tulichikwa. (alama2)

(e) Tunga sentensi moja mojaukkttmia alama zifuatazo za udkifishaji

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(alam 4)

(i) ritifaa

(ii) parandesi

(iii) ckikuduku

(iv) mshangao

(f) Tunga sentensi ukionyesha niatumizi ya vitenzi vya silabi moja katika jinsi ya

kutendesha ukitumia silabi hizi ... (alam 3) (i) -la

(ii) nywa

(iii) fa

(g) *Taja na ubainishe aina za viwakilishi katika sentensi zifuatazo* (alama 4)

(i) He minazi yangu niliyopalilia inakua vizuri

(ii) Mimi niriataka kumwona mwanariadha aliyepata nishani ya dhahabu

(h) *Andika kwa wingi:*

(i) Uta wake nimrefunamkubwa sana

(ii) Merikebu itakayofika kesho itang'oa nanga keshokutwa

(i) Andika upya sentenzi zifiiatazo ukitumia neno amba (alama 2)

(i) Kijiti kilichovinjika kiliimwumiza Anmina mguuni

(ii) Barua zitakazoandikwa na baba kesho zitatumwa mwaka uj ao

(j) *Sahihisha sentensi hizi:* (alama 2)

(i) Bahasha ilionunuliwa jana ni kubwa na mzuri

(ii) Mananasi hizi zinauzwa ghali kwa sababu zimeiva vizuri sana

**11.**

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(a) *Kwa kutumia kirejeshi kifaacho₉ rekebisha sentensi ifuatayo kwa njia mbili tofauti*

Yulendiyeinkwasiambayealiyeniisurika (alama 2)

(b) *Andika umoja wa sentensi hizi:*

(i) Kwato za wanyama hutufaidi

(ii) Mnabdca vyeti vya kuwasaidia?

(c) *Andika ukubwa wa*

Mwizi aliiba kikapu na ng'ombe

(d) *Tunga sentensi sahihi ukidhihinsha wingi wa majina yafuatayo*

(i) Ukanda

(ii) Uzee

(e) *Sahihisha sentensizifuatazo bila kugeuza maana*

(i) Kikombechenyekimevunjikantkipya

(ii) Nimepeanakilabukwamwalimumkuu (alamal)

(f) *Tunaweza kusema katika chumba au*

(i) ………………………………………………………. (ii) ……………………………………………………….

(g) *Andika sentensi zifuatazo katika halt ya kutendewa*

(i) Yuleng'ombealizaandamanikubwajana

(ii) Mavu hawa wamemsumbua Nyatogo kwa muda mrefu

(h) *Kwa kurejelea ngeli za mahali, andika sentensi tatu ukionyesha matumiziya kila moja* (alama 3)

(i) *Andika sentenm za mseto kutokana na mbilifupi uizopewa*

(i) Mwanafunzi amesoma kwa bidii. Mwanafunzi anataka kupita mtihani

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(alamal)

(ii) Leonimerucknyumbani. Sipendelei kuishi hapa - (alama 2)

(j) *Geuza sentensi hizi kutoka msemo wa taarifa hadi msemo halisi*

(i) Mamaalisemanichukuenafakayetunikauzesokoni (alama2) (ii) Mwalimualiombaaletewevitabuvyake kutoka darasani (alama 2) (k) *Eleza maana mbili tofauti za sentensi hii.*

Wenzake wamelipwa pesa zao, yeye bado amelala (alama 2)

**12.**

(a) Eleza matumizi matatuyaKIna utunge sentensi moja kwa kila mojawapo.

(alama 6)

(b) Tambulisha viwakilishi nafsi katika sentensi zifuatazo, halafu u/igeuze sentensi hizokwawingi .

(i) Nilisomakitabuchake

(ii) Umekuwa mwadilifu kupindukia

(iii) Alishinda nishani ya dhahabu (alama 6)

(c) *Akifisha sentensi hit -*

Watu wengi warnezoea kusema ajali bwana basi yakaishia hapo lakini kufanya hivyo ni sawa. (alama 3)

(d) *Andika sentensi hizi kwa umola* (alama 2)

(i) Mafuta haya yanachuruzika sana

(ii) Miinuko ile ndiyo mwanzo wa milima ya Chungu

(e) *Sahihisha sentensi zifuatazo:* (alama 2)

(i) Kile kitabu kilipasuka ni changu (ii)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Mtotomwenyeameangukaninduguyangu

(f) *Kanusha:*

(i) Matawi ya mti ambayo yalikauka yalikatwa (alama 2)

(ii) Matofali haya yanatumiwa kwa ujenzi wa nyumba

(g) *Andika sentensi hizi upya ukitumia -o-te-*

(i) Chakula kikibaki hutupiliwa mbali (alama 2)

(ii) Kila nyumba unayoingia unapata watoto wawili

h) *Yapange majina yafuatayo katika ngeli zake*

(i) Neno...........................................

(ii) Kiongozi........................................

(iii) Mate........................................... (alama 3)

*j) Ukizingatia neno lililo katika mabano, andika sentensi hizi katika haliya kutendeka* (alama 2)

(i) Daraja hili(vuka)tu wa kati wakiangazi (ii) Kitabu hicho (soma) ijapokuwa sura zingine hazimo

(j) *Tunga sentensi ukionyesha matumiziya:*

(i) -enye (alama 2)

(ii) -enyewe

**13.**

(a) Tumia viashiria vya kutilia mkazo katika sentensi zifutazo

(i) Kibogoyo................ Ndiye anayehitaj i meno ya dhahabu

(ii) Vyakula................. mvipikavyo nyinyi, nasi twavipika

(b) Geuza sentensi zifuatazo ziwe katika haliya umoja

(i) Huku kuimba kwenu kuzuri kutawapendeza wageni

(ii) Hii miche ni mizuri sana, itatufaa (alama 2)

(c) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumiaviunganisliivifaavyo

(i) Chakula hiki hakina mchuzi. Hakina chumvi *(*alama 1)

(ii) Romeo aliamka. Alitazama saa yake Akaia kiamsha kinywa mbio mbio

(alama 2)

(d) Ziandike upya sentensi zifuatazo kwa kufaata maagizo uliyopewa

(i) Nimemleta paka ili aue panya wote wanaotusumbua hapa kwetu nyumbani

(anza: Panya......) (alama2)

(ii) Mbwa ambaye aliripotiwa kuwa ameibwa amepatikana katika bwawa la maji

(anza Katika bwawa.....) (alama 2)

(e) Andikakwamsemohalisi sentensi. Tajiri alishangaa kuwa niliweza kuubeba mzigo huo peke yangu (alama 2)

(f) Piga mstari vivumishi katika sentensi hizi

(i) Sina nguo yoyote niwezayo kuvaa (alama 1)

(ii) Mtoto mwenyewe ataileta kalamu (alama 1)

(g) Andika vitenzi vinavyotokana na majina haya;

(i) mfuasi (ii) kifaa

(iii) mharibu (alama 3)

(h) Kanusha

(i) Ungemwuliza vizuri angekujibu bila wasiwasi (alama 1)

(ii) Andika kinyume

Mjomba alichomeka upanga kwenye ala - (alama 2) (i) Eleza maana nne tofauti za sentensi hii

Alinunuliwa samaki na mtoto wake (alama 4)

(j) Eleza tofauti bainaya sentensi hizi

*(i)* Ningekuwa na pesa ningenunua shamba

(a) Ningalikuwa na pesa ningalinunua shamba (alama 2)

B.

(a) kamilisha tashbihi zifuatazo

(i) Baidika kama

(ii) Mzima kama

(b) Tumia tanakali za sauti zifuatazo kukamilisha sentensi hizi;

(i) Sauti ya waimbaji haikusikika tena, ilikuwa imedidima...... wageni walipoflka katika jukwaa

(ii) Simba ni mnyama hodari sana, akimkamata swara humrarua (alama 2)

(c) Tunga sentensi mbili tofauti zinazo bainisha maana tofauti kati ya: (i) Nduni (ii) Duni (alama 4),

(d) (i) Mdudu anayetengeneza utandu huitwa (alama 1)

(ii) Mdudu mwenye mkia uliopinda nchani ambao una sumu ni (alama 1)

(e) Andika inethali mojainayotokananamaelezoyafuatayo Asiye na uwezo ataendelea kuwa bila uwezo hata akifanya bidii namna gain (alama 2)

**14.**

(a) Andika udogo na ukubwa wa jina ngoma

(i) ____________

(ii) ……………..

(b) (i) Eleza namna mbili za matumizi ya alama ifutayo ya uakifishi (;)

(ii) Tunga sentensi mbili tofauti zinazoonyesha matumizi hayo.

(c) Tofautishamaanaza sentensi zifuatazo:

(i) Kazi yote ni muhimu

(ii) Kazi yoyote nimuhimu

(d) Tunga sentensi mbilimbili kuonyesha matumizi mawili tofauti ya:

Ka (i) ………………………..

(ii) ………………………

Ndivyo (i) ……………………….

(ii) ……………………….

(e) Tunga sentensi kuonyesha matumizi sahihiyaviunganishihivi

(i) ingawaje ______________________

(ii) ilhali _________________________

(f) Tambulisha kielelezi, kivumishi na mnyambuliko wa kitenzi katika sentensi ifuatayo: Msichana mrembo alikuja upesi akimkimbilia dadake.

(g) Andika kifungu hiki kutoka usemi wa taarifa hadi usemi halisi (alama 2) Watoto waliambiwa na mama yao watakaporudi nyumbani waoge, wale, hala III waanze kusoma moja

kwa moja badala ya kuharibu wakati wao kwa kutazama vipindi vya runinga. Aliwakumbusha kuwa wanaofanya maonyesho kwenye runinga tayari wamefuzu shuleni na wameaj iriwa kazi.

(h) (i) Taja vihusishi vitatu vinavyorejelea mahali, wakati na kiwango

(alama3)

(ii) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya kila kihusishi

(i) Andika sentensi zifuatazo upya kwa kufuata maagizo

(i) Alicheza kwa bidii akawafurahisha wengi waliohudhuria tamasha hizo

Anza kwa: Kucheza

(ii) Karamu hiyo ilifana sana, kila mtu alikula chakula akatosheka Anza kwa:

Chakula

(j) Tunga sentensi mbili tofauti ukitumia vitenzi hivi vya silabi moja

(i) Pa ________________

(ii) La

(k) Unda vitenzi kutokana na maj ina haya:

(i) Mtukufu ______________

(ii) Mchumba

# ISIMUJAMII

**1.** ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata:-***

Niaje wasee! Ma-holiday ndizo hizo tena. Najua ma-mission ni mingi! Lakini jo,

mambo imebadilika ! Ni kubaya maze. Usifikirie kila kitu unaona ni reality, ukadhani ni gold !
Hiyo siyo real life maze ! Round hii maze ni ‘‘Ku-chill!’’ Usipige ma-stunts zingine zitakuacha uki-regret later! NI POA KU- CHILL au aje maze?

a) Bainisha rejista ya mazungumzo haya
b) Kwa kurejelea kifungu andika sifa za rejista hii.
c) Kwa nini watu hutumia lugha zaidi ya moja.
d) Orodhesha hatua tatu zinazoweza kuchukuliwa kusuluhisha matatizo yanayokumba Kiswahili nchini.

2. ***Soma mzungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali :***

**A** : Ohh, dada Naomi
**B** : Dada Ruth (anamsogea kwa bashasha wanakumbatiana). Ahh Mungu asifiwe!
**A**: Asifiwe sana
**B**: Ehh dadangu, miezi ...mingi...sijakuona
**A**: dada wee...Nilitumwa huko kusini ...Kuwahubiria watu injili (mtuo mdogo)singeweza kukata...
**B**: Ehh, usiwe kama Yona
**A**: Habari ya siku nyingi?
**B**; Nzuri Mungu bado ameendelea kunibariki
**A**: Amen!
**B**: Nimeendelea kuiona neema yake
**A**: Amen! Asifiwe Bwana
**B**: Halleluya
**A**: Ni Mungu wa miujiza!
**B** : Amen. Hata nami nimeona neema yake
Bado niko imara katika wokovu katika siku hizi za mwisho
**A** : Amen !
**B** : Ni Mungu wa ajabu kweli !
**A** : Nilikumbana na matatizo lakini nikategemea sala
Kama Paulo na sila… Na nikashinda (anatua). Sikuweza kumpa shetani nafasi…maana ameshindwa
**B** : Ameshindwa kabisa

<u>**Maswali**</u>:-
(i) Hii ni sajili ya wapi ? Fafanua
(ii) Taja na ueleze sifa za sajili hii
(iii) Taja na ueleze mambo **mawili** muhimu yaliyosaidia katika maenezi ya Kiswahili Afrika mashariki na kati

3. Bw. Mosuka : Mheshimiwa spika, naichukua fursa hii kuipinga hoja iliyowasilishwa na mbunge wa Mahira, mheshimiwa Kochaberi kuhusu suala la kuavya....
(a) Hii ni sajili gani?
(b) Eleza sifa za mazungumzo ya sajili hii

4. **ISIMUJAMII**

**(a) Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata** (alama 10)

A: Habari yako ndugu

B: Ndugu…… Ahh! (Anamsogelea) Bwana asifiwe!

A: Asifiwe sana ndugu!

B: Amen! Ahh ndugu yangu, imekuwa vipi umepotea hivyo?

A: Usiwe ha hofu ndugu. Nilikuwa nimeenda kuhubiri huko Nakuru. (Anatua kidogo).

Ilinibidi niende huko, ili kutimiza amri ya Bwana.

B: Eeh, hata Yohana aliendа kuhubiri ……………

A: Habari ya siku nyingi?

B: Nzuri, Bwana ameendelea kunineemeshea baraka zake

A: Amen!

B: Nimeona mkono wake katika kila jambo

A: Amen! Asifiwe Bwana

B: Amen

A: Ameendelea kunibariki sana. Shetani hana nafasi katika maisha yangu

B: Shetani ashindwe

A: Ashindwe Ibilisi.

**Maswali**

i) Toa muktadha wa mazungumzo haya. (alama 1)

ii) Taja sifa zozote mbili zilizojitokeza katika mazungumzo haya. (alama 2)

iii) Huku ukitoa mifano mitatu onyesha tofauti iliyoko kati ya mazungumzo haya na mazungumzo yanayoweza kutokea mahakamani. (alama 3)

b) atatizo ya lugha katika matamshi yafuatayo yanasababishwa na nini? Andika lugha sanifu

(i) Nipeko jai nikunyenge wakati nikikungojeanga (alama 1)

(ii) Tsambi sangu sote simeoswa na tamu ya Yesu. (alama 1)

(iii) Alienda kukojoa baada yake kuhara. (alama 1)

iv) Mimi ninakuja kwa hapa. (alama 1)

5. Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.

“Karibu wageni karibuni

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Come and learn with us lugha ya kiswahili.

Nyote mtabenefit sana"

"Kwa nini?"

"Kwa sababu its a national language"

a) Lugha ngapi zimetumika katika muktadha huu?

b) Mtindo wa kutumia lugha zaidi ya moja katikia mazungumuzo huitwaje?(alama2)

c) Eleza sababu za wazungumzaji kutumia lugha zaidi ya moja. (alama5)

d) Mzungumzaji mwenye uwezo wa kutumia lugha zaidi ya mbili anaitwaje?(alama2)

6.(a) Jadili sifa tatu kuu za lugha ya taifa. (alama 3)

b) Eleza majukumu saba ya lugha za taifa. (alama 7)

## 7. ISIMU JAMII

"Bwana mdogo," alisema kwa sauti ya kite.

'Naam Doctor,' Nikajibu.

'Leo wasikiaje?'

'Nafeel poa'

'Unafanya kazi gani?'

'Nasukuma rukwama'

'Eeh! Bwana, kama watakwa kuishi,acha hiyo kazi ya suruba, unasikia?'

'Ndiyo Doctor"(kisha akanipimapima kwa kifaa alichokuwa nacho…..)

'Leo!' Aliniambia huku akisimama wima na kuchezeshachezesha kifaa chake mkononi,

"N'takuruhusu kwenda nyumbani.Wapaswa kupumzika kwa mwezi mzima pasi kufanya lolote zito."

'N`takupa vidonge vya kumeza.'

'Asante Doctor ,' Nikamshukuru.

## Maswali

a) Mazungumzo haya yako katika rigista gani? (alama 1)

b) Taja lugha zilizotumika katika mazungumzo haya (alama 2)

c) Fafanua sifa za sajili hii (alama 3)

d) Eleza dhima za lugha ya Taifa (alama 2)

e)Taja na ueleze matatizo mawili yanayoikumba lugha ya Kiswahili. (alama 2)

**8.Taja na ueleze** njia tano zinazochongia maenezi ya lugha ya Kiswahili nchini.

(alama 10)

# USHAIRI

1. Alipokwenda kwao, mamaye alimwambia,

Nipa fedha au nguo, nataka kwenda tumia!

Nikosapo hivi leo, nipa kisu tajitia !

Huzunguka akilia kwa maana ya uketo

Ndipo mamaye kawaza, pamwe na kuzingatia,
Fedha zako umesoza, na leo zimekwisha,
Kisu sikukukataza, twaa upate jitia!
Mbele zangu n'ondokea! Wende na ukiwa wako!

Ulipogeuka nondo, nguo ukazingilia,
Kakaka kwa vishindo, usisaze hata moya,
Leo wanuka uvundo, wambeja  wakukimbia!
Mbele zangu n'ondokea ! Wende na ukiwa wako!
Ukijigeuza nyama, kama Simba ukilia,
Watumwa ukawaegema, ukawla wote pia,
Pasi kuona huruma, kutoa wahurumia,
Mbona hukuzingatia? Wende na ukiwa wako!

Si mimi naliokupa, **ukata** huo, sikia!
Kwamba utakuja hapa, nipate kuondolea,
Naapa thama, naapa, sina la kukutendea!
Mbele zangu n'ondokea! Wende na ukiwa wako!

Tamati, nalikomile, ni hayo nalokwambia,
Hapahitaji kelele na kujirisha mabaya,
Na kwamba yakutukie, sema yapate n'elea!
Zidi radhi kuniwea ! Wende na ukiwa wako!

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka

(b) Ni maudhui gani yanayojitokeza katika shairi hili

(c) Taja na ueleze tabia za mnenewa katika shairi hili

(d) Mshairi ametumia uhuru wa utunzi. Taja sehemu mbili alikotumia uhuru huo

(e) Eleza umbo la shairi hili

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi :-

(i) Uketo

(ii) Ukata

2. . ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Msituni nikakuta, nyuki wamo mzingani,
Kwa juhudi wanakita, mara nje mara ndani,
Husuda wameikata, hata hawasengenyani,
Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja

Mchwa nao nikaona, wamejenga masikani,
Wafanya bidii sana, uvivu hawatamani,
Wao husaidiana, tena hawadanganyani,
Mchwa wadudu wa chini, wanaishi kwa umoja

Nalo jeshi la siafu, hutandawaa njiani,
Laenda bila ya hofu, maana ajiamini,
Silaha zao dhaifu, meno, tena hawaoni

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Wa kuwatadia nini ? Kwani wanao umoja.

Nao chungu wachukuzi, nyama warima njiani,
Masikini wapagazi, mizigo yao kichwani,
Ingawa si wachokozi, wakali ukiwahini,
Katu hawafarakani, wanadamu kwa umoja.

Sisi ni wana Adamu, mbona hatusikizani,
Tusitietie hamu, ukubwa kuutamani,
Wachache wataalamu, tuwasadi kwa imani,
Hii "Huyu awezani," yatuvunjia umoja

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka.

(b) Ni sifa zipi nne zinazopewa wanaozungumza.

(c) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia uhuru wake katika shairi hili.

(d) Eleza muundo wa shairi hili.

(e) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari.

(f) Taja mafunzo mawili unayopata kutokana na wahusika wanaozungumziwa.

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hilo.

(i) Chungu

(ii) Tuwasadi

3. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Twamshukuru Mwenyezi. Kamwe wingi ukarimu
Alo na kiti cha enzi, Mola wetu akramu
Kutupa kitu azizi , lugha kutakalamu
Lugha ni kitu kitamu, ujuwapo kutumia

Lugha mkuu mlezi , aleaye binadamu
Hata wanyama ja mbuzi, wema lugha wafahamu
Hafuguwa simulizi, izaayo tabasamu
Lugha huwa ni imamu, ujuwapo kutumia

(3) Lugha hodari mkwezi, akweaye tata ngumu
Huzifyeka pingamizi, zizushazo uhasama
Ikazidisha mapenzi, wapendanao kudumu
Lugha huyeyusha sumu, ujuwapo kutumia

Lugha ndiye mpagazi, mazito kuyahudumu
Pia hupanga vizazi, pasi mbari kudhulumu
Aidha hufanya kazi, ikawa mustakumu
Lugha kwayo ni timamu, ujuwapo kutumia

Lugha ni mpelelezi, maovu kuwakasimu
Huwatowa palo wazi, kashuhudia kaumu
Yasifiwa na wajuzi, kuwa ni kitu adhimu

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

Lugha mkuu hakimu, ujuwapo kutumia

Lugha huizuwa kazi, kutatiza mahakimu
Huwaacha kanwa wazi, wakili kitakalamu
Muhalifu na jambazi, wakaishinda hukumu
Urongo huwa timamu, ujuwapo kutumia

Lugha iwe ni kiongozi, Kizungu au Kiamu
Iwekapo waziwazi, silabi na tarakimu
Huyakimu maongezi,yakasikizwa kwa hamu
Lugha huwa ni muhimu, ujuwapo kutumia.

Lugha ni mapinduzi, wanyonge na wajukumu
Kadhalika ni jahazi, ya nahodha muhitimu
Kufa maji haiwezi, si vina si miizamu
Lugha maji zam-zamu, ujuwapo kutumia

**Maswali.**

Eleza maudhui ya shairi hili

Eleza muundo wa shairi hili

Andika ubeti wa nne katika lugha ya nadhari/ nadharia

Taja huku ukitoa mifano, mbinu tatu za lugha alizotumia mshairi kuwasilisha ujumbe

Eleza maana ya msamiati kama ulivyotumika

Azizi

Uhasimu

Adimu.

4. ***Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali :-***

**SHAIRI A:**

Tunda la elimu zote, wasema wanazuoni,

Ni kwamba mtu apate, kumtambua manani.

Ndipo hadhi aipate, akumbukwe duniani.

Elimu bila ukweli, haizidi asilani

Giza na nuru muhali, katu havitengamani,

Uwongo uje kwa ukweli, itue nuru moyoni.

Elimu ni kama mali, haichoshi kutamani,

Ni bora yashinda mali, taji la wanazuoni,

Elimu njema miali, iangazayo gizani.

Mtu hachomwi na mwiba, na viatu mguuni,

Ulimwengu una miiba, tele tele majiani,

Elimu ukiishiba, U salama duniani.

Wafu ni wasiosoma, watazikwa ardhini,

Hai ndio waulama, wapaao maangani,

Elimu jambo adhima, aso nayo maskini

Elimu ina malipo, utayalipwa mwishoni
Pale uitafutapo, ujira usitamani
Mwanachuoni afapo, mbingu huwa na huzuni.

Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachuoni,
Wao wameongolewa, na ni taa duniani.
Kweli wanapojua, watoe bila kuhini.

Elimu bila amali, mti usio majani,
Haumtii kivuli, aukaliaye chini,
Inakuwa mushkeli, wa kushuri insani,

**SHAIRI B**

Inakera moyo
Hii anga ambayo
Huwasonya njiani
Watokao mashambani
Wa kusalimu kwa bashasha
Wanaoshinda kivulini.

Chini ya mwembe
Wa umma.

Inakera moyo

Hii sebule ambayo

Huwahini mezani

Wagotao nyundo kutwa

Wa kukabili chakula

Wanastarehe daima

Chini ya paa

La umma.

**<u>Maswali</u>**

(a) Pendekeza kichwa kifaacho kwa kila shairi la A na B

(b) Haya mashairi ni ya aina gani?

(c) Taja sifa zozote **tatu** za kishairi katika shairi B

(d) Taja mbinu ya lugha iliyotumiwa :-

(i) Katika mshororo wa mwisho wa ubeti wa saba katika shairi la A

(ii) Katika ubeti wa nne wa shairi la B

(e) Fafanua kwa mukhtasari maudhui ya mashairi yote mawili

(f) Andika ubeti wa mwisho wa shairi la A katika lugha nathari

(g) Taja na uonyeshe jinsi idhini ya ushairi ilivyotumika katika shairi la A

(h) Fafanua maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi:-

(i) Maulama

(ii) Wameongolewa

(iii) Wagotao

[iv] Huwahini

**5.Soma shairi hili kisha ujibu maswali.**

Jicho, tavumiliaje, kwa hayo uyaonayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo
Kwacho, lijalo na lije, nimechoka vumiliyo
Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhi tuyasikiayo
Nayo, visa na mauko, wanyonge wayakutayo
Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo
Naandika!

Hawa, wanotulimiya, dhiki wavumiliayo
Hawa, mamiya mamiya, na mali wazalishayo
Hawa, ndo wanaoumiya, na maafa wakutayo
Naandika!

Hawa, sioni wengine, kwao liko angamiyo
Hawa, uwapa unene, watukufu wenye nayo
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waikutayo
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo
Bado, tafauti sana, kwa pato na mengineyo
Bado, tuling'owe shina, ulaji pia na choyo
Naandika!

**Maswali**

(a) Shairi hili laweza kuwekwa katika bahari zipi? (alama 4)

FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

Thibitisha kila jibu lako.

(b) Eleza dhamira ya mshairi. (alama 2)

(c) Onyesha mifano miwili ya uhuru wa kishairi jinsi ulivyotumika katika shairi. (alama 2)

(d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 4)

(e) Tambulisha kwa mifano mbinu zozote mbili za sanaa katika shairi. (alama2)

(f) Fafanua sifa za kiarudhi zilizotumika katika ubeti wa tano. (alama 3)

(g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 3)

(i) Zuiliko

(ii) Wavune

(iii) Wenye pupa na Kamiyo.

**6.** ***Soma shairi hili kisha ujibu mawali yanayofuata.***

**SABUNI YA ROHO**

Ewe tunu ya mtima, kwa nini wanikimbia?
Ndiwe suluhu la zama, waja wakukimbilia,
Waja wanakutazama, madeni wakalipia,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mafuta ya roho, walisema wa zamani,
Utanunua majoho, majumba na nyumbani,
Umezitakasa roho, umekuwa mhisani,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Matajiri wakujua, wema wako wameonja,
Nguo zao umefua, wakupata kwa ujanja,
Sura Zao ‘mefufua, Wanazuru kila nyanja,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mvunja mlima, onana na masikini
Watazame mayatima, kwao kumekua wa duni

Wabebe waliokwama, wainue walio chini,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Ndiwe mvunja mlima,wapi kapata uwezo?
Umezua uhasama, waja kupata mizozo,
Ndiwe chanzo cha zahama, umewaitia vikwazo,
Ndiwe  sabuni ya roho, Ndiwe mvunja mlima.

Umevunja usuhuba, familia zazozana,
Walokuwa mahabuba, kila mara wagombana,
Roho zao umekaba, majumbani wachinjana,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Nakutafuta kwa hamu, sabuni unirehemu,
Sinilipue ja bomu, sije kawa marehemu,
Niondoe jehanamu, ya ufukara wa sumu,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

Naondoka wangu moyo, nikuitapo itika
Fulusi wacha uchoyo, tatua yalonifika,
Nichekeshe kibogoyo, nami nipate kuwika,
Ndiwe sabuni ya roho, ndiwe mvunja mlima.

(a) Mshairi anaongea na nani katika shairi hili?

[alama 1]

(b) **Taja** majina mengine matatu aliyopewa huyu anayesemeshwa.

[alama 3]

(c) Anayezungumziwa katika shairi hili amesababisha balaa **gani**?

[alama 2]

(d) Mshairi anatoa mwito **gani** kwa mwenziwe?

[alama 4]

(e) **Fafanua** maudhui ya ubeti wa sita.

[alama 2]

(f) Mbinu kadha za uandishi zimetumiwa na msanii kuwasilisha ujumbe wake.

**Taja** mbinu zozote **<u>tatu</u>** na uzitolee mifano katika shairi.

[alama 3]

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

(g) **Fafanua** maana ya:

Sura zao "mefufua, wanazuru kila nyanja.
[alama 1]

(h) **Andika** ubeti wa saba katika lugha nathari. [alama 4]

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

1. Lau dunia nanena, tuseme si ati ati,
Mauti kawa hakuna, katika wote wakati,
Vipi tungelisongana, tunaoishi tiati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

2. Dunia ingetatana, na kizazi katikati,
Huku kwazaliwa bwana, kule kwazawa binti,
Vipi tungeliona, na kuzaa hatuwati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

3. Lau mauti hakuna, tungesongana sharuti,
Kwa viumbe kukazana, wanadamu na manyati,
Vipi tungelijazana, kwa kusitawi umati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

4. Walakini subuhana, kapanga sisi na miti,
Ili tusizidi sana, si wengi na si katiti,
Maisha ya kupishana, yule ende yule keti,
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

5. Ndipo dunia kufana, ikawa kama yakuti,
Kwa uwezewe Rabana, kaipanga madhubuti,

Maisha kugawiana, kayagawa kwa mauti,
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

6. Njia ingekuwa hapana, pembeni na katikati ,
Sote tungeambatana, pa kulima hatupati,
Na njaa ingetutafuna, pa kulima hatupati,
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

7. Peleleza utaona, hayataki utafiti,
Kama tungelikongana , ingelikuwa ni bahati,
Vipi tungelisukumana, katika hiyo hayati?
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

8. Mbele sitakwenda tena, hapa mwisho nasukuti,
Yaeleni waungwana, shauri yake jabaruti,
Yote tuloelezana, katenda bila senti,
Lau hakuna mauti, vipi tungelisongana?

**MASWALI**

a) Shairi hili ni la bahari gani? (alama 2)

b) kwa kutoa mifano mwafaka onyesha jinsi mtunzi wa shairi hili alivyotumia uhuru wa utunzi (alama 2)

c) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)

c) Andika ubeti wa tano katika lugha nathari. (alama 4)

d) Tambulisha mbinu zozote mbili za lugha zilizotumiwa na mshairi (alama 4)

e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi

i)katiti

ii) yakuti

iii) Hatuwati

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

iv) Nasukuti (alama 4)

## 8.KIFO

1. ‘likuwa tisini moja
‘lipojikunja pamoja
Kutuaga mara moja
Safari moja kwa moja

2. ‘lituachia vioja
Raha hatujaionja
Tumezidi na kungoja
Matumaini ya waja.

3. Kifo hatuna faraja
Baba livuka daraja
‘likuwa wetu kiranja
Majonzi ‘lituachia

4. Maisha ‘mekosa haja
Na mama amejikunja
katwa auma viganja
Nyumba sasa inavuja

5. Vitamu nani taonja
Mali sasa imefuja
Mifupa tutaivunja
Mifugo katu uwanja

6. Kifo kwetu sisi waja
Tumaini hutuvunja
Ingawa ndio daraja
Haituweki pamoja

**MASWALI**

1. Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
2. Mshairi ana ujumbe gani ? (alama 2)
3. Taja mbinu zozote tatu za lugha alizotumia mshairi na uzitolee mifano kutoka shairi.(alama 6)
4. Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)
5. Eleza maana ya mistari hii kama ilivyotumika katika shairi. (alama 2)
    i) Baba livuka daraja
    ii) Kutwa auma viganja
6. i) Mshairi ametumia mbinu gani katika maneno haya . (alama 1)
    ‘likuwa
    ‘lituachia
    ‘lipojikunja

ii) Kwa nini akatumia mbinu hiyo? (alama 1)

**9.** ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yote.***

KIPIMO NI KIPI?

Nitampa nani, sauti yangu ya dhati
Kwa kipimo gani, ingawa kiwe katiti
Amefanya nini, La kutetea umati
Kipimo ni kipi?

Yupi wa maani, asosita katikati
Alo na maoni, yasojua gatigati
Atazame chini, kwa kile ule wakati
Kipimo ni kipi?

Alo mzalendo, atambuaye shuruti
Asiye mafundo, asojua mangiriti
Anoshika pendo, hata katika mauti
Kipimo ni kipi?

Kipimo ni kipi, changu mimi kudhibiti
Utu uko wapi, ni wapi unapoketi
Nije kwa mkwapi, au ndani kwa buheti
Kipimo ni kipi?

(a) **Eleza** umbo la shairi hili Alama 4

(b) **Taja** tamadhaliza usemi na kisha utoe mifano Alama 3

(c) **Taja** na ueleze namna mshairi alivyotumia uhuru wa ushairi? Alama 2

FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

(d) **Eleza** maudhui ya shairi hili? Alama 3

(e) **Andika** ubeti wa tatu kwa lugha nathari Alama 4

(f) **Eleza** msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa Alama 4

(i) Katiti

(ii) Gatigati

(iii) Shuruti

(iv) Mangiriti

# FASIHI SIMULIZI

1. (a) Nini maana ya khurafa/kharafa?

(b) Fafanua sifa **tano** za kharafa

(c) Elezea mbinu **nne** za kutongolea hadithi

2. (a) (i) Ngomezi ni nini katika fasihi simulizi?

(ii) Eleza sifa zozote mbili za ngomezi

(b) Onyesha tofauti kati ya vikundi hivi:

(i) **Hekaya**
**Hurafa**

(ii) **Visakale**
**Visasili**

(iii) **Ngano za mtanziko**
**Ngano za mazimwi**

(c) (i) Vitendawili ni nini?

(ii) Fafanua kwa mifano, mbinu zozote nne za lugha zinazopatikana katika vitendawili

(d) Soma kifungu hiki cha wimbo kisha ujibu maswali yafuatayo :

**Kuumeni** : (Waliimba) Tumeupata mpilipili na maua yake. Chikicha x2
**Kukeni** : (Wimbo wao kwa sauti tofauti)
Tausi waendaa x2
Tausi waenda wamuacha mama kwenye banda
**Kuumeni** : (Wakijibu wimbo) Mwacheni aendee x2

Mwacheni aende akaone mambo ya nyumba

**Kukeni** : Mama ataota nini x2

Ataota nini, hana mtu wa kumletea kuni

**Kuumeni** : Ataota moto wa magunzi, wa magunzi, wa magunzi.

Twamchukua , kisura wetu, kisura wetu, kisura wetu.

Tausi ni wetu, sasa, ni kito chema, ni kito chema ni kito chema.

**<u>Maswali</u>**

(i) Wimbo huu ni wa aina gani na unastahili katika hafla gani ?

(ii) Fafanua ujumbe uliojikita katika utungo huu

3. ***Soma kifungu kifuatacho kisah ujibu maswali yafuatayo :***

(vigelegele vya harusi vililia alilili ; x3)

**Kuumeni** : (waliimba) Tumeupata mpilipili na maua yake chikicha x2

**Kukeni** : (wimbo wao kwa sauti tofauti) Tausi waendaa x2

Tausi waenda wamuacha mama kwenye banda.

**Kuumeni** : (wakijibu wimbo) Mwacheni aendee x2

Mwacheni aende akaone mambo ya nyumba.

**Kukeni** : Mama ataota nini x2.

Ataota nini, hana mtu wa kumletea kuni.

**Kuumen**i : Ataota moto wa magunzi, wa magunzi wa magunzi. Twamchukua, kisura wetu,

kisura wetu, kisura wetu.

Tausi ni wetu sasa, ni kito chema, ni kito chema ni kito chema.

(a) (i) Wimbo huu ni wa aina gani, na unastahili katika hafla gani ?

(ii) Bainisha wahusika Kuumeni na Kukeni

(iii) Fafanua ujumbe uliojikita katika utungo huu

(iv) Wimgo huu una umuhim;u gain hafia ulioimbiwa?

(v) Tambua mtindo uliotumika katika utungo huu

(b) Taja na ujadili aina nyingine **sita** za nyimbo

# MASWALI YA KARATASI LA TATU

1) Eleza ufaafu wa anwani Chozi la Heri

2) Athari ya vita katika nchi ya Wafidhina ni kioo cha bara la Afrika. Jadili

3) Jadili dhana ya chozi katika riwaya ya Chozi la Heri

4) Mwanamke katika jamii hii ametwezwa na kutwazwa jadili

5) Akikosa la mama hata la mbwa huamwa kwa kurejelea methali hii eleza umuhimu wa mashirika ya misaada

6) Jamii ya Chozi la Heri ni taswira ya jinsi ukabila unavyoathiri bara la Afrika

7) Malezi ya watoto katika riwaya ya Chozi la Heri ndicho kitovu cha ufanisi na matatizo yote yanayowapiku watoto

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

8) Utumizi wa afyuni katika jamii umeleta mathara mengi . Thibitisha

9) Jadili athari na dhiki zinazotokana na uongozi mbaya

10) Mla, naye huliwa zamu yake ikifika . kwa kurejelea riwaya ya Chozi la Heri thibisha ukweli wa kauli hiyo

11) Riwaya ya Chozi la Heri imejaa aina mbalimbali za migogoro jadili.

12) Uozo wa maadili na kuvunjwa kwa haki ni jambo ambalo lilikuwa la kawaida katika nchi ya Wahafidhina. Thibitisha

13) Riwaya ya Chozi la Heri ni ya Utamaushi jadili kauli hii

14)

## MASWALI ZAIDI YA MUKTADHA

*Tia dondoo katika muktadha wake*

1) " Njoo nikujuze kwa yule binamu vuuk ambaye hukwambia habari yake kila mara"

2) " Atanguliaje kisimani hunywa maji maenge"

3) " Mlaani shetani"

4) “ Huyu ana imani”

5) “ Umu hawa ni marafiki wangu wa chanda na pete. Ni watu wakarimu na wenye imani’’

6) “ Nashukuru kwa kunielekeza kwa wazazi wetu hawa”

7) Wote wawili walitazamana, kila mmoja akiapa moyoni kuwa amewahi kumwona kiumbe huyu mahali.

8) Kweli mimi nilikuwa sikio la mbuzi ambalo nyanya alizoea kusema husikia chunguni

9) “ Leo waonaje tukiwajaribu mababe wetu? Ni vizuri kuanza mapema kabla ya jua la utosini”

10) “ Mama zenu walienda wapi?”

11) “ peace be with you’’

12) “ Kweli milima ndiyo haikutani”

13) “ Nahisi kama nasimulia kisa kirefu chenye mwisho mwema”

14) “ Si kwamba sijawatafuta hamna kituo cha polisi ambacho sijabisha hodi”

15) “ Haiwezekani! Hili haliwezekani! Itakuwa kama kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike”

## MASWALI YA SIFA ZA WAHUSIKA NA UMUHIMU WAO

Jadili sifa za wahusika wafuato na umuhimu wao;

Ridhaa

Mwangeka


MASWALI YA MBINU ZA LUGHA NA TAMATHALI ZA USEMI

Jadili mbinu zifuatazo zilivyotumika katika riwaya ya Chozi la Heri

- Jazanda
- Taharuki
- Kisengerenyuma
- Barua
- Ndoto
- Kinaya
- Taswira
- Swali balagha
- Sadfa
- majazi

# KIGOGO

FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807



FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807

1. Tamthilia ya ‘Kigogo’ ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika. Thibitisha. (alama 20)
2. “Mguu huu ni wako”
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)
   b) Ni tamathali gani ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. Eleza maana yake (al.2)
   c) Msemewa alipewa ahadi zipi (al. 5)
   d) Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji (al. 9)
3. “Dalili ya mvua ni mawingu, lazima tuwe macho”.
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Bainisha tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
   c) Ushauri uliotolewa na msemaji baadaye kama njia mojawapo ya kuwa macho ni wa kidhalimu. Fafanua. (alama 4)
   d) Eleza namna unafiki wa msemaji na upumbavu wa mnenewa unavyodhihirika katika muktadha wa dondoo hili. (alama
   e) Onesha jinsi ukweli wa kauli hii ulivyojitokeza baadaye katika tamthilia. (alama 4)
4. Jadili migogoro inayojitokeza katika tamthilia ya kigogo, kisha utathmini namna ilivyosuluhishwa. (alama 20)
5. “ Do ! Do ! Simameni ! Simameni leo kutanyesha mawe! “
   **(i)** Eleza muktadha wa dondoo hili. ( alama 4)
   **(ii)** Fafanua mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo (alama 4)

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**

**(iii)** Dhihirisha kwa kuzingatia hoja sita jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika tamthilia ya “ Kigogo.” (alama 12)

6. Eleza kwa kutolea mifano mitano mitano jinsi mwandishi alivyofaulu kutumia mbinu za :
   a) mbinu rejeshi
   (alama 10)
   b) sadfa (alama10)
7. Eleza jinsi mbinu ya taharuki ilivyotumika kufanikisha maudhui katika tamthilia ya kigogo. (alama 20)
8. "Maandamano na migomo ni tatizo sugu katika mataifa yanayoendeleaa." Kwa kurejelea tamthilia ya kigogo, eleza chanzo na athari za maandamano na migomo. (alama 20)
9. Jadili jinsi maudhui ya uzalendo yamejitokeza katika tamthilia ya Kigogo (alama 20)
10. Jadili ufaafu wa anwani "kigogo" katika tamthilia ya kigogo. (alama 20)
11. Mwandishi wa kigogo amewajenga wanawake kwa njia hasi na chanya. Jadili kauli hii kwa kutolea mifano kutoka tamthilia (alama 20)
12. "Wananchi katika mataifa ya Afrika hukumbwa na matatizo ya viongozi wanafiki." Thibitisha kauli hii kwa kutolea mifano kutoka tamthilia ya kigogo. (alama 20)
13. Fafanua jalada la tamthilia kigogo (alama 20)

Kwa majibu ya maswali haya tuma ujumbe ama upige simu kwa nambari 0748842695

Pia kuna maswali na majibu ya tumbo lisiloshiba na chozi la heri

Miongozo ya chozi la heri,kigogo na tumbo lisiloshiba ipo

Ukihitaji matini ya sarufi,isimujamii,ushairi(pamoja na maswali na majibu),fasihi simulizi na insha usisite kunitumia ujumbe nikueleze Zaidi.

# TUMBO LISILOSHIBA

**1 "Shibe Inatumaliza" (Salma Omar Hamad)**

"Ubadhirifu unaotendeka katika jamii unatokana na uzembe na mapuuza ya wanajamii. Onesha ufaafu wa kauli hii kwa kurejelea hadithi: Shibe Inatumaliza

**2. "masharti ya kisasa" (alifa chokocho)**

***"...nataka ujue kwamba mimi ni mwanamke wa kisasa, na mwanamke wa kisasa hutafuta mwanamume wa kisasa."***

(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (Alama 4)

(b) Anayesema haya alikuwa na sifa zipi? (Alama 8)

(ch) Anayeambiwa maneno haya alijua maana ya usasa? Thibitisha. (Alama 8)

**3.** ***"Nasema nizikeni hapa."***

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Taja na uelezee sifa za mnenaji wa dondoo hili. (alama 6)

c) Fafanua maudhui yoyofe matano yanayoshughulikiwa katika hadithi hii, (alama 10)

**4.** a) Mashaka ni jina la kimajazi katika hadithi ya "Ndoto ya Mashaka". Jadili. (alama 10)

a) Onyesha namna asasi ya ndoa ilivyoshughulikiwa katika hadithi hii. (alama 10)

***5."Kumekucha na makuchakucha yake."***

i. Fafanua ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya "Ndoto ya Mashaka" (alama 14)

ii. Eleza umuhimu wa mhusika Mashaka. (alama 6)

6.***"Sekta ya elimu imekumbwa na changamoto katika jamii".*** Fafanua kauli hii ukirejelea diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine. (alama 20)

**7.*'Jazanda inatumika katika hadithi ya "Kidege ".*'** Fafanua. (alama 20)

***8. 'Maudhui ya mapenzi yameshughulikiwa vilivyo katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine.'*** Thibitisha kauli hii. (alama 20)

**9."*Umdhaniye ndiye kumbe siye."*** Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi zozote tano katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine. (alama 20)

10. ***"Kesho kama sote tutaamka salama……….kama tutafungua milango ya nyumba zetu"….***

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili
(alama 4)

(b) Eleza tamathali mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili.
(alama 4)

(c) Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya.
(alama 6)

(d) Hadithi hii inaakisi mambo mengi yanayotendeka katika bara la Afrika.
Taja mambo sita (alama 6)

11 .Ukengeushi huzorotesha maendeleo ya kijamii. Jadili kauli hii ukirejelea hadithi ya 'Mkubwa'. (alama 20)

**12.** Kwa kuzingatia hadithi zozote tano eleza uozo wa jamii kama unavyojitokeza katika tumbo lisiloshiba (Diwani) (alama 20)

13 ***"Kesho panapo majaaliwa. Kesho kama sote tutaamka…….. kama tutafungua milango ya nyumba zetu zinazosimamia juu ya ardhi hii adhimu***…"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili
(al. 4)

b) Eleza sifa nne za msemaji
(al. 4)

c) Taja mbinu zozote mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili
(al. 2)

d) Kwa kurejelea hadithi nzima onyesha namna jamii ya kisasa ina tumbo lisiloshiba (al. 10)

14. ***"Rasta twambie bwana!"***

a) Weka dondo katika muktadha (ala 4)

b) Taja mbinu zilizotumiwa na mwandishi katika dondoo hili (ala 2)

c) Ni kwa vipi mzungumziwa anamchukulia mwalimu mkuu kama hambe? (ala 4)

d) Je, mtihani wa maisha ni amwani faafu ya hadithi hii. (ala 10 )

15. *Usiteketeze umati kama kuni zinavyoteketeza moto.Rudi rudi kwa mola wako.*

a. Eleza muktadha wa dondoo hili.
b. Fafanua sifa za msemewa
c. Tambua tamathali ya usemi iliyotumika hapo juu.
d. Ni kwa nini msemewa anatakikana kurudi kwa mola wake?

**FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657/0770195807**